

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 22 Agosti, 2008

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI
(MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa fedha 2008/2009.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2008/2009.

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI – MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

Taarifa ya Msemadi wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 447

Mgao wa rasilimali fedha na vyandarua

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Kwa kuwa takwimu za Serikali zinaonyesha kuwa, Mkoa wa Singida ni wa mwisho kwa pato la mtu kwa mwaka (*per capital income*) nchini:-

(a)Je, ni vigezo gani vilitumika kwenye kugawanya fedha za MCC za Mheshimiwa Rais George W. Bush takriban shilingi bilioni 700 na kuacha Mkoa wa Singida usipate hata senti moja wakati lengo la fedha hizo ni kupunguza makali ya umaskini?

(b)Je, Mkoa wa Singida ulipata mgao gani kati ya vyandarua milioni tano vilivyoahidiwa na Mheshimiwa Rais Bush?

(c)Je, kwenye mgao huo wa rasilimali fedha na vyandarua, mikoa kwa ujumla ilihuishiwa vipi kabla ya kufikiwa kwa maamuzi yaliyotolewa na kwamba, Mkoa wa Singida usipate na mikoa mingine maskini ipate mgao huo?

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mwongozo wa Spika?

SPIKA: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa William Shellukindo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu swali hili halielekei kama ni la Afya?

SPIKA: Swali hili lina?

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Halielekei kama ni la Afya hili, linazungumzia pato la taifa.

SPIKA: Wajibu wa Serikali ni kujipanga kujibu maswali. Sasa nitaona walivyojipanga, nadhani kama wamepanga wao kwamba lijibiwe na Wizara ya Afya kwa sababu linahusu vyandarua.

Nadhani vyandarua hivi ni vya mbu, kuzuia mbu, siyo vyandarua vya urembo na mambo mengine kama ya MCC fedha zilizo kwenye Sekta ya Afya.

Nadhani tuwaachie Serikali tu watusaidie. Ndiyo, sawa sawa. Nafahamishwa hapa, utaratibu ni kwamba sisi tunapeleka kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu anajua namna ya kupanga mionganoni mwa Waziri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka 2008 kutakuwa na kampeni ya kugawa vyandarua kwa watoto wote walio katika umri chini ya miaka 5. Katika kampeni hiyo mikoa yote ya Tanzania Bara itahusika, ukiwemo mkoa wa Singida. Hakuna Wilaya, Kata wala Kijiji ambacho hakitakuwa kwenye mpango huo wa kupata vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu.

(b) Mheshimiwa Spika, fedha zitakazotumika katika kampeni hii ya vyandarua zimechangiwa kutoka maeneo makuu matatu ambayo ni Benki ya Dunia (*World Bank*) asilimia 38%.

Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria yaani *Global Fund* asilimia 58%, pamoja na mfuko wa Rais Bush wa Marekani wa kupambana na ugonjwa wa malaria, (PMI) asilimia 5%.

Jumla ya vyandarua milioni 7.2 vinatarajiwa kusambazwa katika kampeni hii, ili kuhakikisha kuwa watoto wote walio chini ya umri wa miaka mitano, wanapata vyandarua bora ili kujikinga na ugonjwa wa malaria amba unahatarisha zaidi maisha yao.

(c) Mheshimiwa Spika, Mikoa yote kwa ujumla inahusika katika kampeni hii na imehusishwa kutambua idadi ya watoto chini ya miaka mitano na hakuna mkoa ulioachwa ukiwemo Mkoa wa Singida.

MHE. JOHN P. LWANJI: Ahsante Mheshimiwa Spika. Swali hili nililiwasilisha muda mrefu na nilitarajia kwamba lingapata majibu ya kina kwa sababu awali tuliambiwa kwamba malengo ya mfuko huu ilikuwa ni kwenda kuhuishia barabara zetu, mambo ya miundombinu, umeme pamoja na afya kwa maana ya UKIMWI na vyandarua. Lakini ninaona Serikali imetoa jibu kwa ajili ya swali namba (b).

(a) na (c) limeachwa kabisa. Sasa ningelipenda kujua Mkoa wa Singida umepata nini kwa sababu Mkoa wa Singida barabara zake za ndani ni mbaya sana na hasa hii barabara ya kutoka Itigi, Chunyu mpaka Mbeya pamoja na barabara hii ya kutoka Manyoni Kiheka na kwenda mpaka Isanza. Sasa ningelipenda nipaye majibu ya uhakika kwamba sisi tunaishia vyandarua tu?

Halafu utaratibu huu uliotumika katika kujibu swali je, hii si ni njia ya kukwepa maswali ya msingi? Naomba majibu.

SPIKA: Hakuna linalokwepwa hapa. Msisitizo wako wewe Mheshimiwa katika swalii lako ni vyandarua si yako hapa, yako (b) na (c). Kwa hiyo hakuna kilichokwepwa hapa.

Hii pia iwasaidieni namna ya kuuliza swalii, ukiweka msisitizo kwenye jambo, hilo ndilo litachukuliwa. Sasa (b) na (c) yote ni vyandarua. Ni (a) tu ndiyo umesema juu ya Singida sipati hata senti moja. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa majibu.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba niongeze majibu kufuatana na swalii la Mheshimiwa Lwanji, ningependa Bunge lielewe kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imekuwa na uhusiano na juhudi za Rais Bush kabla hata waliposaini *MCC* alipokuja hapa nchini na *MCC* aliyoizungumzia Mheshimiwa Lwanji kusema kweli inakwenda kwenye barabara, maji na vitu kama hivyo, sisi tuna uhusiano na Mfuko wake unaitwa *Presidential Malaria Initiative* ambao ulikuwepo kabla ya *MCC*.

Kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Lwanji aulize swalii kuhusu *MCC* itakwenda kwenye Wizara ambayo inahusika ambayo sisi nadhani hatupati senti hata moja. Ahsante sana.

Na. 448

Hospitali ya Wilaya ya Muheza

MHE. NURU AWADHI BAFADHILI aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Muheza haina hospitali ya Wilaya, bali inategemea huduma kutoka hospitali Teule ya *Mission*:-

Je, ni lini Serikali itaiangalia kwa jicho la huruma Wilaya hiyo ili kuwa na hospitali ya Serikali?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla na baada ya uhuru, Serikali imekuwa ikishirikiana na taasisi za dini na zisizo za kidini kutoa huduma za afya. Kwa kuzingatia misingi ya ushirikiano huo Serikali haikuona ulazima wa kujenga hospitali nyingine katika maeneo ambayo tayari kulikuwa na hospitali za taasisi au mashirika ya dini. Hospitali hizo zimepewa hadhi katika maeneo husika kulingana na mfumo wa utoaji wa afya nchini. Serikali huingia makubaliano na wenye hospitali hizo ili kutoa huduma kwa niaba ya Serikali katika maeneo yao. Hivi sasa Serikali inatumia hospitali 23 kama hospitali

teule za Wilaya ikiwemo hospitali ya Muheza, Hospitali moja kama Hospitali Teule ya Mkoa (Dar es Salaam) na Hospitali mbili za Rufaa (*KCMC* na Bugando).

Hali hii inaboresha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi inayopewa umuhimu mkubwa sasa ulimwenguni pote. Jukumu la Serikali kwa hospitali hizi ni kutoa fedha zote zinazohitajika kuendesha hospitali. Hii ni pamoja na mishahara, dawa, vifaa na fedha kwa matumizi mengine ya kila siku. Halmashauri za Wilaya zina jukumu la kusimamia huduma katika hospitali Teule za Wilaya/Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inazihudumia hospitali teule za Wilaya kama hospitali za Serikali na kwa kuwa utaratibu uliopo Wilaya moja haiwezi kuwa na hospitali mbili za Wilaya, tunadhani haitakuwa vema kujengwa hospitali nyingine ya Wilaya ya Muheza kwa sasa.

Naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuhimiza ushirikiano huu, hasa sasa ambapo Serikali inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Katika Kijiji ambapo tayari kuna Zahanati ya Shirika la Dini au binafsi kusiwe na haja ya Halmashauri kujenga Zahanati nyingine na vile vile vituo vyatya afya. Halmashauri ifanye makubaliano na wamiliki wa vituo hivyo ili vitoe huduma kwa niaba ya Halmashauri. Wizara imeandaa utaratibu wa makubaliano hayo yaani (*Service Agreement*).

MHE. NURU AWADHI BAFADHILI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake aliyonipa. Lakini ingawaje tunatakiwa kuwa kwenye hospitali teule kusiwe na vituo vyatya afya. Kwa kuwa katika Wilaya ya Muheza, Wilaya imepanuka sana, watu ni wengi na katika hospitali teule ya Muheza wanakuwa wanarundikana kiasi cha kuwa huduma inakuwa ni ndogo.

Je, Serikali inafikiriaje kutumia majengo ya zamani yaliyokuwa hospitali ya Mbaramu kufanya ni kama ni kituo cha afya cha Muheza. (*Makofifi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza niweke kumbukumbu vizuri katika *Hansard* nimesema, sikusema kwamba mahali pana hospitali teule pasiwe na vituo vyatya afya. Nimesema mahali ambapo pana hospitali teule au vituo vyatya afya basi isirudie sehemu ile itafutwe sehemu nyingine kujengwa. Nilitaka niliseme hilo kuweka kumbukumbu vizuri.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nakubaliana kwamba hospitali teule inafurika kwa sababu haina hospitali anayoidai Mheshimiwa Mbunge, lakini vile vile vituo vyatya afya pale ni vichache. Mheshimiwa tumekuwa tunawasiliana na Halmashauri na vile vile tunazungumza na Wabunge kwamba jukumu la kujenga vituo vyatya afya ni jukumu la Halmashauri husika.

Lakini vile vile hakutakuwa na tatizo kama Halmashauri yenyewe itaona ile hospitali iliyokuwa ya zamani Mbaramo kama wakikifanya kituo cha afya hakutakuwa na

tatizo ili mradi waboreshe majengo na waongeze zile huduma muhimu na sisi kama Serikali tutawasaidia kupeleka wafanyakazi na vifaa vya tiba kama ilivyo kawaida katika sehemu nyingine tunavyofanya. Ahsante sana.

Na. 449

Mfereji wa Bungoni

MHE. MUSSA A. ZUNGU aliuliza:-

Kwa kuwa mfereji wa Bungoni, Wilaya ya Ilala unaopakana na jimbo la Ukonga unapokea maji ya mvua toka barabara kuu za *TANROADS* na kwa kuwa mfereji huo ni mkubwa na wakati wa mvua huleta mafuriko na ajali kwa wakazi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza upya mfereji huo na hasa ukiwa ndio njia pekee ya maji ya mvua toka *Nyerere Road*?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfereji wa Bungoni umekuwa ukipokea maji ya mvua kutoka eneo la kiwanda cha KIUTA na eneo la *Quality Group* katika barabara ya Nyerere ambayo ni barabara ya *TANROADS* kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Vile vile maji ya mvua yanayokusanyika kutoka kwenye mifereji mipya ya mradi wa barabara za *Community Infrastructure Upgrading Programme (CIUP)* na maeneo ya makazi ya Bungoni, Ilala, Buguruni huingia kwenye mfereji huu wa Bungoni ambaa kwa wingi wa maji yanayokusanyika ni mdogo kuyahimili.

Aidha, takataka ambazo zinatupwa kwenye mfereji na wakazi wa maeneo hayo zimekuwa zikichangia pia kuziba kwa mfereji na kusababisha mafuriko.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuoina tatizo hilo, mwaka wa 2006 ilimteua Mhandisi Mshauri kufanya uchunguzi wa tatizo hilo na baada ya uchunguzi wake Mhandisi Mshauri alipendekeza mambo yafuatayo:-

(i) Ujenzi wa makalvati makubwa mawili ya kuvusha maji barabara ya Nyerere eneo la *Quality Group* linalotazamana na eneo la kampuni ya *UNICO*;

- (ii) Ujenzi wa mfereji mkubwa zaidi wa chini ya ardhi wenye urefu wa mita 338 utakaoanza kando kando mwa barabara ya Nyerere na kujengwa chini ya barabara nyembamba hadi kukatiza reli iendayo Bara kutokea Dar es Salaam;
- (iii) Ujenzi wa mfereji wa wazi mpana zaidi ya uliopo kuanzia relini ambapo ule mfereji wa chini ya ardhi utakomea; hadi kukatiza barabara ya Uhuru eneo la Bungoni ambapo mfereji utaingiza maji katika bonde la Msimbazi; na
- (iv) Ujenzi wa *Box culvert* kuvuka barabara ya Uhuru mahali ambapo mfereji unavuka barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi huo kwa sasa zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 2.3 fedha ambazo Serikali inazitafuta ili kutengeneza mifereji hio.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha hizo, Wizara yangu ya Miundombinu kuititia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Dar es Salaam imekuwa ikifanya usafi mfereji wa chini ya ardhi pamoja na makalvati yaliyopo katika barabara ya Nyerere ili kuwezesha maji kupita kwa urahisi. Napenda niishauri Manispaa ya Ilala kusimamia usafi wa maeneo hayo ili kupunguza takataka ngumu katika mfereji huo.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Tatizo kubwa ambalo limejitokeza na kero ambayo wananchi wanapata, mvua zinapokuja zaidi ya wiki tatu, wananchi wanashindwa kukaa katika nyumba zao na tatizo lenyewe linatokana na mradi huu wa *CIUP* ambao umeboresha maeneo ya Buguruni na Kiwalani.

Mheshimiwa Spika, wameweka mifereji mipyä, lakini maji yanamwagikia katika mfereji wa zamani na hii kwa kweli inawanyima raha wakazi wa Bungoni. Tumefanya jitihada binafsi za kuzungumza na watu wa *CIUP* wamekubali kutazama tatizo hili kuwa na wao labda waurekebishe mfereji ule. Je, Serikal iko tayari kutuunga mkono kusaidiana na sisi ili tuweze kukamilisha zoezi hili na *CIUP*?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana naye kabisa Mheshimiwa Mbunge juu ya ukubwa wa tatizo hili na ndiyo maana Serikali imefanya utafiti huo na kubainisha kiasi cha fedha zinazotakiwa na katika kutatua tatizo hilo. Nataka tu nimhakikishie katika hili tuko pamoja na tutakuwa tayari kusaidiana kutatua tatizo hilo kwa kadri fedha zitakapokuwa zinapatikana.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wizara hiyo hiyo, swali refu sana ukurasa mzima linaloulizwa na Mheshimiwa Abdul Marombwa wa Kibiti.

Na. 450

Kutengeneza gati katika Bandari ya Nyamisati

MHE. ABDUL J. MAROMBWA aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mafia pamoja na Wilaya ya Rufiji (eneo la *DELTA*) wameamua kutumia bandari ya Nyamisati iliyoko Wilaya ya Rufiji badala ya ile ya Kisiju iliyoko Wilaya ya Mkuranga ili kusafirisha abiria na mizigo yao na kwa kuwa, hali ya gati iliopo sasa haina uwezo wa kupokea boti au mashua zaidi ya moja kwa wakati na kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imeanza kutengeneza gati hii kwa kiwango kidogo kutokana na ukosefu wa fedha.

(a) Je, Serikali iko tayari sasa kuunga mkono jitihada za Halmashauri ya Wilaya ili kuweza kukamilisha ujenzi wa gati hiyo inayogharimu zaidi ya shs. 100,000,000/=?

(b) Kutokana na ongezeko kubwa la magari ya mizigo yanayopita kwenye barabara inayoelekea katika gati hiyo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango angalau cha lami nyepesi ili iweze kupitika bila matatizo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Miundombinu, majibu kwa swali lile refu kushinda yote kwa leo nadhani.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Mafia na Rufiji kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia bandari ya Kisiju, Wilayani Mkuranga ambayo iko chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari (*TPA*), kusafirisha abiria na mizigi yao.

Eneo la Nyamisati lililoko Wilayani Rufiji ambalo wananchi wanatumia sasa, halipo katika orodha ya bandari zinazosimamiwa na Mamlaka ya Bandari (*TPA*) kulingana na Sheria ya Usimamizi wa Bandari (*The Ports Act*) ya mwaka 2004.

Hata hivyo, kutokanana hali iliyojitokeza ya wananchi kuhamia Nyamisati, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, Serikali imeliona hilo na kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*), inafanya utafiti sasa wa tatizo la gati iliyopo Nyamisati ili kushauri hatua zinazopaswa kuchukuliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara, Mkoa wa Pwani imekuwa ikifanya matengenezo kila mwaka barabara toka Bunju hadi Nyamisati ili iweze kupitika bila matatizo. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali kupitia *TANROADS* imetumia jumla ya fedha, shilingi milioni 59 kwa ajili ya kufanya matengenezo mbalimbali kwenye baadhi ya maeneo katika barabara hii na katika mwaka huu wa fedha 2008/2009, barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 90.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti, kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga barabara hii kwa lami nyepesi ambayo kusema kweli lami hii pia haihimili magari makubwa kama itatakiwa itumike kwa ukamilifu unaostahili. Wizara yangu itaendelea kufanyia matengenezo kila mwaka kuhakikisha kuwa inapitika vizuri kwa kadri Bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa utafiti huu unaofanywa na Mamlaka ya *TPA* haujulikani utakamilika lini. Nilikuwa naiomba Serikali itoe muda kwamba utafiti huu utakamilika lini?

Swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji tayari imeshaandaa *bioque* kwa ajili ya upanuzi wa gati hii. Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuitumia bioque katika utafiti huo na niwakabidhi leo hii? Nashukuru Mheshimiwa Spika.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba nishukuru jitihada za wananchi wa Wilaya ya Rufiji kwa kuanza jitihada hizo za kutaka kujenga hiyo bandari ya Nyamisati. Lakini kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba baada ya kutambua hilo tumeanzisha huo utafiti ambao unafanyika kusema kweli si kwa bandari hii tu ni katika bandari zote nchini ambazo zoezi lake litakamilika Desemba 2008 yaani mwaka huu. Kwa hiyo, kutokana na utafiti huu tunaofanya nadhani tusubiri ushauri wa utafiti utakapokuwa umepatikana ndipo sasa ushauri anaoutoa Mheshimiwa Mbunge wa kutukabidhi hilo zoezi ambalo wameshaanza kulifanya tunaweza tukaupokea.

MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH: Ahsante Mheshimiwa Spika. Ni kweli kwamba sasa hivi wananchi wa Mafia upande wa abiria tunatumia bandari ya Nyamisati lakini bado tunatumia kwa kusafirisha mizigo katika bandari ya Kisiju. Lakini shughuli hizo zote huwa hazifanyiki kwa ufanisi zaidi na kwa uhakika na kwa usalama kwa sababu ya gati la Mafia lenyewe kule tunakotoka bado halijajulikana lini litajengwa. Sasa nilikuwa naomba kumwuliza kwa kuwa mambo yote yameshakuwa tayari na ilikuwa taarifa za ufunguaji wa tenda ufanyike tarehe 22 Desemba mwaka jana. Lakini mpaka leo kimya. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawenza akatuambia ni lini hasa shughuli kamili ya ujenzi wa bandari ya Mafia utaanza ili bandari hizo za Nyamisati na Kisiju nazo ziweze kufanya kazi vizuri zaidi na wananchi wapate usalama wao, wa maisha yao na mali zao?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Niseme tu kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, Serikali ilishatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa hiyo gati ya Mafia, kilichobakia tu ni zile taratibu na mchakato wa kuweza kuanza ujenzi huo na kama alivyosema ye ye mwenyewe, tarehe ya kufungua zile tenda ilikuwa imeshaandaliwa na sasa hivi ndiyo Wizara yangu inafuatilia, wakati wowote zoezi la ujenzi wa gati hiyo ya Mafia utafanyika.

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri

amezungumzia utafiti ambao utafanyika katika eneo zima la maeneo ya pwani kuhusu magati madogo madogo ambayo yanahudumia wananchi.

Je, Mheshimiwa Waziri katika utafiti huo gati la Pangani linahusika kwa sababu tayari Serikali ilikwishaahidi kutoa fedha kulikarabati gati hilo?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane naye tu kwamba huu utafiti tunaoufanya ni kwa nchi nzima na kwa bandari zote na haya magati madogo madogo ni pamoja na hilo la Wilaya yake ya Pangani.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shah alisema kwamba hizi *tender* ilikuwa ifunguliwe Desemba na leo ni Agosti miezi minane baadaye. Hivi Serikali iko *serious* kutoka Desemba mpaka leo miezi minane. Gharama za ujenzi zinapanda, hamwoni kwamba huku kuchelewesha mradi kama huu mnaongeza gharama ambazo ni mzigo kwa Taifa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana kabisa kwamba jinsi tunavyochelewa ndivyo gharama zinavyozidi kupanda.

Lakini niseme tu kwamba wakati mwingine katika hii michakato ya kuanza ujenzi wa shughuli zozote zile za miundombinu kuna vipengele vingine ambavyo vinakuwa ni vya lazima sana mviangalie kwa umakini na kwa hiyo katika ufuatiliaji huo gharama zingine haziepukiki.

Kwa hiyo, nataka tu niahidi kwamba kama nilivyomwahidi Mheshimiwa Mbunge wa Mafia kwamba tutalifuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba ujenzi wa gati ya Mafia unaanza haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Na. 451

Kuboresha Maeneo ya Visiwa

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mikakati mizuri ya kuboresha maeneo mbalimbali ya kiutalii ikiwa ni pamoja na visiwa vya Gozi, Kebere, Bumbile, Kome na Nyabulo.

Je, Serikali itaboresha lini visiwa hivi ili viwe sehemu ya utalii hivyo kuchangia kwenye pato la Taifa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Visiwa vya Gozi, Kebere, Bumbile, Kome na Nyabulo viko katika Ziwa Victoria. Katika kutambua umuhimu wa kuendeleza utalii katika maeneo mbalimbali nchini, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Kagera na Mwanza, ilifanya zoezi la kubainisha vivutio vya utalii na maeneo ya uwekezaji katika Mikoa hiyo. Zoezi hili lilibaini kuwa visiwa vyote vilivyotajwa hapo juu ni makazi ya kudumu na vinatumika kwa shughuli za uvuvi na kilimo.

Aidha zoezi lilibaini kuwa kisiwa cha Kome, kina hifadhi ya msitu wenyewe hekta 2,100. Msitu huu una wanyama na ndege mbalimbali, mapango ya mawe na sehemu ya matambiko ya kabilia la Wazinza. Kisiwa hiki kwa kutumia hifadhi hii ya msitu, kinafaa sana kwa shughuli za utalii ikolojia.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi la kubainisha vivutio kufanyika, ripoti ya vivutio vyote vilivyotembelewa iliandaliwa na ilijumuisha sifa za kila kisiwa kilichotembelewa.

Vile vile mapendekezo ya wataalam kuhusu uendelezaji wa visiwa na vivutio vingine yaliandaliwa. Ripoti ilioandaliwa ilijadiliwa katika kikao cha pamoja na menejimenti ya Mkoa, wawakilishi kutoka Wilaya zote na wadau wa utalii kilichofanyika Mkoani Kagera. Aidha ripoti hiyo pia iliwasilishwa kwenye siku ya utalii duniani iliyofanyika Mkoani Kagera mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kikao hicho cha pamoja kilipendekeza umuhimu wa Halmashauri zote za Mikoa husika kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Ili maeneo yanayofaa kuendeleza utalii yatengwe kwa ajili hiyo, Wizara yangu ilishaonyesha utayari na iko tayari kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri katika kuandaa mipango ya kuendeleza utalii katika maeneo hayo.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuzihimiza Halmashauri za Wilaya za kanda ya Ziwa Victoria kuharakisha mchakato wa kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo ya vivutio yaliyoainishwa ili maeneo hayo yaweze kuendelezwa kwa ajili ya utalii.

MHE. SEVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nakubaliana naye majibu yake pamoja na mkutano uliofanyika katika Mkoa wa Kagera, tarehe hiyo aliyoitaja. Lakini napenda kumfahamisha kwamba mkoa wa Kagera ninavyoufahamu bila nguvu za Serikali kuisaidia si rahisi wenye na Halmashauri zake kuandaa. Kuna kisiwa kimoja cha Lubondo ambacho kina viumbwe vingi ambavyo ni vya ajabu hasa mamba, masato ya ajabuajabu. Je, serikali inaingiza kipato shilingi ngapi na mkoa wa Kagera unafaidika vipi na kisiwa chake hicho?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la nyongeza la dada yangu Mheshimiwa Mwijage, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuendeleza utalii ni jukumu zito ambalo linahitaji msukumo wa kiserikali. Lakini hili jukumu la kupanga matumizi bora ya ardhi ni suala la Halmashauri. Kama tulivyosema kwenye utafiti uliofanyika na wataalamu kwamba maeneo yakishakuwa yamebainishwa yametambulika, hapo sasa Wizara itashirikiana na mkoa katika kuyatangaza.

Katika sekta ya Utalii wadau wakubwa mara nyingi ni sekta binafsi, kwa mafano kwenye takwimu za utalii inaonyesha kwamba zaidi ya 90% ya mapato yanakwenda kwa *private players* kwa maana ya wanaotoa huduma ya usafiri na wanaotoa huduma ya hoteli. Sasa yakishaandaliwa maeneo, maeneo ya kujenga hoteli yakatengwa, sekta binafsi itahamasishwa ili iweke hoteli maeneo hayo. Halmashauri zitaboresha miundombinu ya kuelekea kwenye maeneo hayo.

Lakini kwenye suala mahususi la kisiwa cha Lubondo, takwimu ya mapato yanayopatikana kwa sasa siwezi nikaipata au nikaitoa kwa hapa, lakini kisiwa hiki tumekuwa tukikiendeleza na katika miaka miwili iliyopita *TANAPA* wametenga boti ambayo inasafirisha wageni kutoka kisiwa kidogo cha Kome eneo la Nkome kwenda kisiwani pale. Kwa hiyo, lengo ni kuendeleza visiwa hivi lakini mapato mengine ambayo yamepatikana hadi sasa ni taarifa ambayo nitamwandalia Mheshimiwa Mbunge, baadaye. Niombe tu kwamba tuanze kwanza tuandae huu mpango, tutenge maeneo sisi tuko tayari kuweka nguvu yetu kusaidia mkoa.

SPIKA: Mheshimiwa Maneno, wapi na wapi Chalinze ya Mkoa wa Pwani na Kagera? Lakini swali la nyongeza halafu Mheshimiwa Ruth Msafiri, swali la mwisho la nyongeza. (*Kicheko*)

MHE. RAMADHAN A. MANENO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri; kwa kuwa, hifadhi za taifa kwa maana ya mbuga, ambapo mbuga ya Saadani iliyopo katika Jimbo la Chalinze, Mkoa wa Pwani inaingiza pato kubwa sana kwa Taifa, lakini mahali ambapo inapotokea migogoro kwenye maeneo hayo pato la taifa linapungua kwa maana hata watalii hawawezi kwenda kwenye maeneo hayo kutazama wanyama na kuingiza pato la taifa. Je, Mheshimiwa Waziri, anafahamu kwamba katika mbuga ya Saadani bado kuna migogoro kati ya *TANAPA* na wananchi. Je, yuko tayari kwenda kumaliza tatizo lile haraka iwezekanavyo ili pato la taifa liongezeke?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mhweshimiwa Maneno, Mbunge wa Chalinze, kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hifadhi hii ya Saadani imeanzishwa muda si mrefu sana na hakika panapoanzishwa hifadhi mpya migogoro midogo midogo inayohusu mipaka na mambo mengine yanayohusu sheria za *National Parks* yanajitokeza.

Kwa hiyo, matatizo yaliyoko tunayafahamu na juhudzi za kuyatatuza zinaendelea, *TANAPA* wamekuwa wakizungumza na wananchi kila mara.

Ninaamini kwamba katika muda si mrefu tutaweza kuwa tumetatua matatizo yote. Matatizo yaliyopo hasa yanatokana na ugeni wa zoezi hili au ubadilishwaji wa sheria ambayo sasa inatumika ya *National Parks* ni tofauti na mazingira ambayo yalikuwepo pale nyuma.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo katika swali linaloendelea sasahivi. Kwanza naomba niweke vizuri kwa mujibu wa rekodi, kisiwa hakiitwi Gozi, kinaitwa Gozba.

Mheshimiwa Spika, baada ya masahihisho hayo naomba nishukuru majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tu nipende kusema kwamba kati ya kisiwa cha Kimagi na kisiwa cha Kitua, huwa kuna mapango pale, pengine hilo eneo hajaweza kulifikia kuliona.

Lakini swali langu ninalopenda kuuliza, utalii uko wa aina nyingi ukiwepo wa *sight seeing*, kutoka hivi visiwa viliviyotajwa hapa kutoka Gozba kwenda Kelebe, kwenda Bumbile, kwenda mpaka Nyabulo, ni maeneo mazuri sana ya kutazama hata ukiwa ndani ya maji tu kwenye boti unatembea.

Lakini tatizo kubwa linalokabili visiwa hivi vyote kwa pamoja ni tatizo kubwa la usafiri. Nina hakika kwamba utalii hauwezi ukaimarika bila miundombinu. Na hili ndio tatizo kubwa lililo ndani ya ziwa Viktoria katika visiwa vyake. Je, Serikali itatusaidia kuona kwamba inatusaidia kushirikiana na Wizara hii na Wizara nyingine kuona kuwa inasaidia kuboresha usafiri pamoja na simu ambapo mawasiliano ya simu hayapatikani katika visiwa hivi hasa Kelebe na Gozba ili kuweza kuhakikisha kwamba hizi juhudzi za utalii zitawenza kufanikiwa katika visiwa hivi? Ahsante sana.

SPIKA: Ningejua swali lako la nyongeza ni refu kiasi hiki nisingekupa nafasi lakini, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili. (*Kicheko*).

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana kwa msukumo wake anaouweka katika uendelezaji wa utalii kwenye eneo la mkoa wake. Lakini kama alivyosema mwenyewe katika Suala hili kwamba wadau wa uendelezaji wa utalii ni wengi, mmojawapo ni sekta ya mawasiliano kama alivyosema. Sisi kama watu ambaao tumepeewa jukumu la kuendeleza utalii hakika tupo tayari kushirikiana na wenzetu kuhamasisha wenzetu wa Wizara ya Mawasiliano na bahati nzuri naamini kwamba wadau wa eneo hilo wanasikia, watu wa kampuni za *Zain* na zingine ili wawekeze kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kuboresha mawasiliano.

Kadhalika ni chagishe Halmashauri husika ziboreshe miundombinu hasa usafiri wa majini amba ni wa boti na wenyewe unahitaji kuboreshwa. Sasa nani anatakiwa aboreshe haya ni wadau wote na si Wizara yangu pekeyake. Mimi kwa upande wa Wizara yetu niseme tuko tayari kushirikiana na wenzetu, tuko tayari kuyatangaza maeneo haya lakini sekta binafsi nayo ishiriki kikamilifu katika *worker services* kama *hotels* na maeneo mengine ya Halmshauri ya shiriki katika kuboresha miundombinu.

Na. 452

Mahakama Kutumia Hansard

MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. ZITTO Z. KABWE) aliuliza:-

Je, ni lini Mahakama Kuu ya Tanzania itaanza kutumia *Hansard* kutunza kumbukumbu za Mahakama?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swal la Mheshimiwa Zitto Kabwe Zuberi, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mahakama Kuu divisheni za Mahakama ya Biashara na Mahakama ya kazi wanatumia *Hansard*. Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani mitambo ya *Hansard* imeshafungwa na itaanza kutumika hivi karibuni. Huduma hii itaendelea kusambazwa katika Mahakama zote za Tanzania kadiri Bajeti itakavyoruhusu. Sanjari na uwekaji wa mfumo husika mafunzo haya ya matumizi yake yanatarajiwa kuendeshwa kwa Wahweshimiwa Majaji wote, Mahakimu, Makarani na *Stenographers*.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Ahsante. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuharakisha matumizi ya mitambo hiyo ya *hansard* ambayo tayari imeshafungwa ambayo iliyopo sasa kwasababu *system* iliyopo imepitwa na wakati na tumeambiwa itaanza kutumika hivi karibuni. Hivi karibuni ndio lini?

Mheshimiwa Spika, swal la pili. Amesema huduma hii itaendelea kusambazwa kadiri Serikali itakapopata pesa, yaani kadiri Bajeti itakavyoruhusu. Ina maana Bajeti isiporuhusu huduma hii haitaendelezwa. Je, hakuna *mechanism* nyongine yoyote ya kuwezesha mahakama zetu nchini kuwa na *hansard*?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema *hansard* inategemea Bajeti. Kwa hiyo, jinsi ambavyo Bajeti itakavyoongezwa ndivyo tunavyoweza kufunga mitambo ya *hansard* katika mahakama zetu. Na la pili, mpango mwengine ambao tunao ni chini ya *Legal Sector Reform Program*, kama wafadhili watatusaidia tunaweza kufunga mitambo ya *hansard* katika mahakama mapema iwezekanavyo.

Na. 453

**Ushirikiano Hafifu Kwa Tume ya Haki za Binadamu
na Utawala Bora**

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKAR K.n.y. MHE. MWADINI A. JECHA
aliuliza:-

Kwa kuwa, miongoni mwa changamoto ambazo zinakwaza utendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ni kitendo cha baadhi ya walalamikiwa kutotoa ushirikiano wa kutosha kwa Tume ikiwa ni pamoja na kutojibu hoja za Tume na kutotoa nyaraka zinazohitajika wakati wa uchunguzi wa malalamiko yanayowasilishwa kwao; na kwa kuwa, hali hiyo husababisha uchunguzi kuchukua muda mrefu na kuathiri malengo ya muda mrefu na kuathiri malengo ya Tume ya kutoa haki kwa muda mfupi kadiri inavyowezekana:-

Je, Serikali inachukua hatua gani ya kukabiliana na tatizo hili ili kusaidia kukuza ufanisi wa kiutendaji wa tume hiyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA
NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa kwa sasa kiwango cha ushirikiano kati ya watendaji mbalimbali wanaolalamikiwa na wananchi na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni wa kuridhisha ingawa kuna baadhi ya maeneo machache ambayo yana udhaifu.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalosababisha Tume kutopata haraka majibu kutoka kwa watendaji mbalimbali linasababishwa na Tume kutokuwa na ofisi zake mikoani.

Kwa sasa Tume ina matawi yake Lindi, Mwanza na Zanzibar tu. Hali hii husababisha malalmiko yanayohusu mikoa mingine nje ya matawi hayo na iliyo mbali na Dar-es-Salaam kuchelewa kuleta majibu au maelezo ya malalamiko inayohusu watendaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua tatizo hili Tume inakusudia kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kufungua ofisi ya Kanda huko Moshi, Dodoma na Mbeya. Hatua hii itasaidia kurahisisha ufuatiliaji wa malalamiko katika mikoa iliyoko kwenye Kanda hizo. Mpango huu utatekelezwa hatua kwa hatua kutegemea upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufungua ofisi hizo.

(ii) Tume itaendelea kutoa elimu kwa lengo la kuhimiza watendaji katika Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma na Sekta binafsi juu ya umuhimu wa kujibu na kushughulikia masuala yanayoletwa na Tume.

Mheshimiwa Spika, aidha Tume itaendelea kuendesha mafunzo na semina kwa wahusika wote kuhusu mbinu za kushughulikia malalamiko na umuhimu wa kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Mwanashera Mkuu, lakini naomba nimwulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza. Kwa wale wananchi wanaoishi nje ya Kanda hizi ambazo zimetajwa. Je, anatamka nini kuhusu ufuatiliaji wa haki zao?

Mwanasheria Mkuu, hajui kwamba haki inayoleleweshwa ni haki ambayo inakataliwa? Na kucheleleweshwa kwa haki za wananchi hawa ni sawasawa na kuwakatalia haki zao?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa wale amba wanaishi nje ya sehemu ambazo tumezitaja kwamba ofisi za kanda zitafunguliwa wanapata matatizo katika kufuatilia malalmiko yao. Tume imejipanga kwa kuona kwamba kama ikiwezekana iwafuate wale watu amba wamelalamikiwa ili kuwaomba waweze kukusanya yale maelezo yao kuhusu malalamiko yaliyopelekwa kwao.

Mheshimiwa Spika, la pili. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba haki iliocheleweshwa ni sawa na haki ambayo haitapatikana. Kwahiyo ninamuhakikishia kwamba Tume imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba haki inapatikana haraka iwezekanavyo. (*Makofi*).

Kupeleka Simu za Mezani - Kibakwe

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Kibakwe unakuwa kwa haraka sana, umeme upo, mawasiliano ya simu za mikononi yapo, lakini kinachokosekana ni simu za mezani, *TTCL*, ambazo zingesaidia kuleta Maendeleo kwa haraka:-

Je, Serikali itapeleka lini huduma za simu za *TTCL* kibakwe ili wananchi waweze kufaidika na mawasiliano hata ya *internet* ambayo kwa sasa ni muhimu sana duniani kote?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TTCL* iko katika mchakato wa kutafuta mikopo kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na kupanua wigo wa huduma za mawasiliano nchini. Fedha hizo pia zitaiwezesha *TTCL* kupanua huduma zake katika maeneo inayoyahudumia kwa sasa pamoja na maeneo mapya.

Aidha, upatikanaji wa fedha hizo itaiwezesha kampuni hiyo kufikisha huduma ya simu za mezani na hata huduma za *internet* sio tu kwa wakazi wa mji wa Kibakwe bali wananchi wote wataweza kufaidika na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, mpango wa upanuzi wa mtandao wa kutumia fedha ya mkopo ni wa muda wa miaka mitatu na utaanzia katika miji mikuu na sehemu za biashara ikifuatiwa na mikoa na kisha wilaya. Lengo ni kuhudumia kwanza maeneo yenyewe watu wengi ili kurudisha gharama na kuanza kulipa deni.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *TTCL* inatambua mchakato wa Serikali unaolenga kupata fedha kutoka mfuko wa Mawasiliano kwa wote, *Universal Communication Access Fund*, ambazo pia zitasaidia sana na kwa haraka kujenga mtandao wa mawasiliano usiotumia waya, *wireless*, pamoja na mtandao wa simu za mezani.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri, na nipongeze tu jitihada za serikali katika kusaidia kampuni hii ili iweze kuongeza mtandao wake. Labda tu pengine kwa kuwa Kibakwe ni karibu. Je, Naibu Waziri, yuko tayari twende akaone harakati za kiuchumi ambazo zimeongezeka hivi karibuni baada ya ugunduzi wa madini ya vito vya safaya na shughuli za kiuchumi zinazofanyika pale kwa ujumla pale Kibakwe na Wota siku yoyote kabla ya Bunge hili kumalizika?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninapenda nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Simbachawene na kuwaambia wananchi wa Kibakwe kwamba Mbunge wao yuko mbioni kuhangaikia mawasiliano yao tunawaomba wawe na uvumilivu.

Pili, ni kumhakikishia Mheshimiwa Simbachawene kwamba mimi niko tayari na kama tulivyopanga, kama haitawezekana leo tutakwenda kesho maeneo hayo. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awaweke watu sawa ili tuwaeleze ni nini tunakusudia kufanya katika kuboresha mawasiliano Kibakwe pamoja na Mpwapwa. Namwomba Mheshimiwa Lubeleje, naye tuone huo mnara uliojengwa ambao miaka miwili haujafanyakazi. (*Makofi*).

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, simu za mezani za *TTCL* zinatumia umeme na kwa kuwa kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna vijiji ambavyo kwa mpango wa *MCC* vitapata umeme, vijiji vya Lupeta, Kisokwe, Idilo, Msagali Chunya na Ng’hambi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba kwa kuwa vijiji hivyo vitapata umeme sasa iko haja ya kuvipelekea huduma ya *TTCL*?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyojiba kwamba simu zinahitaji umeme basi tuone kwamba umeme umefikishwa huko Lupeta na vijiji vinginevyo halafu sisi tuwaombe makampuni ya simu ikiwemo *TTCL* waweze kuboresha huduma zao katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge, ameyataja.

Lakini hivi sasa kuna chaja zinazotumia *solar* ambazo zinauzwa hapa ni 30,000/= kwa wale ambao wangependa kutumia kule vijijini, ni vizuri basi Waheshimiwa Wabunge, muwashajihishe wananchi wenu waweze kutumia ili wapate huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, vilevile *internet* inapatikana kwa kutumia simu za mkononi, naomba muitumie nafasi hiyo ili muweze kufanya biashara na kuwafahamisha vilevile wananchi wetu kule kwamba wakitaka taarifa zozote za mazao na kitu chochote wanawenza kukipata kwa kutumia *internet* kwa simu yao ya mkononi. Waitumie huduma hiyo ambayo imo katika simu ya mkononi.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa mji wa Kibakwe unafanana sana na mji wa Mwandoya ulioko kwenye Jimbo la Kisesa. Je,

wakati harakati za kupeleka mawasiliano ya simu za mkononi unaofanywa sasa na Wizara katika Jimbo la Kibakwe, mji wa Kibakwe, utaenda sambamba na upelekaji wa haraka wa mawasiliano ya simu za mkononi ulioko mji wa Mwandoya?

SPIKA: Nadhani ni shida tu zinafanana, lakini Kibakwe na Mwandoya hata hazifanani, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. (*Kicheko*).

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la ziada la Mheshimiwa Mpina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge watakumbuka nilipokuwa najibu hoja mbalimbali zilizotolewa wakati tukiwasilisha Bajeti yetu, tulisema kwamba nia ya Serikali ni kuona tunafikisha mawasiliano ya simu katika miji na vijiji vyote.

Kwahiyo, mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwandoya, kwamba tutaendelea...

SPIKA: Aah, Mwandoya ni kijiji (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba radhi, samahani sana. Mheshimiwa Mpina, kwamba tutaendelea kuwashamasisha makampuni ya simu waone umuhimu wa kupeleka mawasiliano ya simu katika maeneo hayo.

Lakini nimhakikishie kwamba tukianza suala hili la simu za vijijini kutumia ule mfuko ambao utaanza Disemba, nina hakika *speed* ya kufikisha mawasiliano ya simu katika maeneo hayo itakuwa ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, niwaombe tu wananchi wa kijiji cha Mwandoya na vijiji vingine wawe na stahamala, mawasiliano yatafikishwa.

Watoa huduma wa mawasiliano ya simu nia yao ni kufanya biashara na kwenye biashara ni vijijini ambako wananchi wako na wana uwezo wa kutumia mawasiliano hayo. (*Kicheko*).

Na. 455

Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Kwa kuwa, Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, *PSRC*, ilimaliza muda wake kwa mujibu wa sheria ya mwaka jana; na kwa kuwa, kazi za kurekebisha Mashirika yaliyobaki zimehamishiwa *CHC* lakini Kamati ya Bunge ilishauri Serikali iunde Taasisi ya Kudumu ya Kurekebisha Mashirika hayo:-

- (a) Je, ni Mashirika mangapi ambayo hayajarekebishwa hadi sasa?
- (b) Je, Serikali inasema nini kuhusu kuunda Taasisi ya kudumu ya kurekebisha Mashirika ya Umma?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE.JEREMIA S. SUMARI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Jimbo la Lupa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, wakati Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, *PSRC*, inamaliza muda wake mnamo tarehe 31/12/2007, jumla ya mashirika 37 yalikuwa hayajarekebishwa. Kwa sasa urekebishaji na ubinafsishaji wa Mashirika hayo upo katika hatua mbali mbali na unaendelea.

(b)Mheshimiwa Spika, kazi ya kurekebisha Mashirika ya Umma pamoja na kufuatilia Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa kwa hivi sasa inafanywa na *Consolidated Holding Corporation, CHC*. *CHC* ipo kwa mujibu wa Sheria Na. 23 ya 1997 na marekebisho ya mwaka 2007. Aidha, kwa mujibu wa sheria hiyo, itakapofikia mwaka 2011, *CHC* itakuwa imemaliza muda wake. Lengo la Serikali ni kuwa na chombo cha kudumu ambacho kitasimamia urekebishaji na ufuatilaji wa Mashirika ya Umma yaliyorekebishwa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza. Kwa kuwa, *Consolidated Holding Corporation* iliundwa kusimamia mali na madeni ya Mashirika yaliyorekebishwa, kusimamia mali na madeni lakini *PSRC* iliundwa kurekebisha, sio kusimamia, kurekebisha mashirika ya umma. Kwahiylo, *PSRC* ina uzoefu na taaluma ambayo imejengeka kwa muda mrefu. Je, taaluma hiyo na uzoefu huo upo *CHC*, la kwanza?

Mheshimiwa Spika, la pili. Je, Serikali inaweza ikayataja hayo mashirika 37 ambayo bado hayajarekebishwa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli *CHC* ndiyo iliyochukua majukumu ya iliyokuwa *PSRC* lakini katika kuchukua majukumu hayo vilevile baadhi na wengi wa Wakurugenzi na Watendaji waliokuwa *PSRC* wamehamishiwa *CHC*. Kwa hiyo wamepeleka utaalamu na uwezo wao ambao walikuwa wameujenga kwa muda mrefu wakiwa *PSRC*. Kwa maana hiyo *CHC* ya sasa ina nguvu na uwezo zaidi mana yake inachanganya sasa uwezo wake kama *CHC* wa watendaji wao wa pale awali na pamoja na hawa ambao wamehamishwa kutoka *PSRC* kuja *CHC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mashirika 37 ambayo bado kazi inaendelea ya ama kuyarekebisha au kuyabinafsisha. Kama nilivyosema yako 37, nitataja baadhi. Kwanza *National Microfinache Bank*, ambayo kama tunavyojua Serikali imezindua uuzaaji wa hisa zake tarehe 18, mwezi huu na ninawahamasisha Waheshimiwa Wabunge, wanunue hisa kwenye Benki hii ili wawe na hisa na washiriki katika uendelezaji wa uchumi wa nchi yetu. Uuzaji wa hisa hizi unaishia tarehe 8 mwezi ujao.

Shirika lingine ni *NIC, National Insurance Corporation*, kuna *TPC*, Shirika la Posta, kuna *TTCL*, kuna *TDFL*, kuna Kampuni ya Ndege ya Tanzania, *ATCL* na makampuni mengine ambayo kwa sababu ni mengi ninaomba nimpatie Mheshimiwa Mbunge, orodha kamili kama atahitaji na kama kuna Mbunge mwengine ambaye atahitaji basi tutafanya hivyo ili wapate taarifa kamili.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa makubaliano yaliyofanyika hapa Bungeni, ni kwa Wizara ya Fedha kuunda taasisi ambayo itajumuisha *PSRC* na *CHC* na sio *CHC* kuchukua watu kutoka *PSRC* na kwa kuwa makubaliano hayo yalikubalika na kutoa muda wa miezi minane kuanzisha taasisi hiyo.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hilo haliendani na makubaliano yetu tuliyoyafanywa hapa ndani ya Bunge hili Tukufu? (*Makofi*).

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdalla Omar Kigoda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nakiri kwamba tulikubaliana hivyo lakini tafsiri yetu ilikuwa kwamba tuunde chombo ama kiwepo chombo ambacho kitakuwa na uwezo wa kufanya kazi iliyokusudiwa. Ama kiiwe *CHC* ama kiwe chombo kipyga moja kwa moja. Lakini na wale watendaji waliokuwa *PSRC* waliohamishiwa *CHC* walikuwa na uwezo unaokubalika.

PSRC haikuvunjwa kwa sababu watendaji wake walikuwa wameonekana hawafai, la hasha.

Kwanza muda wa *PSRC* ulikuwa umekwisha. Lakini vilevile kazi ambayo ilikuwa imebakia ambayo wangeendelea nayo vilevile ilikuwa imepungua kwa kiasi ambacho Bunge na Waheshimiwa Wabunge waliona ni busara sasa muda wa *PSRC* ukafikia ukomo na kuhamishiwa majukumu yake kwenye chombo kipyga cha *CHC*.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wabunge kwamba ikiwa itabainika ni vyema sasa kuanzisha na kuunda chombo kipyga badala ya *CHC* basi jambo hilo litafanyika.

Na. 456

Kupanda kwa Thamani ya Shilingi na Mfumuko wa Bei

MHE. ZUBEIR ALI MAULID aliuliza:-

Kwa kuwa, siku za hivi karibuni tumeshuhudia kuimarika kwa Shilingi ya Tanzania baada ya kupanda kwa thamani yake ikilinganishwa na Dola ya Marekani (US\$):-

(a)Je, kwa nini ukweli huo haukusaidia bei za bidhaa mbalimbali nchini kuteremka na badala yake bidhaa nyingi muhimu kama Sukari, Saruji na nyinginezo zimezidi kupamba bei na kuwa udhia kwa walaji?

(b)Je, ni lini Serikali itaananza chombo ambacho kitadhibiti upandishaji holela wa bei za bidhaa mbalimbali pamoja na huduma na kama chombo hicho kipo, kwa nini kinashindwa kutekeleza majukumu yake kwa kudhibiti bei holela?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Kwamtipura, lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na Dola ya Marekani imeendelea kuimarika siku za hivi karibuni. Kuongezeka kwa thamani ya shilingi huwezesha mfumuko wa bei kupungua kutokanana kupungua kwa bei ya malighafi na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Hata hivyo, unafuu huu unaweza usionekane mara moja katika kupungua kwa mfumuko wa bei kwa sababu yapo mambo mengine yanayochangia katika kuongezeka au kupungua kwa mfumuko wa bei na gharama za bidhaa nchini.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia lilipelekea bei za mafuta katika soko la ndani ya nchi kupanda na kuchangia moja kwa moja kuongezeka kwa mfumuko wa bei. Kuongezeka kwa bei za mafuta kumesababisha pia kuongezeka kwa gharama za uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi na huduma, ambazo hutumia mafuta katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa bei ya sukari kulitokana na kupanda kwa gharama za uzalishaji, ikichangiwa na gharama za usafirishaji na mabadiliko ya hali ya hewa hapa nchini. Kiasi kikubwa cha sukari kinachotumika nchini huzalishwa na viwanda vyetu.

Vile vile, kupanda kwa bei ya Saruji kunatokanana ongezeko la mahitajiya Saruji hapa nchini katika sekta ya ujenzi, kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa hiyo nje na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa bei za bidhaa na huduma zinapangwa kutokana na nguvu ya soko. Aidha, kwa kuwa Serikali inatambua athari za kupanda kwa gharama za maisha zinazosababishwa na mfumuko wa bei, Serikali inaratibu kwa karibu mwenendo wa mfumuko wa bei, ili kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa na gharama za huduma mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za kudhibiti ongezeko la holela za bei za huduma na bidhaa. Hatua zinazotumika ni pamoja na zifuatavyo:-

o Serikali imanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na maji (*EWURA*) ili kudhibiti ongezeko la holela la bei ya mafuta pamoja na kusimamia mwenendo, upatikanaji, usambazaji na uuzaji wa mafuta nchini.

o Serikali imenzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Safari za Nchi Kavu na Majini – *SUMATRA*, ambayo inafuatalia na kusimamia kwa karibu nauli za usafiri na usafirishaji.

o Serikali pia imekuwa ikichukua hatua za dharura kudhibiti bei ya bidhaa muhimu kama Sementi kwa kudhibiti uuzaji wake nje ya nchi na vilevile kupunguza kodi ya forodha ili kushawishi wafanyabiashara kuagiza bidhaa hiyo toka nje ya nchi ili kuboresha upatikanaji wake.

o Serikali imanzisha Tume ya Ushindani wa Biashara (*FCC*), kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii ya Kitanzania inafanya biashara katika msingi wa ushindani

ulio sawa. Mfanyabishara hafanyiwi bugudha na mlaji analindwa na kutouziwa bidhaa zisizo na ubora na au bei ya juu.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu marefu na mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo sana la nyongeza la kumwuliza.

Kwa kuwa, kimsingi Mheshimiwa Waziri anakubaliana nami kwamba bei za mafuta duniani zina athari kubwa sana katika mfumuko wa bei na kwa kuwa hapa Tanzania tunaweza tukaliondoa hilo Tanzania kwa sababu tunayo Nishati na Gesi pamoja na mafuta yapo lakini Serikali inaoneka na imefanya *investments* ambayo haitoshi sana katika sehemu hii.

Je, Mheshimiwa Waziri au Serikali iko tayari kutekeleza yale maneno aliyojasema jana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwamba ukitaka kula nawe uliwe kwa ku-*invest* zaidi kwenye sekta ya mafuta ili tuweze kuondokana na haya matatizo ambayo tunayo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuber Ali Maulid, kama ifuatavyo:-

Ni kweli tulimsikia Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete akisema kwamba lazima uliwe ili ule, sasa kama Mheshimiwa Rais keshasema hivyo basi mimi ninachoweza kufanya ni kurudia tu kwamba Serikali itakubali kuliwa ili na wananchi wapate kula.

SPIKA: Lakini fursa hiyo tunamwachia Rais tu ninyi msiwe mnarudiarudia tu hapa hayo mambo! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umeshapita .
SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo. Tukianza na wageni mtaniwia radhi leo ni wengi kidogo nadhani wamechanganyika na wa jana na wale wa siku ya leo.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Bernard Membe anao wageni kutoka katika Jimbo lake la uchaguzi la Mtama nao ni Wenyeviti wa Kata zote 15 za Jimbo la Mtama wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Lindi Ndugu Gwaja, naomba wasimame tafadhali. Karibuni sana, na ninatumaini mtaendelea kumlea vizuri Mheshimiwa Membe kwa sababu baadhi yetu tunampenda sana. (*Makofi*)

Leo Zanzibar kuna wageni wengi sana. Wageni wa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano). Ni kutoka katika Jimbo lake la Uzini, Ndugu Mzee Rajab Khatibu wa Jimbo la Uzini CCM, karibu sana.

Ndugu Ally Juma, Katibu wa Mpapa - nadhani ni tawi hili la Mpapa. Ndugu Amour Mohamed Katibu wa Mchangani, hii ni kama Mtwara unajua majina ndiyo maana kweli nchi hii ni moja maana yake lah! Mchangani iko Mtwara, Zanzibar na Mafia pia. Ndugu Haji Vuai, ni Katibu Vijana Pagali, Ndugu Shaaban Idd Katibu wa Fedha wa Jimbo na Ndugu Hassan Mussa, Mwenyekiti wa Kiboje Mkwajuni. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine kutoka Zanzibar ni wageni wa Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, ambao ni Ndugu Haji Wadi Haji Mwenyekiti wa Jimbo, karibu sana Mwenyekiti. Ndugu Hamdu Vuai Suleima Katibu wa Jimbo, Ndugu Mohamed Sule Katibu Mwenezi, Ndugu Pandu Haji Yakoub Katibu Fedha na Uchumi, Ndugu Ally Nahodha Ally, ambaye ni Katibu Mwenezi wa Wilaya, Ndugu Shafi Hamadi Ally Katibu Msaidizi wa Wilaya na Ndugu Idris Amir Haji Afisa Wilaya. Karibu sana. (*Makofi*)

Pamoja nao wapo Waheshimiwa Madiwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Riziki Suleiman Sule, Mheshimiwa Mariam Suleiman Haji, Mheshimiwa Subira Ally Pira, Mheshimiwa Abdullaziz Hamadi Ibrahim, Mheshimiwa Ramadhani Aga Amour, Mheshimiwa Haji Khamis Chum, Mheshimiwa Ameir Simai Ope. Karibuni sana.

Tunaendelea tu na Zanzibar, wageni wa Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Makatibu wa Matawi ya CCM yaliyopo ndani ya Jimbo la Kitope.

Nao ni Ndugu Khamis Khamis, Ndugu Hilda Duncan Sikombe, Ndugu Juwate Bourice na Ndugu Asha Abdallah karibuni sana. (*Makofi*)

Karibuni sana wageni wetu na Ndugu zetu kutoka Zanzibar tunafurahi mara kwa mara mnapokuja mnazidi kuimarisha umoja wa nchi yetu.

Wageni wa Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri wa Nchi TAMISEMI ni Ndugu Waziri Abdallah Said, Ndugu Kashindye Kombwe, Ndugu Zilabela Kombwe, Ndugu Yahya Msema kweli na Ndugu Rajabu Khamis. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Takribani wote ni wanafunzi. Kwa hiyo, nawatakia kheri katika mafunzo na masomo yenu.

Mgeni wa Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, ambaye ni Bwana Revid Ghalil kutoka Garilea Israel, *Our guest froma Israel. Please stand up.* Naona hakukuwa na mawasiliano mazuri pengine. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa ni Waheshimiwa Madiwani 20 na watumishi saba (7) kutoka Halmashauri ya Wilaya Nkasi. Wamefuatana na Viongozi wao ambaye ni Ndugu David Ngalula na Sumuni Mwanakulya. Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, karibuni sana. (*Makofi*)

Niseme tu hapa kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Rukwa wana utaratibu mzuri sana wanawaalika kwa pamoja Madiwani kwa zamu Halmashauri kwa Halmashauri na ninadhani leo wanakamilisha Mkoa wao wa Rukwa. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje ni Mkewe Mheshimiwa Mbunge, ambaye anaitwa Eveline Madeje akiambatana na kikundi cha akina Mama 15 kinaitwa *Neema Group* kinachoongozwa na Mama Mchungaji Mary Kanyamala na Mama Chomola. Haikusemekana kikundi hiki ni cha kufanya shughuli gani lakini ni *Neema Group* ni kwaya. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa George M. Lubeleje ni Wana kwaya 50 kutoka katika Kanisa la *AIC Chang'ombe* la Dar es Salaam wakifuatana na Mchungaji wao Elikana Gonda wa Kanisa la *AIC Dodoma*. Wamekosa nafasi, basi wanansikia huko waliko.

Wageni wa Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan amba ni Viongozi 35 wa Chama cha Mapinduzi yaani Wenyeviti, Makatibu wa Kata, Wachumi, Makatibu wa Wenezi kutoka katika Kata 10 za Jimbo la Kinondoni wameambatana na Viongozi wa msafara amba ni Bwana Thadeo Kiwenge, Mjumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Kinondoni. Ndugu Charles Mgonja Kata ya Ndugumbi na Ndugu Rehema Kazenga Katibu wa Jimbo. Karibuni sana.

Kumbe wale walikuwa ni wale Viongozi 35 kutoka Kinondoni, ahsante sana. Mnafahamu na Spika pia makazi yake ya Dar es Salaam yapo Kinondoni.

Wageni wa Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ni mtoto wa Dada yake ambaye ni Bwana Philip Nguma, anatoka *Kizota Pharmacy* pamoja na watoto wake ambaao ni Ivan, Ian na Ivo. Karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga ni Rajab Kipendi ambaye ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Ntuntu, Mheshimiwa Ramadhani Mkaku, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Sepuka, Ndugu Hussein Mayombwe, Mwenyekiti wa CCm Kata ya Dungunyi, Ndugu Mussa Julius, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Mgungira na Ndugu Obeid Madai, Katibu Mwenezi Kata ya Ihanja. Ahsanteni sana na Karibuni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, ambaye ni mdogo wake anayeitwa Sussan Kapelega, ahsante na karibu sana. unafananafanana na dada yako. (*Makofii*)

Wanafunzi 70 na Walimu 3 kutoka shule ya Sekondari ya Kikunde Tanga, nadhani hawa ni wengi pengine wapo kule kwenye *basement*. Wanafunzi 30 kutoka Kikuyu shule ya Msingi Dodoma, ahsanteni sana vijana pamoja na Walimu tunawatakatia mafanikio katika masomo, karibuni sana.

Pia wanafunzi 15 kutoka Shule ya Msingi Mlimwa B kundi lingine hilo pamoja na Walimu wao, karibu sana na ahsante sana, nawatakatia kheri katika masomo na Walimu katika ufundishaji.

Wageni wa Mheshimiwa Juma H. Killimbah ni Mheshimiwa Fadhil Mkenka Mwenyekiti wa CCM Kata ya Urugitu. Mheshimiwa Joel Zefania Mkoma Diwani wa Kata hiyo hiyo. Ndugu Richard Mtambi Mwenyekiti wa CCM Tawi la Mang'ole na Ndugu Samuel Maige Mwananchi kutoka Mang'ole, nadhani ni shabiki wa Mheshimiwa Mbunge. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge lao kwenye *Speakers Gallery* tunaye mgeni kutoka nje ya nchi yetu lakini ni binti ambaye ni raia tu wa Tanzania, anafanya kazi kule Uingereza. Yeye ni Bibi Susan Mzee naomba asimame. Yeye kwa wadhifa ni Katibu wa Chama cha Mapinduzi wa Tawi la *United Kingdom* likijumlisha *England* na *Northern Ireland* na sasa hivi kwa taarifa tu ni kwamba kuna mashina ya wanachama Uingereza 470 na wanachama wa CCM wamekwishakiuka idadi ya 600 imebidi wasitishe kwanza kwa sababu miundombinu haitoshelezi kuwashudumia. Kwa hiyo, wanaendelea na utaratibu mpya ili kuweza kuongeza wanachama zaidi. Lakini tawi hili ni la kipekee kwa kweli ni la kipelee na mimi nimewatemelea kule Uingereza. Hawabaguani kabisa wakiwa kule wana nafasi yao pale katika mji unaoitwa Reding karibu na London ambako kila wiki Watanzania wa vyama vyote vya siasa wanakutana chini ya ufadhilli wa tawi hili la CCM la London. Nadhani na hapa kwetu tungefuata mfano huo na wanashikiana katika mambo mengi sana ya furaha na huzuni na wanafarrijiana na ni juhudzi za binti

huyu Sussan Mzee ndiyo zimewezesha kushamiri kwa tawi lisilo na ubaguzi. Nakupongeza sana. (*Makofii*)

Lakini pia nitambue kazi kubwa sana ambayo Balozi wetu kule Uingereza Mheshimiwa Mwanaidi Maja anayofanya, ye ye amekuwa karibu sana na tawi hili. Kwa sisi wengi ambao tunasafiri na amejitahidi sana kuweza kuitangaza nchi yetu vizuri sana nadhani sehemu ya kuongezeka kwa watalii kuja nchini ni kutokana na juhudzi zinazofanywa pale Ubalozi wa London.

Mwisho nimtamke tu mlezi wa tawi hilo ambaye ni Bwana Shahibu Maja, Mume wa Mheshimiwa Balozi ye ye ndiye Mlezi wa Tawi lile la Chama cha Mapinduzi kule UK. Nawapongeza kwa kazi nzuri. Sasa matangazo ya vikao. Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda anahitaji Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakutane leo saa tano asubuhi katika ukumbi namba 231.

Ndugu Mbaga kwa niaba ya Katibu wa Bunge, anaomba kusema kwamba leo saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa kutakuwa na Semina fupi inayohusu shughuli za Bandari upande wa *TICS*. Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa katika semina hiyo kuweza kupata taarifa za Maendeleo ya kampuni hiyo ya *TICS* katika kuimarisha Bandari yetu. Wanafunzi 70 kutoka Kikunde Kilindi nilidhani nimewataja hawa lakini nimekumbushwa basi nadhani watakuja baadaye wako *basement* kwa sasa. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mbunge wa Kilindi. Baadaye itakapopatikana nafasi nadhani wataingia hapa ndani. Waheshimiwa Wabunge, baada ya hilo tangazo la semina napenda tu nifahamishe tu ifuatavyo mambo machache.

Kwanza, mukutano au kikao cha Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge ni Saa 8.30 na kitaongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika kwa sababu nina udhuru wa kufutilia mambo fulani yenye maslahi muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Kwanza kuhusu wageni kutokuwepo naomba hivi, aliyealika au Mheshimiwa anayealika wageni tunapoamka akaona kwamba pengine hawapo basi atufahamishe mezani tusiwe tunatambulisha hewa, unasema wageni halafu hawapo haipendezi.

Waheshimiwa Wabunge wale ambao mna wageni wengi wale wanaokuja kama kundi kama wanafunzi au Waheshimiwa Madiwani idadi ni kubwa usipokuwa umearifu takriban siku mbili au tatu kabla tunapata shida kwa sababu ikiwa ni wa kushtukiza siyo rahisi kupata nafasi kwenye *gallery* nafasi za wageni 30 kwa taarifa ya siku moja tu siyo kitu rahisi.

Kwa hiyo, kwa kuwa mara nyingi wanakuwa wanatoka mbali ni rahisi kujua tarehe watakayofika hapa basi tukifahamu tunawapa nafasi na inapunguza bughudha kwa wageni. Lakini pia inaondoa ile hali kwamba umealika wageni halafu siku husika wanajikuta wamebekwa kwenye *basement*.

Lingine, kutohana na ombi maalum la Waheshimiwa Wabunge la Hotuba ya Mheshimiwa Rais Kikwete ya jana, itachapishwa nakala na tutagawiwa. Lakini zaidi ya hivyo kuna ombi kwamba tuweze kujadili tutashirikiana na Mheshimiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, tuone katika zile siku zetu tatu zile yaani tarehe 27, 28 na 29/8/2008 tuchague angalau pengine hata nusu siku tuweze kuitafakari hotuba ile muhimu sana kwa sababu ukisogezza mbele zaidi basi ile mantiki yake na maonjo yake yanakuwa yamepungua. Kwa hiyo, itakuwa vizuri tuifuatilie kwa kujadili.

Nitangaze tu kwamba katika muda ule wa siku tatu zile za shughuli binafsi za Wabunge baada ya kuhitimisha shughuli za Serikali au zitakuwa zimebaki siku mbili nadhani 28 na 29 haitawezekana kujadili taarifa ya Kamati ya Madini, ili tuitendee haki Taarifa ya Kamati ya Madini yenyepeke yake inahitaji siyo chini ya siku mbili.

Kwa hiyo, tumeona badala ya kuilazimishalazimisha tu halafu wakachangia wachache basi ni vema tuweze kuileta katika Mkutano wa kumi na tatu.

Basi baada ya matangazo hayo sasa tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Tunao wachangiaji sita, tutajitahidi katika muda huu uliopo. Mkumbuke kwamba tunahitimisha hoja hii leo asubuhi kwa kipindi hiki mpaka mchana saa saba.

Kwa hiyo, Wabunge walioomba kuchangia ni Mheshimiwa Kilontsi Muhamma Mpologomyi, Mheshimiwa Ramadhan Athuman Maneno, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto ambaye hayupo. Kwa hiyo, ni watano tu.

Tunaanza na Mheshimiwa Kilontsi Muhamma Mpologomyi.

MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie machache kwenye hoja hii ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha salama usiku wa leo nikiwa mchangiaji wa kwanza kuhusu hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, nimpongeze pia Naibu wake, Katibu Mkuu na Maofisa Wakuu wote

wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kujenga heshima ya Tanzania kila mahali duniani.

Kwa hiyo, ninawapongeza sana na ninaunga hoja mkono. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi ambayo yameelezwa ndani ya hotuba yake ambayo yamezingatia maslahi ya taifa letu lakini heshima ya nchi yetu pia inategemea kwa kiwango kikubwa sana ufanisi unaopatikana kwenye Balozi zetu za nchi za nje na mimi naomba niipongeze Wizara hii kwa kazi kubwa ya ukarabati wa Ofisi za balozi zetu ambayo wamekuwa wanafanya nchi za nje, nawapongeza sana Wizara hii.

Pale Brucels tulikuwa hatuna Ofisi kwenye ubalozi tunakodi ubalozi una matatizo mara kwa mara mara lakini nafurahi kwamba sasa tumepata ubalozi mzuri tu, maofisa wanakaa vizuri tu hata wageni ukienda unapata mahali pa kukaa na kufanya shughuli zako. Ile nyumba ya Balozi ambayo kwa miaka mingi ilikuwa haikaliki ukienda kukaa kule inavuja sasa ni nyumba nzuri sana.

Naomba zile shughuli ndogondogo ambazo zimebakia kwenye nyumba ya Balozi ile watengewe fedha na kazi ile iweze kumalizika haraka iwezekanavyo. (*Makofî*)

Mwaka jana tulipoongozwa na Mheshimiwa Spika kule Geneva kwenye Mkutano wa *IPU* ye ye Mheshimiwa Spika alipondoka kwenye London tulipata fursa ya kukaribishwa na Balozi wetu nyumbani kwake.

Ana nyumba moja nzuri sana na nafikiri nyumba ile sijawahi kuiona kwenye Ubalozi wowote, ni nyumba nzuri sana. Lakini ile nyumba ina chini na juu lakini ni vipande vipande maana ni mbovu, ukienda kwenye *basement* kote ni hovyo, hakuwezi kukalika, hakuwezi kuwekeka kitu lakini ni *one of the best houses* ambazo tunazo kwenye Balozi zetu. Kila mmoja anayeiangalia nyumba na hata sisi Wabunge tuliokwenda pale kwa kweli tulisikitishwa sana na hali ya nyumba ile.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atenge fedha, nyumba ile itengenezwe itatujengea heshima kubwa, ile ni nyumba yetu. Lakini pia tumekuwa pale Geneva kwa muda wa miaka mingi leo hii nilipotembelea Ubalozi ule wa miaka ya tisini tulikuwa angalau na ofisi nzuri kuliko tulizo nazo. Baadaye ofisi zile zimeendelea kupungua na sasa tunajikuta ni kama hatuna ofisi pale Geneva. Naomba Mheshimiwa Waziri tununue ofisi ya Ubalozi wetu pale Geneva tujenge heshima ambayo tunaihitaji.

Mheshimiwa Spika, pale India tuliponuna ile nyumba yetu na tukanunua nyumba ya Balozi heshima iliongezeka kwa kiwango kikubwa na Geneva na mahali pakubwa hatuwezi kukaa bila ofisi za Ubalozi zeny heshima na hadhi ya Tanzania, Tanzania ni nchi kubwa, tuache kujidharau sisi wenyewe, ni nchi yenye heshima inaheshimika. Tukisimama tunazungumza vitu tuna heshima kubwa katika Afrika.

Lakini ukienda unakuta tuna ofisi ambayo hata watu wamebanana hata mtu haelewi tunapita wapi, ofisi moja wamekaa watu wanne, haitujengei heshima hata kidogo.

Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe Ubalozi wetu wa Switzerland unakuwa na hadhi inayostahili, zile ofisi zitengenezwe na ile nyumba ya Mheshimiwa Balozi iweze kujengwa vizuri na iweze kutengenezwa. Ni nyumba moja nzuri sana sidhani kama tuna nyumba kama ile mahali popote tulipo na Ubalozi katika dunia hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kuzungumza linahusu wakimbizi. Miaka ya nyumba nilikuwa nazungumza sana habari za wakimbizi. Wakimbizi wamekuja katika Mkoa wa Kigoma, *entry point* ya wakimbizi wengi walioingia ni katika Jimbo langu, Tarafa ya Manyovu, Muyama, Herujuu wanaingia Kasulu wanakwenda Makambini lakini kazi kubwa ya kuwapokea na kuwaingiza kwenye vijiji na kutumia mashule, misitu, shule zetu, mali zetu, rasilimali zingine na chakula cha wananchi ilifanyika katika hivi vijiji vilivywapokea wakimbizi na wakati huo Wilaya haikufanya kazi, viongozi wote walifanya kazi ya wakimbizi. *Both Regional and District Administration* hazikufanya kazi zilihudumia wakimbizi hawa wakitumia muda ambao wanagetumia kwa ajili ya maendeleo ya wakazi wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kuzungumza humu ndani nikasema ni jambo moja kuelewa kazi kubwa ambayo watu wa Mkao wa Kigoma wamefanya kwa ajili ya ujio wa wakimbizi katika Taifa hili. Lakini jambo lingine la kufikiria ni mzigo gani ambao watu wa Mkao wa Kigoma wameubeba kwa ajili ya wakimbizi na kwamba kwa hili wanahitaji kuwa *compensated* na kwa hili wanahitaji watambuliwe na nashangaa sijawahi kusikia hata siku moja hotuba ikitolewa au mtu akisifu juhudu kubwa ambazo watu wa Mkao wa Kigoma wamefanya kwa kuhimili mapigo ya athari za wakimbizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni kwamba Serikali ikae, izungumzie ni namna gani wanaweza kuwa-*compensate* wananchi wa mkoa ule. Pili, viko vijiji ambavyo wakati wa vurugu hizo za wakimbizi ambazo zimepoteza maisha ya watu, mifugo. Nilipokuja hapa nikaomba lazima tudai fidia katika Serikali ya Burundi nikaambiwa kwamba ile si Serikali ambayo inaweza kuelewa mambo yanavyokwenda na kwamba tuwaache watakapokuwa Serikali kamili tutawadai. Tatizo humu ndani tunazungumza vitu hakuna ufuatiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kungekuwa na ufuatiliaji kuna watu wanaotoka Kijiji cha Nyakimwe walikuwa wanalima, wakauawa na askari wa Burundi, *the whole family* ikauawa, watoto wakabaki ni yatima. Nilipoomba msaada wa Serikali hakuna majibu, wale watoto mpaka leo wanahangaika.

Mheshimiwa Spika, kuna mifugo iliibiwa katika Kijiji cha Kibane, Kitambuka na Muyama nikasema tudai mifugo hii maana imechukuliwa na mingine tumeikuta Burundi, hakuna kinachofanyika, tutadai Serikali itakapokuwa imetulia. Sasa Serikali ya Burundi imetulia, nina imani tunaweza kurudi nyuma kuidai fidia Serikali ya Burundi.

Kutunza Warundi ndani ya Tanzania *it is an International humanitarian obligation that is real international humanitarian obligation* lakini kwamba sasa hata athari kama hizi za vifo ukiondoa ujambazi mwingine mwingine ambao umekuwa ukifanyika ni vizuri tukadai fidia kwa watu wetu waliopoteza maisha.

Kigoma imekuwa ika-host wakimbizi kwa miaka mingi na Kagera nayo imekuwa ikifanya hivyo hivyo. Hii mikoa inahitaji kufikiriwa. Nafikiri hili limeeleweka na litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka nilizungumze ni kuhusu utekelezaji wa mkataba wa *Economic Partnership Agreements*. Mkataba huu bahati mbaya sikuwepo wakati wa kujadili hotuba ya Wizara ya Biashara lakini ni kwamba huu mkataba ulikuwa *initialled* mwaka jana mwezi Desemba, mwisho wake ilikuwa ni tarehe 3.

Zile agreements zote kwa kizungu wanasesma they were scaled back to become WTO compatible interim deals made mainly on trade goods and signed enhanced. Zikasainiwa kwa haraka kwa sababu WTO wanataka hii mikataba yote isainiwe haraka haraka ikasainiwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka Desemba, 2007 *fewer than one third* ya ACP countries zote zikawa zimesaini ile *interim EPA* ambayo inaitwa *framework EPA* ili kutimiza lengo la *deadline*, leo tunapozungumza zaidi ya nchi arobaini hazijasaini, *Financial Times* la Uingereza liliandika hivi nitasoma kwa Kiingereza kwa ruhusa yako:-

"The Financial Times described the result leading to EPA initialling as a TANGOLD cuts fraud if not a mangled docks breakfast and this was explained as a fair description of the undertaking. Cajoled kubwa katika utaratibu huu mzima ilikuwa ni regional economic integration, tumekuwa tuna-negotiate lakini tuna-negotiate trade but it is not all that itakayofanya mkataba huu kuwa wa maana katika Maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ya *development dimension, regional integration*, wametugawanya wakasema sisi Kusini hatuwezi kwenda lazima turudi *East Africa*, *Fernap* ndipo tulisaini mkataba wa *customs* kwamba ukisaini mmoja huwezi kwenda huko lakini soko lako bado ni dogo na unataka kubwa. Najua Serikali ina mtazamo mpana kwamba sasa tunataka twende *Eastern, Southern and Central Africa* kama tunaweza kuwa *block* moja, lakini ninyi mpaka mje ku-negotiate hilo mfikie huko mnakokwenda, *SADC* mtakuwa mmeshatoka na nalizungumza hili kwa sababu nimemwona Waziri anazungumzia habari ya *SADC* kwamba itakuwa soko huru, *it will not include* Tanzania, Tanzania haitakuwemo katika lile soko huru la Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo yanafanyika katika hiso *negotiations* na mojaya mambo hayo ni pamoja na viwanda vyetu vya sukari ambavyo vinauza katika EU chini ya Mkataba wa *International Sugar Protocol*. Huu mkataba nina wasiwasi hivi katika Serikali yetu nani ana-negotiate mkataba huu. Nimekutana na wafanyabiashara wale *private* ambao ndio wame-invest hapa, *there the ones who negotiating this particular agreement*. Nimekutana nao *a couple of time*, wame-employ a consultant kule London, *it has been negotiating an International sugar protocol*. Lakini ni kwamba makubaliano haya ni lazima iyafaidi nchi inayozalisha zao hilo ndivyo inavyokwenda. Nilifikiri hilo nalo nilitaje ili tuweze kwenda nalo na tuweze kufika mahali tulifanyie kazi, tufaidike maana zinaweza kutolewa *benefit* zikaenda kwa mwekezaji tu, nchi tukawa hatufahamu, inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu hiki kitu ambacho nakiita *the international Economic meltdown*. Leo hii dunia nzima ipo *in a crisis* ya kila aina ndiyo maana tunazungumza *inflation* yetu iko juu na kila kitu kipo juu hapa. Sasa uchumi unakwenda vibaya na hapo ndipo tuna kazi kubwa kama Taifa. Kazi ni ngumu, Mataifa makubwa yakinaka hali hii itaacha leo hii wako *busy wana-diversify into biofuels* ambayo wanajua nchi maskini hazina uwezo nayo, hatuna viwanda vya *biofuels*, bei.....

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzajij*)

SPIKA: Mheshimiwa Mporogomyi kumbe ni kengele ya pili, pole sana. Ahsante sana.

MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Spika, kwanza nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, yenye matumaini na inaonyesha dira ya Maendeleo katika Serikali hii ya Awamu ya Nne. Pia nimpongeze Naibu Waziri pamoja na Naibu Katibu Mkuu kwa maandalizi mazuri walivyofanya na kuweza kutuletea hotuba hii iliyosomwa jana pamoja na maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje kwa kweli inatupa matumaini makubwa sana ya kuelekea kwenye Maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hiso naomba nianze kuchangia kwenye suala linalogusa Chuo chetu cha Diplomasia cha pale Kurasini. Ninavyofahamu hapo awali hiki chuo kilikuwa na ushirikiano mkubwa sana na nchi ya Msumbiji na mpaka sasa sina hakika kama Mheshimiwa Waziri atanifahamisha au kulifahamisha Bunge lako Tukufu kama ushirikiano huo upo na nchi ya Msumbiji na kama bado yapo ni kwa asilimia ngapi na wao mpaka dakika hii mchango wao ni nini katika chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuchangia ni hili linalohusu utoaji wa *visa* kwenye balozi za Marekani na Uingereza. Yapo manung'uniko sana kwa wananchi wa Tanzania wanaopata usumbufu mkubwa sana kwenye Balozi hizo wanapokwenda kuomba *visa*. Wote tunafahamu suala la *visa* linahitaji umakini mkubwa kwenye kuzitoa lakini sielewi Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje inapokea vipi kilio hiki cha wananchi kupata usumbufu mkubwa wanapokwenda kuomba *visa* katika nchi hizo. Nalisema hilo kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, nalisema kwa sababu nchi yetu ya Tanzania hatusifikasi sana kwa kuwa wagumu wa utoaji *visa* lakini zipo Balozi ambazo ni marafiki zetu tumewakaribisha hapa nchini, wanafanya kazi lakini suala la *visa* kumpa Mtanzania ni tatizo kubwa sana ambalo linachukua muda mrefu hatimaye watu kutokuwa na imani na hizi nchi ambazo wakati mwingine tunazisema ni rafiki.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza hapa Tanzania. Yapo malalamiko pia, wanapotaka kuja kuwekeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa ili wapate nafasi ya kuja kuwekeza vipo vikwazo vidogo vidogo wanavyovipata kupitia kwa watendaji wetu waliopo kwenye ofisi zetu za Balozi huko nje.

Naomba suala hili wakati anaweka hitimisho ya hotuba yake basi atueleze kwa nini kunatokea manung'uniko kama hayo ambayo hayailetei sifa nzuri nchi yetu wakati kwa sasa ina dira na mwelekeo mzuri wa kuweza kukubalika ndani ya ulimwengu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nilitaka kufahamu maafisa wetu walioko kwenye balozi zetu huko nje jinsi gani wanavyoitangaza Tanzania, wanavyoweka ushirikiano na watu wanaohitaji kuja kuwekeza Tanzania.

Nalisema hili kwa sababu Mheshimiwa Rais jana amezungumza suala la utalii jinsi lilivyochukua nafasi kubwa kwa hivi sasa. Lakini ni Balozi ngapi sasa hivi zimeamua kuitangaza Tanzania hatimaye kuingizia pato nchi yetu. Tumefikia hatua sasa ziweke hata *information centre* ya kuweza kuitangaza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, unaweza kwenda kwenye balozi zetu pale ukataka uone jinsi gani wanavyoitangaza Tanzania yaani wanayo tu kwa kuwa ni Tanzania na wao wapo Ubalozi wa Tanzania lakini kuutangaza utamaduni wa Mtanzania kwenye sekta ya utalii na vivutio mbalimbali bado hatua hiyo haijawa makini vya kutosha.

Naomba Serikali ilitazame sana suala hili kwa sababu leo kuja kuambiwa Tanzania kwa mwaka tuna watalii laki nane na wakati huo huo sasa ndiyo Marekani wanaanza kufika baada ya harakati tulizofanya za kuwekeza fedha juzi juzi wakati nchi yetu ina miaka arobaini na nne ya uhuru.

Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo utaona jinsi gani Balozi zetu zilivyokuwa hazijishughulishi kikamilifu jinsi ya kuitangaza Tanzania. Sasa kama mlima siku zote ulikuwa unatangazwa huko Kenya, Ofisi za Balozi zipo, hayo wanayasikia, wanayaona kwenye vyombo vyaya habari lakini bado walikuwa hawajajituma kuitangaza Tanzania.

Tunaomba Mheshimiwa Waziri alitilie maanani sana ili nchi yetu iweze kupata mapato ya kutosha kwenye sekta mbalimbali za kuingizia tija nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu safari za Rais anavyokwenda nje pamoja na Waziri wetu Mheshimiwa Membe. Nataka niseme kwamba zile safari zimeleta mafanikio na matunda makubwa sana kwa mujibu wa *speech* ya jana ya Rais. Wengi walikuwa wanakebehi sana hizo safari, lakini jana kwa *speech* ya Mheshimiwa Rais imevunja mzizi wa fitina uliokuwa unasema anapokwenda huko anakwenda kufanya kazi isiyokuwa na manufaa. Mengi tumeyaona jana ameleeza jinsi gani barabara zitakavyopata ufumbuzi, umeme utakavyopatikana na mambo mengine tu ambayo ameleeza vizuri sana na kila mtu mwenye kupenda Maendeleo ya nchi hii anastahili aipongeze hotuba ya Rais aliyoitoa jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine yameahidiwa fedha, nchi nyingine zimeshampatia fedha kwa ajili ya Maendeleo au miradi hiyo ambayo inataka kuwekezwa katika nchi yetu. Sasa bila safari hizo ambazo wenzetu wanazikebehi hayo yaliyoelezwa jana yangeweza kupatikana wapi. Kwa kweli mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais wetu anafanya kazi kubwa sana nami namwomba Mheshimiwa Waziri Membe anipelekee salaam zangu kwa Mheshimiwa Rais wakipata hizi safari waende tu kututafutia fedha, wala wasiogope. Waliyoyafanya ni makubwa, tunawaunga mkono kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, nataka Mheshimiwa Waziri anifahamishe, matatizo yalitokea pale Afrika Kusini. Waafrika Kusini walikuwa wanawaondoa wageni, Waafrika Kusini walifanya machafuko makubwa dhidi ya wageni na wageni hao wakiwemo Watanzania wanaoishi Afrika Kusini.

Matatizo yale yalikuwa ni makubwa sana, sasa nataka Mheshimiwa Waziri anifahamishe Tanzania tulikabiliana nalo vipi suala lile ukiacha kutazama tu kwenye televisheni na kwenye vyombo vya habari vingine.

Mheshimiwa Spika, tunataka kujua kama Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ililishughulikia vipi suala lile na ni Watanzania wangapi ambao walipoteza maisha na Watanzania wangapi walipoteza mali zao lakini usalama wao kwa wale ambao waliwarudisha na wale ambao walibaki Afrika Kusini basi naomba Mheshimiwa Waziri atufahamishe kwani leo limetokea Afrika Kusini, kesho linaweza kutokea kwenye nchi nyingine. Kwa hiyo, Wizara itambue kwamba Mtanzania aliyekwenda mahali kwa uhalali anastahili kupata haki zote kuitia Ofisi zetu za Balozi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumza ni suala la *VIP Lounge* hasa pale Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam. Imefikia mahali imekuwa ni kero kubwa, hata ukifika wakati wa safari huelewi nini maana ya *VIP*. Inafikia mahali *VIP* ya pale Dar es Salaam hata watu ambao unawaona kwenye harambee za kuchangia michango ya elimu nao mnakutana pale wana hadhi za *VIP*.

Mheshimiwa Spika, sasa tunashindwa kuelewa na tunaomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie wenye stahili ya kuingia pale ni akina nani. Inafikia mahali mnasimama kama vile mnangoja basi kwenye stendi ya daladala. Tunaomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuweka mazingira mazuri, stahili ya watu ambao wanatakiwa waingie kwenye kile chumba cha wageni maalum.

Mheshimiwa Spika, nalizungumza hilo kwa sababu gani, zipo nchi hata Wabunge wanapokwenda hawapati stahili hiyo, mwezi wa jana nilikwenda *South Africa* wanasema mtu ambaye anastahili kuingia kwenye chumba kile kwa ngazi ya Wabunge ni Spika lakini Mbunge mwagine huna hadhi hiyo lakini hapa Dar es Salaam au Tanzania kwenye *VIP* zetu hali hiyo haipo, kila yule ambaye unakutana naye tu hata mtaani unaye pale ndani. Sasa tuambiwe kama zipo nchi hatustahili watuambie nchi fulani mnastahili hivi, nchi fulani hamstahili hivi ili tuepukane na huu usumbufu tunaoupata tukienda kwenye hivyo viwanja vyatundege, ni usumbufu mkubwa sana na ni kero kubwa sana haituletei heshima nzuri Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kinachonisikitisha ni kwamba, ukarimu wetu umezidi mno, wenzetu wanapitia hapo *VIP* lakini sisi tunapokwenda kwenye hizo nchi hiyo hali haipo. Hatutetei kwamba Wabunge wawe *VIP* muda wote lakini ile heshima basi iwepo, kama sisi tunajaribu kuwa wakarimu basi na wao wawe wakarimu na wenzetu wa mambo ya nchi za nje wajaribu kutuambia au kuwaelimisha hawa wenzetu, jamani mnayoyafanya wananchi wetu sisi hawaridhiki nayo au viongozi wetu pia hawaridhiki nayo haya mnayotufanyia. Naomba Mheshimiwa Waziri alitazame hilo kwani halituletei sifa nzuri pale mnapoongozana watu watatu msafara mmoja mwagine anaambiwa nenda huku, wewe mwagine pitia huku, haileti picha nzuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuchangia ni jinsi ambavyo Wizara inavyofanya kazi kwa bidii na katika kipindi hiki kwa kweli Mheshimiwa Waziri Membe na Naibu wake wamefanya kazi ambayo inaonekana machoni mwa Watanzania. Nawaombea Mheshimiwa Membe na Mheshimiwa Balozi kwa wapiga kura wao kwani muda mwangi hawapo Majimboni wawavumilie kwani wanayoyafanya yanaonekana machoni mwa Watanzania. Nawapongeza sana na kuwatakia kila la kheri, wafanye kazi kwa bidii na tutashirikiana nao kwa hali na mali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kuyasema hayo, naomba niwatakie kila la kheri watu wote wa Wizara, waendelee kuwa na juhudni kubwa ya ufanyakaji kazi lakini yale mambo ya msingi ambayo yanakera, ambayo ni kero kati ya Tanzania na nchi nyingine ni vizuri wakayafanya kazi ili nchi yetu iwe kwenye heshima kubwa kama ilivyo hivi sasa.

Tanzania sasa inakopesheka, Rais amesema, Tanzania sasa ina heshima basi heshima hiyo iwe kwenye kioo kizuri cha Wizara ya Mambo ya Nchi za nje kwenye chini ya uongozi mahiri wa ndugu yangu Mheshimiwa Bernard Membe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo narudia kusema tena nawapongeza wote walioshiriki kuandaa hotuba, naipongeza Kamati ya Mambo ya Nje kwa hotuba yake nzuri, wamejipanga chini ya usimamizi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masilingi, wanaisaidia sana Wizara lakini kubwa zaidi pale ambapo inapofikia ukaguzi wa hizo Balozi zetu basi ifikie mahali Kamati inayohusika iende kwenye hizo Balozi kama zilivyo Kamati nyingine zinavyokwenda kwenye mikoa kuangalia mapato na matumizi ya maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niseme machache kuhusu Wizara hii muhimu ya Mambo ya Nje. Kwanza kabisa nikupongeze wewe binafsi kwa kuwa Rais wa *CPA*. Unafanya kazi ya kidiplomasia.

Pia, hongera sana lakini pia niwapongeze Waziri Mheshimiwa Membe, Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Seif Idd, Naibu Katibu Mkuu Balozi Sanga kwa kazi nzuri pamoa na timu yenu yote mnayofanya nayo kazi bila kusahau juhudhi kubwa alizozifanya Katibu Mkuu ambaye ni mgonjwa ambaye bila shaka atapona baada ya muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe pungezi za dhati kwa maafisa wetu wa Kibalozi walioko nje ya nchi yetu ambao wanafanya kazi nzuri na kwa kweli katika mazingira magumu sana. Nadhani Waheshimiwa Wabunge wenyewe ni mashahidi, tunapotembea nje ya nchi tunakuta maafisa wetu wanahangaika kweli, kwanza ni wachache sana katika Balozi zetu na vitendea kazi ni duni sana.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka nilikwenda pale Addis Ababa nikakuta kuna gari mbili. Moja ni gari ya Balozi, *Benz* ya zamani iliyochakaa chakaa halafu na gari eti ndiyo gari ya ofisi ambayo kwa kweli nilikataa kuingia kwenye gari hiyo kwa sababu ni gari chafu sana na wanasema ndiyo gari tuliyokuwa nayo na mahali kama Addis Ababa pale ni mahali muhimu sana.

Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri kuna vituo na vituo, kituo cha Addis Ababa ni muhimu sana, ni kituo ambacho ndiyo sura yetu pale. Kwa hiyo, naomba sana waongeze vitendea kazi na watumishi.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi nilivyokwenda pale nilikuta kuna watumishi wawili tu na Balozi watatu na kwa kweli kwa namna ya pekee nimpongeze sana Balozi Mangachi ambaye nasikia amehama, amekwenda Nigeria, anafanya kazi nzuri sana lakini kubwa zaidi alilonifurahisha Balozi yule alikuwa pia ni Balozi wa Kiswahili pale *African*

Union na napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atueleze, Balozi Mangachi pale Addis alianzisha mkakati wa kujenga kituo cha Kiswahili kwa ajili ya AU na tukapata kiwanja na kwa bahati alinitembeza, nikatembelea na kukiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliporudi hapa wakati ule na Waziri wangu Profesa Maghembe tukiwa *Labour* tukam-*engage* aliyekuwa Waziri wa *Foreign Service* wakati ule Mama Migiro pamoja na Balozi Sanga jambo hili analifahamu vizuri sana. Akasema wanapeleka pesa kwa ajili ya ku-*develop* kiwanja kwa ajili ya kuwa na Kituo cha Kiswahili Addis Ababa pale kwa ajili ya soko letu la *AU*.

Sasa nataka baadaye nijue mkakati wa kuendeleza kiwanja kile kwa ajili ya Kituo cha Kiswahili umefikia wapi. Kiswahili ni bidhaa na bidhaa hii lazima iendelezwe. Sasa ningependa baadaye Mheshimiwa Waziri anieleze juhudhi hizo zimefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu Balozi zetu mwaka jana mwezi Novemba, mimi nilipata bahati ya kuongoza ujumbe wa vyombo vyta habari kwenda Nordic, nikaenda Sweden pale, nikakuta Ubalozi wetu wa Sweden uko hoi bin taabani, una watumishi wawili, watatu hivi na unahudumia nchi sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Balozi za Nordic zina historia na sisi tangu enzi za hayati Mwalimu Julius Nyerere ni Balozi za Sweden, Norway, Denmark na Finland ni Balozi zimekuwa zikitusaidia tangu tunapata Uhuru wa nchi yetu. Lakini pale kwa kweli hali si nzuri watumishi ni wachache sana na kwa namna ya pekee kwa kweli naomba nimpongeza sana Balozi Dr. Benny Mosses anafanya kazi sana na kubwa sana pale anajituma sana. Alituhangaika sana sisi tulipofika pale akatupeleka *airport* saa tisa za usiku, anafanya kazi ya kujituma kweli kweli Balozi yule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninachosema Mheshimiwa Waziri Balozi kama hizo ambazo ni *strategic*, maana Ubalozi wa Sweden hauwezi kuwa kama Ubalozi wa Burundi haiwezekani hata kidogo lazima muwe na Balozi ambazo ni *strategic* ambapo rasilimali zinapelekwa pale kama alivyosema jana Mheshimiwa Rais, tunatoa fedha ili tupate fedha.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri Balozi hizo ambazo ni *strategic* zipo nyingi ziweze kupewa kipaumbele na kwa bahati sasa Mheshimiwa Waziri ye ye ni mzoefu mkubwa kwenye Wizara na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi yupo hapo ana uzoefu wa muda mrefu na Balozi Sanga na timu yake. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, nahisi kutamka kwamba Ubalozi wa Sweden siyo kama Ubalozi wa Burundi inaweza ikatuletea tatizo kidogo, nadhani ungesahihisha hilo. Kwa sababu Burundi ni majirani zetu.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, na wewe ni mwana diplomasia, nakushukuru sana kwa kunisahihisha vizuri. Nimesema basi Balozi hizi hazifanani. Balozi zote zina hadhi sawa na Burundi ni majirani zangu nisije nikagombana nao bure nikiri kwamba nao ni Ubalozi muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna Balozi Mkakati basi, tuziite hivyo. Lakini ni kweli kama nilivyosema Burundi siyo Ubalozi mbaya au mdogo hapana, ni Ubalozi ambao pengine kimkakati unawenza usiwe sawa sawa na Ubalozi mwingine kama wa Sweden na Denmark. Ahsante kwa sahihisho hilo, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja yangu ya msingi hapo ni Wizara hii kuwa na Balozi *strategic* zile ambazo zitatusaidia kuweza kuendeleza sekta mbalimbali za uwekezaji kama utalii na kadhalika. Hoja yangu ya msingi ilikuwa ni hiyo. Tena umenikumbusha na Burundi wamenialika niwatembelee loh, nilitaka kufanya kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilipenda niliseme kwa kweli ni kuipongeza kwa dhati kabisa Wizara hii kwa juhudu kubwa sana za kufanikisha ujenzi wa daraja la Malagarasi. Sisi wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwa kweli tunapongeza sana safari hizi mnazozifanya Mheshimiwa Waziri, juhudu hii alianza nayo Mheshimiwa Rais akiwa Waziri wa *Foreign Affairs* wakati ule, akaanzisha mchakato huu kwa wenzetu wa Korea Kusini na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri umeendeleza na tunashukuru kwamba sasa daraja hili la Malagarasi sasa limefika mahali pazuri, linaanza kujengwa ikiwa ni pamoja na zile kilometra 45 za lami kwenye bonde la mto wa Malagarasi hadi Nguruka.

Kwa kweli sisi watu wa Kigoma hiyo ni faraja kubwa sana na tunaomba kama alivyosema Mheshimiwa Ramadhani Maneno pale muendelee kutembea duniani, endeleeni kutembea duniani kwa manufaa ya Watanzania na mjue kabisa tunawaungeni mkono na wananchi wa Kigoma wanawaunga mkono sana katika ziara zenu hizo ambazo zina manufaa. Mnachokirejesha nyumbani ni mrejesho muhimu sana, tunasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa jambo la tatu, ambalo ningependa kulizungumza kidogo ndugu yangu na jirani yangu Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi ameligusia kuhusu wakimbizi. Lakini mimi nilizungumzie katika sura hii ya hizi shughuli za *MONUC* katika Kongo ya Mashariki. Shughuli za *MONUC* katika Kongo ya Mashariki ni shughuli za kiulinzi, kiusalamu na kiitafiki katika Kongo ya Mashariki na wanatumia rasilimali nyingi sana za Mkoa wa Kigoma pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, wanatumia Bandari ya Kigoma na wanatumia barabara zetu za Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba tu, kwa sababu jambo hili nakumbuka hata Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, mimi niliteta naye nikazungumza naye jambo hili analifahamu vizuri. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, hawa ndugu zetu wa *MONUC* maadamu wanafanya kazi nzuri kwa ndugu zetu wa Kongo ya Mashariki ambao ni majirani zetu basi wakarabati miundombinu wanayoitumia katika Mkoa wa Kigoma.

Kwa mfano, wana ndege kubwa zile za mizigo (*cargo plane*), wana helkopita kubwa kabisa zile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ndiyo mara ya kwanza kuona helkopita inabeba magari ya kijeshi sita na zinatua pale Kigoma. Kwa kweli zinaharibu ule uwanja wetu wa ndege ambao ni uwanja wa ndege wa charangawe na Mheshimiwa Spika, umeutumia na umeuona. (*Makofi*)

Sasa ilikuwa ni ombi tu na hili pia tulimdokezea Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, mlifuatilie mnapokuwa kwenye vikao vyenu. Mheshimiwa Bernard Membe nimeambiwa kwamba unasafiri hivi karibuni kwenda New York, hebu zungumza na hao watu, tunahitaji fedha kidogo kukarabati ule uwanja wa ndege kuweka lami ili ndege zao ziendelee kutumia uwanja ule kwa maslahi ya wenzetu wa *Eastern Congo*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana hili la kuweka lami kwa uwanja wa ndege wa Kigoma, miundombinu ya bandari yetu ya Kigoma na barabara hizi mbili zinazoingia katika uwanja wa ndege, barabara ya kutoka Mwanga hadi uwanja wa ndege na barabara ya kutoka Mji wetu wa historia wa Ujiji hadi pale uwanja wa ndege. Si fedha nydingi kazi inaweza ikafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumze ni kuhusu hali tete iliyopo katika nchi ya Burundi. Katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 20 amesema mambo yanakwenda vizuri Burundi, labda nimpe taarifa tu wale ni majirani maana Jimbo langu linapakana na Burundi hali si shwari. Hali si shwari na nafikiri kuna haja kubwa sana ya Serikali yetu kuendeleza shughuli za kidiplomasia kwa wenzetu wa *Palipehutu – FNL* ili waweze kusikilizana na wenzao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako, Mheshimiwa Waziri ni majuzi tu wanadai asilimia 50 ya viti kwenye Serikali ya Burundi, jambo ambalo wenzao wamekataa, sasa inaweza ikatuletea hali tete na hatimaye kuweza kuzalisha wakimbizi wengine wengi katika eneo letu hili la Kigoma ambao tunapokea wakimbizi wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumze ni diplomasia ya kiuchumi na biashara. Mimi nataka kufahamu katika mkakati huu wa diplomasia hii ya biashara na uchumi ni namna gani Balozi zetu zinatusaidia katika kusaidia harakati za uwekezaji katika nchi yetu na hasa kutambua wawekezaji na makampuni makini yanayokuja kuwekeza hapa kwetu ili kuerekana na makampuni ya Wazungu wajanja wanaokuja wengi tu hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri wakati umefika Balozi pengine Wizara waanzishe kitengo cha ukachero wa biashara maana tulidanganywa kwa mfano Richmond hii, akina Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe walikwenda mpaka Texas, Marekani kule, kumbe kuja kukuta Richmond ni duka la vitabu. Hivi kweli Ubalozi wetu pale Marekani, Washington wasingefanya kazi hii wakagundua hili mpaka watu kuhangaika kiasi hicho kwenda mpaka Taxes. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nipo kwenye Kamati ya Nishati na Madini, juzi tunaambiwa wenzetu wa Barrick waliidanganya Serikali kwamba eti *stock exchange* za duniani hazipendi kuona Serikali inamilihi hisa kwenye migodi. Mambo ya uongo tu haya, hivi Balozi zetu haziwezi kutusaidia kufanya ukachero tukayajua hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri wakati umefika wawekezaji hao na mikataba hii Balozi zetu zitusaidie kujua wajanja hao, kwa sababu wajanja siyo Waafrika peke yao, wajanja ni pamoja na wazungu wajanja wajanja wanaokuja hapa, wengine hata sifa hawana. Balozi zetu zitumike kutusaidia kuweza kuwatambua wajanja hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie na Azimio la Yokohama kwenye kitabu cha hotuba yake Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 30 na 31. Pengine mimi ningependa kujua yale mambo ambayo Serikali ya Japan imeahidi, *understanding* yangu ni kwamba wameahidi kwa Tanzania. Sasa nataka kujua miradi ile mikubwa, kwa mfano, kilimo cha mpunga, uwekezaji binafsi wa watu kutoka Japan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kujua kuna mkakati wa namna gani hasa? Ni eneo muhimu sana nataka kujua ni mkakati wa namna gani na wanawekeza wapi ili tugawane rasilimali hizi jamani. Kwa mfano, mimi ningetarajia kwamba wawekezaji hawa wakija moja ya maeneo ya kuelekezwa ni kwenye Ziwa Tanganyika, ni Ziwa ambalo halina mwekezaji hata mmoja katika uvuvi kwa mfano. Sasa ningeomba sana pengine baadaye Mheshimiwa Waziri na wenzake wanaweza kutueleza Azimio la Yokohama watupe *details* zake ni mambo gani hasa wanayoyazungumza, na miradi hii tutaigawanya namna gani katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilikuwa nataka sana kufahamu juu ya jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabla ya kengele ya pili na mimi nikubaliane kabisa na hoja ya Mheshimiwa Ramadhani Maneno, jamani *Dar es Saalam Airport* hakuna VIP pale, pale kuna vurugu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati natoka Ulaya mwezi Novemba, 2007 tumekuja na wafanyakazi wa *Saskatel* wanaokuja kuwekeza katika Kampuni ya Simu nao wanapita VIP, nao wamevaa kaptula ehee, pale hakuna VIP kuna vituko kama alivyosema Mheshimiwa Wilson Masilingi pale, kuna vituko fulani tu. VIP yetu haina hadhi na kwa kweli lazima *Foreign Affairs* wabadilishe hali hiyo. Watu wanaopita VIP jamani siyo kwa rangi zao ni kwa hadhi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninakubaliana kabisa na hoja Mheshimiwa Ramadhani Maneno kwamba jamani matumizi ya VIP lazima yaangaliwe siyo *Dick and Tom* wanapita kwenye VIP lounge. Sasa wazungu wamepafanya ni mahali pa kwenda hata kuvutia sigara jamani! VIP lounge lazima iwe na heshima yake. VIP maana yake inatumika kwa viongozi na watu mashauri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba sana jambo hili Mheshimiwa Waziri walifanyie kazi na watu wa itifaki ili kile chumba kiwe na heshima. Sasa chumba kile kinakuwa

kama alivyosema juzi kulikuwa kumejaa watu pale, watoto wanalia, wengine wanavuta sigara ni aibu tupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja hii, namuomba Mheshimiwa Waziri ayatekeleze au ayafanyie kazi baadhi ya mambo niliyoyasema. Nashukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Hiyo *VIP* mnayoisema wala siyo *VIP* ni chumba kilichopangwa kuwa Ofisi ya Meneja wa *Airport*, klijengwa wakati mimi nikiwa Waziri wa Ujenzi, *VIP* ilikuwa ijengwe pengine. Kwa hiyo, msigombanie hapo hapo, cha msingi hapo ni kwamba Serikali ijenge *proper VIP*. Tunaendelea Mheshimiwa James Lembeli, halafu wa mwisho ni Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah. (*Makofi*)

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Napenda kuanza kwa kumpongeza Waziri Mheshimiwa Bernard Membe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa Bajeti nzuri iliyosheheni kila aina ya maneno ya kulipa matumaini Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pongozi nyingine ni kwa Waziri mwenyewe Mheshimiwa Bernard Membe kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya na kwa kweli amedhihirisha kwamba ni Waziri ambaye anaweza kuifanya kazi yake kwa ufanisi mkubwa. Amekuwa ni kioo cha Tanzania sehemu mbalimbali za nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa ni mfupi kwa sababu utajikita katika sekta moja ndogo ya uchumi wa kidiplomasia(*economic diplomacy*), kimsingi naunga mkono sera hii. Lakini nina matatizo ya kuamini kwamba utaratibu huu uthalisaidia sana Taifa hasa katika masuala ya kiuchumi na yale ya kibiashara. Kila mzungumzaji aliyesimama hapa amesema tatizo la watumishi katika Balozi. Utakuta ubalozi una watumishi wawili, kimsingi wako pale kwa masuala yanayohusu diplomasia. Sasa ndani ya Bunge hili tunaelezwa kwamba masuala ya uthali siui na nini watafanya watu hawa. Sasa mimi nashindwa kuelewa ofisi yenye watu wawili itafanyaje kazi kwa tija? Wako pale wale wawili kwa masuala ya diplomasia. Sasa unawaletea tena na masuala ya uthali.

Mimi ningependa nizungumzie sekta ya uthali na utaratibu huu ambao umejitokeza hivi karibuni Serikali kupeleka fedha katika Balozi kwa ajili ya kutangaza vivutio vya uthali wa Tanzania. Mimi nasema kwa uzoefu nilionao utaratibu huu ni kupoteza fedha za walalahoi, hazifanyi kazi zilizokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya uthali au biashara ya uthali ni biashara inayohitaji utalaam na ni *very sensitive*. Mimi nina ushahidi wa kutosha niliwahi kwenda katika Ubalozi mmoja Stockholm ambako kulikuwa na maafisa wawili na hawa kulikuwa na mmoja pia alikuwa anajihuisha na kutangaza na kugawa makabrasha ya uthali wa Tanzania. Jambo la kusikitisha sana alikuwa anagawa makabrasha ambayo yalikuwa yanatumiwa na *TCC* wakati taasisi ambazo zilikuwa zinakwenda kwa shughuli maalum ya kutangaza uthali pale zilikuwa zimepeleka vipeperushi *latest*. Sasa mtu kama huyu

kweli anaitendea haki nchi yetu? Kwa hiyo, mimi nashindwa kuamini kwamba utalii unaweza kutangazwa katika nchi kwa kupitia ofisi zetu za ubalozi. Watumishi wengi walioko katika Balozi hizi wana taaluma zao kwa hiyo, suala la utalii ni *secondly*, wapo wengine wamekaa nchi za nje zaidi ya miaka kumi, anakuja mtalii pale anaulizia Gombe iko wapi (*how do I get to Gombe*), hajafika Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Gombe utaiuza kwa namna hiyo kweli? Mimi nafikiri Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje iishauri Serikali, taasisi hasa Wizara husika ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ipeleke waambata wa masuala ya utalii katika Balozi zetu. Tunaweza kuanza kwa kuchagua nchi ambazo zinatuletea wageni wa kutosha kama Marekani, Uingereza pale, Tokyo na China. Nakumbuka Balozi Sanga alipokuwa China ye ye mwenyewe alikuwa ana utashi wa kutaka kuitangaza Tanzania China. Kwa hiyo, mara kwa mara aliwasiliana na *TANAPA*, aliwasiliana na Ngorongoro ili aweze kupatiwa vipeperushi. Sasa hii inatokana na mapenzi ya mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kweli utaratibu huu umeanza kufanyiwa kazi mimi nilikuwa nataka Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje iniambie mwaka jana na tukatangaziwa humu ndani ya Bunge, kwamba kuna utaratibu wa kuitangaza Tanzania katika Jiji la London mabasi ya ghorofa 100 yatapambwa na vivutio vya Tanzania bango kubwa litawekwa pale *Hethrow Airport* shilingi milioni 600 zimepelekwa *London*.

Sasa mimi nataka Wizara inihakikishie na inithibitishie kwamba fedha hizi ambazo kimsingi zilitakiwa zipitishwe katika Ubalozi wetu wa London kama kweli zilipelekwa kupitia Ubalozi wa London ili Ubalozi uweze kufuatilia kuona matumizi ya hizi fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri anafanya majumuisho nitapenda aniambie je, fedha hizo zilipelekwa kupitia akaunti ya nani, pili ni mabasi mangapi ambayo yalipambwa na vivutio vya Tanzania ni sehemu gani pale *Hethrow Airport* bango linaloelezea vivutio vya Tanzania limewekwa? Nimepita pale London nina uzoefu na London nimeangaza sijawahi kuona kitu chochote kinachoonyesha *Tanzania the land of Zanzibar and Kilimanjaro*. (*Makofi*)

Napenda nipate ufanuzi wa haya mambo. Kwa sababu nina wasiwasi, wasiwasi wangu uko katika uzoefu nilionao. Fedha imepelekwa Ubalozi wa Tanzania - Malaysia kusaidia kutangaza vivutio vya Utalii wa Tanzania. Ningependa Waziri aniambie hiyo fedha imefanya kazi yake sawa sawa au imetumika vinginevyo. Lakini ninazo taarifa kwamba kuanzia mwezi wa nne haijapeleka mishahara Ubalozi wa Tanzania pale Malaysia. Kwa hiyo, hela ambazo zimepelekwa kwa ajili ya kutangaza Tanzania ndani ya Malaysia ndizo zimelipa mishahara ya *local staffs*. Sasa ni kweli tunawatendea haki Watanzania? Hela imepelekwa kwa shughuli nyingine inafanya kazi nyingine. Labda niulize ni kwa nini tunafungua Balozi katika nchi mbalimbali wakati uwezo wa fedha hatuna? Hii ni aibu kwa nchi yetu. Wale *local staffs* wakashajua kwamba hawa jamaa hawajapata mishahara *obviously* wanasema. Sasa haya ningependa nipate majibu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Bernard Membe, yeye mwenyewe binafsi kwa sababu utalii ndani ya damu yake umemfanya kila anapokwenda kutangaza utalii wa nchi. Wakati akiwa Ubalozini Canada mimi mwenyewe nakumbuka kwa wiki mbili tumefanya naye kazi ya kuitangaza Tanzania kule Calgali, Edmonton na kwa kweli tangia miaka ile mpaka leo bado anaifanya kazi hiyo. Basi mimi namuombea kwa Mwenyezi Mungu kwamba ampe afya njema na nguvu za kutosha aendelee kuitangaza Tanzania katika nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze Rais kwa kazi ambayo anaifanya. Kazi hii kimsingi ilitakiwa ifanywe na wahuksika, lakini inafanywa na kiongozi wa nchi pamoja na kwamba ni wajibu wake, lakini hatumtendei haki ana kazi nyingi za kufanya. Pale *New York* amefanya kazi nyingi za kuitangaza nchi yetu yeye mwenyewe binafsi. Kwa hiyo, napenda nimpongeze pia kwa kazi nzuri anayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania mara nyingine inanihuzunisha, utalii peke yake ungeweza kutuvusha kwenye matatizo tuliyonayo. Jana Mheshimiwa Rais hapa alisema ndiyo kwanza pato letu linalotokana na utalii limefikia dola bilioni moja, lakini sisi ni mabingwa wa kutangaza kwamba Tanzania ni nchi yenye vivutio vingi, ina nini, mipango yetu hapa ndani haiendi sawa sawa. Mheshimiwa Rais jana amesema ukitaka kula lazima uliwe. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa kwa nini Wizara hii ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje hazitaki kuliwa? Vivutio viko hapa, tumia fedha, *invest* kwenye *marketing* watakuja tu watalii. Lakini linapokuja suala la Tanzania kuwa na ofisi za mauzo ya utalii katika nchi mbalimbali hatutaki, inatafutwa njia za kuzila hizo fedha zingeweza kuwalipa hawa watu. Ni kwa nini na tutaendelea kuwa maskini kwa sababu hii pato la Tanzania kutoptera na utalii leo hii lingefikia labda dola bilioni tatu, nne. Kuna nchi hapa ambazo hazina vivutio kama vya kwetu. Lakini sisi wenyewe ndani kwa *interest* zetu tunakwamisha mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano tozo mbalimbali ambazo zimekuwa zikitozwa kwenye hifadhi, kwenye *game reserves* iwe za uwindaji, iwe za kuingia kupiga picha sisi wenyewe humu ndani ndiyo tunazikalia tunaziteremsha chini utapata nini? Uganda hapa ukitaka kwenda kumuona *Gorilla* kwa saa moja ni dola 400 mpaka 500 usipomuona ukitaka kuendelea kumwona *you pay again*. Sisi hapa tumelumbana hapa tembo wetu tunamuza kwa bei ya kutupa kila kitu. Sasa hili suala la umaskini litaishi lini? Rasilimali zetu tunazifuja sisi wenyewe. Mungu iko siku moja atatuadhibu kwa sababu vitu vyote tulivyonavyo vitatoweka, halafu sijui tutaanza kujisifia vitu gani. Madini yataisha pia hivi hivi na tatizo kubwa ni ubinafsi wa watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba nimalizie hapo kwa kusema kwamba ningependa sana, nitafurahi sana Mheshimiwa Waziri anieleze zile shilingi milioni 600 zilizokwenda London pale zimepitia akaunti gani, lakini pili idadi ya mabasi ambayo yalipambwa vivutio vya Tanzania na kwa miezi mingapi kwa sababu hayapo tena na lile bango la Tanzania pale *Hethrow Airport* liko sehemu gani. Ufanuzi mwengine ni fedha zilizopelekwa Malaysia kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii wa Tanzania

zimetumika kama ilivyotakiwa au zimetumika kulipa hiyo mishahara ya *local staffs?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na nimesimama mchana huu nikiwa mchangiaji wa mwisho na hasa kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia ndani naomba tu nichukue nafasi hii nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii Mheshimiwa Bernard Membe, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Balozi Seif Idd pamoja na Naibu Katibu Mkuu Balozi Sanga. Lakini pia nitumie fursa hii nimtakie tu afueni ya haraka sana Mheshimiwa Katibu Mkuu, Balozi ambaye yuko nje kwa matibabu nchini Ujeruman. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue nafasi hii tena nikupongeze wewe mwenyewe kwa hivi juzi kwa uteuzi ulioupata kuchaguliwa kuwa Rais wa *CPA* na hii kweli inaonyesha ni jinsi gani nchi yetu inavyoweza ikawa inathaminika nje ya nchi yetu na kwa majirani zetu na duniani kote kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu Tanzania sasa imepata fursa katika *CPA* wewe ukiwa Rais, lakini pia tunaye Katibu Mkuu, wa *CPA* anayetoka Tanzania, Balozi Dr. William Shija. Kwa hiyo, hili ni suala la kujivunia unapoweza ukawa kwa wakati mmoja mmeshika nyadhifa kubwa na zinazotambulika hapa duniani.

Mheshimiwa Spika, labda kabla sijaendelea mimi naomba *ni-declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo, katika haya yote yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri na yale maoni yaliyotolewa na Kamati, mimi ni mmoja kati ya wale walioshiriki kwa dhati kabisa ili kuiboresha na kuweza kuhakikisha Wizara hii inafanya kazi kwa maslahi ya nchi yetu na maslahi ya Tanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mwenyekiti wetu na Wanakamati kwa ujumla kwa ushirikiano ambao kwa kweli mara kwa mara tunapoona kwamba tulikuwa tunapata mikwamo, lakini tulikuwa tunahakikishiwa kwamba tunashirikiana ikiwa ni pamoja na wewe na ofisi yako, lakini na Wizara kwa kweli nawapongeza sana, ushirikiano ambao tunakwenda nao ni ushirikiano mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia juu ya kuingia katika mfumo wa uchumi duniani huwezi ukakwepa suala la sayansi, teknolojia na mawasiliano. Lakini pamoja na hayo huwezi pia ukakwepa juu ya ushirikiano wa wewe nchi baina ya nchi zingine na jukumu hili kwa nchi yetu ya Tanzania inasimamiwa na Wizara hii ya Mambo ya Nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Chama chetu ya mwaka 2005/2010 nitaomba kwa ridhaa yako niinukuu inazungumza ukurasa wa 143, ibara ya 117. Inasema hivi; “Mwelekeo wa sasa wa sera za CCM ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa unaongozwa na Sera ya Diplomasia ya Uchumi, hivyo Ofisi zetu za Ubalozi zinahitaji ziimarishwe kiutaalam.”(Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitarudia hapa, Ofisi zetu za Kiubalozi ziimarishwe kiutalam, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inazungumza katika kipindi cha mwaka 2005/2010 msisitizo utakuwa katika kuendeleza diplomasia ya uchumi na kuchukua hatua zifuatazo na hizi hatua zimetajwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni dhahiri kabisa Ilani imetuelekeza na ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri haya yote ameyaeleza yanayotokana na Ilani yapo ukurasa wa 57. Ameorodhesha malengo ya Wizara katika mwaka wa fedha 2008/2009. Ametaja kutoka kipengele cha kwanza mpaka kipengele cha sita yote hayo ameyataja kutokana na Ilani. Sasa hoja yangu ni nini na sisi kwa Wanakamati kwa ujumla ni juu ya hali ya jinsi tunavyoichukulia, ufinyu wa Bajeti wa Wizara hii ili kuharakisha haya ambayo pengine Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyapendekeza ndani ya Bunge lako Tukufu, ni dhahiri kweli Balozi zetu bado zina hali mbaya na hasa tukizungumzia suala hili linaloitwa la utaalamu.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu nyingi ukiziangalia zinao waambata lakini utakuta ni waambata wa Kijeshi, waambata wa masuala ya kisiasa lakini tunahitaji zaidi ya hapo. Tunahitaji tuwe na waambata mbalimbali kulingana na hali ya nchi kama ambavyo amezungumza Mheshimiwa James Lembeli, sasa hivi. Huwezi likatokea suala linalohusiana na madini likawa linahitaji *negotiation* kati ya nchi na nchi leo tukaja tukaitumia Wizara ya Nishati na Madini kutoka hapa ndiyo ikaenda kufanya suala hilo lakini kama tuna muambata anayehusika na masuala ya madini katika nchi inayohusika hilo linaondoka na wala halina tatizo. (Makofi)

Kwa hiyo, hili ni suala la Bajeti na naamini kwamba kwa sababu Wabunge mmeona na kwa sababu Bunge hili tunahusika sasa katika kuandaa Bajeti mimi nilikuwa nafikiri katika *priorities* zinazokuja ili tuone tuzijengee uwezo Balozi zetu ili tuweze kuhakikisha sasa zinapata hili suala la utaalam ambayo itakuwa ni hatua mojawapo ya kufanya kwamba Wizara inafanya kazi vizuri. Naamini kabisa kama tutaziimarisha Balozi zetu hata haya masuala tunayoyalalamikia amezungumza nafikiri kama siwezi kukosea amezungumza Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, alizungumza masuala mbalimbali hasa ya mikataba. Tukatoa muambata anayehusiana na masuala ya kisheria akawa yupo ofisi ya Kibalozi kule katika Ubalozi wetu akafanya shughuli hizi zote za kitaalamu, kwa hiyo, hata mikataba ya nchi ikawa inapitishwa atajua pamoja na hiyo tunayosema kwamba kwa ajili kama upelelezi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya nje yako kwa namna tofauti, lakini nilikuwa nafikiria na kwa sababu tunasema tunafanya kazi kwa uwazi zaidi na hatuna kinachotuzuia, nilikuwa nafikiri kwa kuwa hata haya Mashirika yasiyo ya Kiserikali yamekuwa na uwezo wa kuweza kuwa wana *access* ya kuwasiliana na marafiki nje ya nchi naamini kwamba wana marafiki nje ya nchi na wanawapatia misaada kwa ajili ya kuendeleza maendeleo ya nchi badala ya Serikali nao ni vizuri ikafikia wakati nao

wakatambulika kule Balozi zetu za nje ili kwamba Balozi ikafahamu ikajua kwamba kuna Shirika fulani la Tanzania lina mawasiliano na Shirika fulani kwa ajili ya mambo haya ya kimaendeleo ya nchi yetu, hii itasaidia sana. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, nije nizungumzie suala la ushirikiano na hasa nchi za majirani zetu hawa. Nikirudi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 144 kifungu (c) imeeleza bayana juu ya zile kazi ambazo Wizara inapaswa na nchi yetu jinsi ilivyo juu ya ushirikiano ya Kimataifa, kipengele hiki kinasema naomba ninukuu; “Kushiriki katika kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Uchumi Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Afrika (AU), Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande wowote na Umoja wa Mataifa.” (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, nafurahishwa sana na msimamo wa nchi yetu iliouonyesha hivi majuzi baada ya migogoro ya nchi za Kenya na nchi za Zimbabwe, hii ndiyo kutekeleza hasa yale yaliyopo katika ilani. Migogoro iliyotokea kule Tanzania ilisimama kwa msimamo wake kwa miguu yake kutekeleza kuonyesha kwamba yenyewe haiwezi ikawa inafungamana na upande wowote. Lakini nitumie fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri Mheshimiwa Bernard Membe kwa kazi nzuri waliyoitumia wakati ule wote kuweza kuelezea hali halisi jinsi ilivyo na msimamo wa Tanzania. Lakini pia nichukue nafasi hii nizungumze niseme kwamba yaani naomba sasa kwako hili suala la mazungumzo la hawa watu ambao tunashirikiana nao naomba tufikie wakati tubadilike, tuwaeleze wazi juu ya kufanya mabadiliko, tuwe ni watu ambao tunaendana na watu tuende na ushirikiano wa wanadiplomasia wa kweli tusiwe tunaendelea tu muda wote kwa kuwa na migogoro ambayo haina maana kila siku tutakuwa tunafanya utatuzi wa migogoro. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Bernard Membe pamoja na Mtukufu Rais kwa kuwa ni wanadiplomasia waliokomaa basi naamini juhudhi hizi wanazifanya kwa dhati kabisa na mambo yote yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tena kuhusiana na ilani kipengele “H” ukurasa 145; “Kutambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Ughaibuni (*Tanzanian diaspora*) na kuweka utaratibu wa kuwawezesha kuchangia maendeleo ya nchi yao. Napongeza tena Wizara hii ya Mambo ya Nje na kweli kazi hii imeanza kuifanya vizuri hasa tulipoanzia pale kwenye Mkutano wa *Sullivan*, hii ilikuwa tunasema ni *African in the diaspora*, lakini pamoja hawa ni Waafrika ambao wanaishi nje ya Bara la Afrika, lakini naipongeza sana kazi iliyoanza na inayofanywa kwa sababu jana kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais tumeelezwa mafanikio ambayo yameanza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema kazi hii iendelee vizuri na hasa napongeza sana ule mkutano jinsi ulivyoandaliwa na nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mratibu wa Mkutano ule Mama Shamim Nyanduga, kwa kweli aliweza kufanya kazi kubwa sana na ambayo kazi hiyo inahitaji ipongezwe na watu wote. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie na hizi changamoto mbalimbali ambazo zinakuja na tunashiriki. Mimi labda nianzie na *Helsinki process* ambayo ilianzishwa mwaka 2003. Katika hotuba Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba huu mchakato itakapofika mwaka 2008 mwezi Septemba basi ripoti itakuwa inakabidhiwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. (*Makofi*)

Naamini changamoto ni nzuri lakini changamoto hizi zinahitaji pia tuwe tunaona *impact* yake ni nini. Nilikuwa nafikiri hilo ni zuri sana, lakini tuwe tunajua kwamba hizi changamoto zinaishia ishia vipi. Kwa mfano mmoja naweza kuzungumza tulikuwa na changamoto moja iliyowahi kuwepo inaitwa *New Partnership for Africa Development (NEPAD)*, lakini hii changamoto hata ilipoishia tayari tupo pale imeshaingia kwenye APRM.

Mheshimiwa Spika, sasa ni muhimu tukawa tunafahamu tunapoanzisha changamoto ya kwanza tunakwenda na changamoto hii ya kwanza tulipoishia ikaja changamoto nyingine tukajua kwamba hapa tuliishia vipi na hapa tunaendelea vipi. Lakini kama tutakuwa kila siku tu tunakuja na changamoto mpya tukaingia tukatoka changamoto hii tukaingia katika changamoto hii bila ya kujua ile changamoto ya kwanza iliishia wapi kwa kweli bado Watanzania walio wengi watasikia tu kwamba ni kitu gani na hawajui ni kitu kipi kinachozungumzwa na hawajui kimefikia utekelezaji wake wa awali.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru tena wewe mwenyewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii na pia nimpongeze Waziri tena pamoja na Naibu wake pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na niwatakie kheri tu katika utekelezaji wa majukumu ya Bajeti hii ya mwaka 2008/2009 na Mungu awajalie ili tutakapokutana tena basi tutakapokwenda katika Bajeti inayokuja *inshallah* mambo yatakuwa mazuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Juma Killimbah.

Waheshimwa Wabunge nimepata maelewano na Mheshimiwa mtoho hoja Waziri wetu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwamba watahitaji dakika 50 tu badala ya 75 na kwa maana ya majumuisho na wamegawana kama ifuatavyo; Mheshimiwa Naibu Waziri Balozi Seif Idd ataongea kwa dakika 15 halafu Mheshimiwa mtoho hoja ataongea kwa dakika 35. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Balozi Seif Idd, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na uzima hadi hivi sasa na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwako Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CPA uchaguzi wako huo ni heshima kwa Bunge letu. (*Makofi*)

Aidha, napenda nimponeze Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Waziri Mkuu na kuitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kura nyngi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwapongeza Mawaziri wote na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa tena katika nafasi zao mbalimbali. Pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunituea tena kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii. Hii inaonyesha imani kubwa aliyonayo juu yangu namuahidi kuwa nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kutekeleza kazi zangu kwa juhudini, maarifa, uaminifu na uadilifu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa msaada anaonipa wa kuniongoza na kunielekeza ili nitimize wajibu wangu kwa ufanisi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na naomba uendelee na utaratibu wako huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa kunivumilia wakati sipo jimboni kwani wanajua kazi ninazozifanya ni heshima niliyopewa mimi lakini pia wamepewa wao. Hata hivyo najua wananchi wangu wa Kitope hawana wasiwasi kwani hata kama sipo jimboni mambo jimboni humo ya kuwaaletea maendeleo yanakwenda vizuri. (*Makofi*)

Napenda kutoa pole zangu za dhati kwa familia zote zilizopoteza Waheshimiwa Wabunge wenzetu kwa nyakati tofauti na kwa hivi karibuni akiwa Mheshimiwa Chacha Wangwe. Nawaomba wawe wavumilivu, wastahimilivu na subira katika kipindi hiki kigumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo sasa napenda kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Michango yote iliyotolewa na Wabunge tunaithamini kwani ina nia ya kutuongoza katika kazi zetu Wizarani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nijibu hoja hizo moja baada ya nyine hoja, hizo ni nyngi na inawezekana sitoweza kuzimaliza zote katika muda niliopewa lakini mtoa hoja ataziendeleza. (*Makofi*)

Kwanza, Mheshimiwa Ramadhani Maneno ameulizia yaliyotokea Afrika ya Kusini dhidi ya wageni, Wizara ilichukua hatua gani? Wizara yangu ilifuatilia kwa makini sana, hatuna taarifa kuwa kulikuwepo Watanzania waliofariki katika matatizo hayo, lakini Watanzania wengi walifika Ubalozini na kutaka kurejeshwa nyumbani. Tulifanya utaratibu wa kuwarejesha Watanzania hao nyumbani na tulikodi basi na liliwafikisha nyumbani salama. Hao kwa wale waliotaka kurejeshwa nyumbani lakini wapo ambao hawakutaka kurudi nyumbani pamoja na matatizo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi amezungumzia juu ya nyumba ya Balozi wetu Geneva, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, kwamba nyumba hiyo sasa imeshatengenezwa na iko katika hali nzuri sana na iko sawa kabisa na heshima ya nchi yetu kama Balozi wa Tanzania. Waheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Michael Laizer na Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* wamezungumzia juu ya suala kwamba Serikali iangalie upya maslahi ya Mabalozi, makazi pamoja na ofisi zao nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuboresha maslahi ya watumishi nje upo katika *Foreign Service Regulations* ya mwaka 1979 ambayo inafanyiwa mapitio ili kwenda na wakati. Suala tunalishughulikia kwa kushirikiana na Taasisi nyingine zikiwemo Wizara ya Fedha na Uchumi na Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Suala la majengo limepeewa msukumo baada ya kazi kubwa ya Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama kufanikisha Wizara yetu kutengewa kasma ya maendeleo ambayo haikuwekwa awali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika pia tutatumia fursa zilizopo za ubia na Mashirika ya Hifadhi ya Jamii. Mpango wetu ni kuwa ifikapo mwaka 2017 Wizara iwe inamiliki majengo ya Ofisi na Nyumba katika Balozi zetu. Kwa kuanzia tutanunua jengo New York katika mwaka huu wa fedha ikiwa Bajeti hii itaidhinishwa na Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul Kimiti ametoa wazo la kufanyika kwa semina kuhusiana na faida ya diplomasia ya mikutano kama ule wa *Sullivan* haswa katika kusaidia kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kupunguza umaskini. Maoni haya ni mazuri na tumeyapokea na tutayaafanya kazi na kumpatia majibu. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Paul Kimiti amesemea kuhusu mikataba kwamba Tanzania kuridhia mikataba mingi na kujiunga na Taasisi nyingi za Kimataifa ambazo wakati mwingine tunashindwa kuzichangia na akauliza je, Wizara haioni kuwa kuna ulazima wa kuzipitia upya Taasisi zote na kuona zipi za manufaa kwetu na ni zipi sio za lazima sana tuzipunguze. Nchi yetu inanufaika vyema na taasisi hizi kwenye nyanja za kujenga uwezo au *capacity building*, ajira za wananchi wetu na kuunganisha nguvu na nchi nyingine katika kutafuta maslahi ya pamoja. Kimsingi gharama za kuwa nje ya taasisi hizi zinaweza kuwa kubwa kuliko kuwa wanachama wa taasisi hizo. Hata hivyo wazo la Mheshimiwa Mbunge limepokelewa na tutalifikari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Michael Laizer, ameulizia kuhusu vikao vya ujirani mwema au ametoa wazo kwamba vikao vya ujirani mwema vifanyike kati ya Tanzania na Kenya ili kuimarisha uhusiano mzuri na kupeuka kukamatwa kwa Watanzania katika eneo la mpakani la Namanga na kupelekwa Kajiado. Vikao vya ujirani mwema kati ya Tanzania na Kenya vinafanyika na isitoshe achilia mbali kufanyika katika sehemu za Mipakani lakini hata Mawaziri wetu Waziri wa Mambo ya Ndani wa Tanzania na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Kenya pia wanakutana kuzungumzia maslahi ya nchi

zetu na wananchi wake. Kwa hiyo, tumelipokea wazo hilo na tutalifikisha pia Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye na Mheshimiwa Juma Killimbah wamezungumzia Wizara ifanye jitihada maalum za kuajiri wataalam wa fani za uchumi na biashara ili iendane na diplomasia ya kiuchumi na biashara ili iendane na diplomasia ya kiuchumi. Pia Balozi zisaidie upatikanaji wa masoko na bidhaa zetu hasa za kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kuwapeleka waambata wa biashara katika Balozi zetu. (*Makofi*)

Wizara inazingatia ushauri huu na inakiri umuhimu wa kuongeza nguvu kazi yenye taaluma katika fani hizo. Kusaidia katika upatikanaji wa masoko ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yetu ya sera ya mambo ya nje yenye msukumo katika diplomasia ya uchumi. Wizara inakubaliana na ushauri huu na tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuangalia jinsi bora ya kulishughulikia suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fatma Mikidadi amesema semina zifanywe kuelezea maana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na jinsi ya kuimarishe pamoja na kutafuta nchi nyingine marafiki kama Comoro kuungana nao. Tumelipokea wazo lake na pia tunakubali wazo la kuungana na Comoro ni jema kwa kuwa azma ya Bara letu ni kuwa na Serikali moja ya Afrika, wenzetu hawa tutaungana nao tutakapofika hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Manju Msambya wamezungumzia je, Tanzania haioni sasa kuna sababu za kuwa na Ubalozi nchini Angola ili kutumia fursa za kiuchumi zilizoko nchini humo. Angola tulikuwa nao Ubalozi. Mwaka 1994/1995 wakati wimbi la kupunguza baadhi ya Balozi zetu kwa sababu za kiuchumi lilipokuja, haikuwa Angola peke yake ilipofungwa, ilikuwa Angola, *DRC*, Rwanda, Burundi, Netherlands. Kwa hivyo, tunaujua umuhimu wa kuwa na Ubalozi Angola na ndiyo maana tulifungua mara tu baada ya Angola kujikomboa. Kwa hivyo hili ni wazo zuri kila hali itakapoturuhusu tutaweza kuufungua Ubalozi wetu kule Angola pamoja na Netherlands sababu hata Netherlands nayo bado hatujafungua na iliingia katika mkumbo huo huo wa kufungwa wakati ule wa mwaka 1994/1995, lakini bado pale tunaye *Honorary Consul* ambaye anasaidia katika shughuli zetu za kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Kijiko amezungumzia Balozi ziwe na orodha za Watanzania katika maeneo ya uwakilishi ili waweze kusaidiwa pindi wanapokuwa na matatizo. Tumekuwa tukihusisha Jumuiya za Watanzania waishio Ughaibuni na umepata muitikio mzuri na ndiyo maana mara nyingi tunasema Watanzania wanapokwenda nje ya nchi wajitahidi kwenda kujiorodhesha Ubalozini. (*Makofi*)

Aidha, kama nilivyojulisha Bunge lako Tukufu Wizara imeamua kuanzisha Kitengo cha Watanzania waishio Ughaibuni, kitengo hicho kitasaidia kutatua changamoto hizi. Lakini niliwahi kujibu swali hapa Bungeni nikasema kwamba kila

Ubalozi una Maafisa wanaoshughulikia maslahi ya Watanzania na hivyo tutajitahidi kutekeleza maelekezo haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro ameeleza kwamba maofisa waliokaa kwenye vituo kwa muda mrefu ambao wameonyesha ufanisi na tija wasihamishwe. Kupelekwa na kurudishwa kwa maofisa katika Balozi zetu kunatawaliwa na Kanuni za Utumishi wa Nchi (*Foreign Service Regulation*), hatuwezi kupeleka maafisa kule wakakaa dumu daima. Bunge hili hili litanilaumu kwamba kuna maofisa wengine huko wamegeuka wafalme, kwa hivyo, utaratibu wa *Foreign Service Regulations* utaendelea kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis ameulizia je, Tanzania inaunga mkono wazo la kuwa na Serikali moja ya Afrika. Ndiyo tunaunga mkono kwa sababu huo ni uamuvi wa Umoja wa Afrika ambao Tanzania ni mwanachama wake na kwa hivyo tunaunga mkono suala la Serikali moja wakati utakapofika. Mheshimiwa Kabwe Zitto, yeye anasema kwa nini hotuba ya Bajeti imeshindwa kutambua juhudzi za Mtanzania Dr. Salim Ahmed Salim katika suala zima la Darfur au ni siasa za uchaguzi mwaka 2005? Ni vipi Serikali na hasa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imemshirikisha Dr. Salim Ahmed Salim katika uamuvi wake wa kupeleka Jeshi la kulinda amani Darfur. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua mchango mkubwa sana wa Dr. Salim katika mgogoro wa Darfur. Napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba katika hotuba yetu ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 aya ya 23 ukurasa wa 12 ilielezwa kwa undani mchango mkubwa wa mwanadiplomasia huyu mkongwe wa Tanzania. Kwa hivyo, hakuna suala kabisa la uchaguzi wa 2005. Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed amezungumzia nini kimezuia Tanzania na Umoja wa Afrika angalau kulaani wale wanaoendeleza mauaji na mateso kwa wananchi katika Jimbo la Darfur nchini Sudan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa mstari wa mbele kupinga na kukemea aina yoyote ya udhalilishaji na ukiukwaji wa haki za binadamu katika jimbo la Darfur. Ikumbukwe pia tulikuwa Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mwaka 2006 tulikuwa sehemu ya uamuvi wa kupeleka Jeshi la kulinda amani la Umoja wa Mataifa. Aidha, Tanzania ilitoa ahadi ya kupeleka kikosi cha kulinda amani chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa azma hiyo iko palepale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Kabwe Zitto, ameuliza kwa kuwa Mheshimiwa Waziri hajagusia kitu kuhusiana na Mapinduzi ya Kijeshi ya Mauritania, naomba kauli ya Serikali. Kauli ya Serikali inaendana na yale maamuvi ya Umoja wa Afrika Tanzania haiyatambui, haiungi mkono Mapinduzi hayo, msimamo wa Umoja wa Afrika uko wazi kwamba Umoja wa Afrika hawatambui Mapinduzi yanayofanywa kwa kuangusha Serikali halali zilizowekwa katika nchi hizi, kwa hivyo, Tanzania haitambui Mapinduzi hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed ameuliza ni nini msimamo wa Tanzania.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliwasilisha jana asubuhi lakini nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri waliyoitoa wakati wa kujadili hoja niliyoiwasilisha.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 47 wamechangia na kati ya hao 17 kwa mazungumzo na wengine 30 kwa maandishi na jumla ya maswali 92 tumeulizwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema mapema kwamba hatutaweza kujibu maswali yote 92, tunaahidi kuyaweka kwenye maandishi maalum na baadae kijitabu hicho kitatolewa kwa Waheshimiwa Wabunge ili waweze kupata majibu sahihi ya maswali yao. Lakini yapo maswali machache ambayo tumechagua kuyajibu hapa hapa.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kwa kuongea hapa Bungeni kama ifuatavyo; Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Athumani Maneno, Mheshimiwa Kilonsti Mpologomyi, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale waliochangia kwa maandishi napenda kuwatambua kama ifuatavyo; Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalosyi, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Ludovick Mwananza, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Dr. Omar Kigoda, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Ruth Msafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana katika hotuba yangu sikuwatambua wahisani ambao wanaisaidia sana nchi hii, napenda kwa maksudi kabisa na kwa rekodi nitambue nchi

rafiki pamoja na nchi Wahisani ambao wanaisaidia sana nchi hasa katika Bajeti (*GBS*). Nchi hizo ni pamoja na Norway, Marekani, Sweden, Finland, Canada, Denmark, Japan, Uswiss, Uhlanzi, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Hispania, China, Korea, Kuwait, Italia na Ireland. Napenda pia kwa ujumla niyatambue Mashirika yote ya Kimataifa ambayo yameisaidia nchi yetu kama vile *IMF* na *World Bank*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza na suala la kiutawala kabla sijaenda kwenye masuala ya kidipolimasia ya Afrika na Tanzania kwa ufupi. Swali kubwa ambalo jana niliulizwa ni kuhusu matumizi ya shilingi 4,100,127,574/= ambayo yalitumika vibaya na Balozi zetu katika kipindi cha ukaguzi wa mahesabu na lililetwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Kwanza napenda kushukuru kwamba katika Balozi zetu 32 Balozi 22 sasa zimepata hati safi tofauti na mwaka jana ambapo Wizara yangu haikupata hati safi na Balozi saba pamoja na mmoja ndizo zilizoleta tatizo lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa matumizi ya ruzuku ya shilingi 1,531,000,000/= maelezo yake ni kwamba hapa hapakuwa na suala la upotevu bali ni suala la nani awe Mkaguzi wa Chuo cha Diplomasia. Chuo cha Diplomasia kina utata kwa sababu ni Mkataba kati ya Chuo na Msumbiji kukawa na Kampuni maalum iliyoteuliwa kufanya mahesabu ya Chuo cha Diplomasia. Kwa hiyo, watu wa Ukaguzi walipokwenda kule wakakuta inakingana yaani kwa mujibu wa sheria inabidi yule Mkaguzi ndiyo azikague na si Mdhibiti Mkuu wa Serikali. Tunalifanyia utaratibu rekebisho hilo. Lakini pesa zile hazikupotea likikuwa ni tatizo la Ukaguzi haukufanyika na Mdhibiti wa Serikali kama ilivyokuwa imepangwa na fedha zilizokuwa zikaguliwe ni hizo shilingi bilioni 1.5 na zipo na tunangoja ku-clear hili suala la Msumbiji ili watu wetu wa Udhibiti wa Mahesabu na Mkaguzi wetu aweze kulikagua hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la karadha la thamani ya shilingi 71,832,169,000/= hii ilikuwa ni mikopo ya Maofisa wetu Balozini na inahusu samani za majumbani mwao. Maafisa hao wanakatwa fedha hizo kutoka kwenye mishahara yao kwa mujibu wa taratibu zilizopo na fedha hizi hurejeshwa zote kwa wakati unaostahili. Kwa hiyo, sasa hivi Maafisa wetu wanaendelea kukatwa zile shilingi bilioni 71 na mwakani tutazitolea taarifa. Masurufu ya shilingi 13,819,000/= fedha hizo zimerejeshwa zote kwa sasa na salio ni shilingi 1,000,086,941.80/= na taarifa zote hizi tayari tumeshaziwakilisha kwa Mdhibiti Mkuu wa Mahesabu pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu usuluhishi wa fedha za maduhuli shilingi 689,044,355/= suala hili linashughulikia kiufundi katika mtandao wa malipo ya Serikali (*IFMS*). Ni tatizo la kiufundi; hili linahusishwa na shilingi 169,309,325/= zinazotakiwa kusuruuhishwa kwenye mtandao na tukilimaliza hili tutalirekebisha pia. Lakini pia kuna suala la Ubalozi wa Malaysia limesemwa na Waheshimiwa Wabunge kadhaa na swali liloulizwa na ndugu yangu Mheshimiwa James Lembeli na baadae Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, liliulizwa kwamba kuna pesa zilizotumwa kule Ubalozi Malaysia za utalii na je, tuna uhakika zimetumika vizuri? Napenda kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba hadi kufikia Juni, 2008 kabla ya mwaka wa fedha kumalizika Balozi zetu zote zilipelekewa mishahara ya wafanyakazi wake, lakini ni kweli kwamba hadi kufikia Juni kati ya Aprili na Juni mwaka 2008 hatukuwa tumepeleka pesa za matumizi mengine (*OC*) na hizo ni kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Kwa upande wa Malaysia Wizara ya Maliasili na Utalii ilitoa katika kila Balozi kati ya dola 20,000 na dola 10,000 za kusaidia kutangaza utalii. Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba Malaysia walipelekewa dola 10,000 hatuna taarifa na mimi kama Waziri sina taarifa yoyote mbadala inayoeleza matumizi tofauti na yale yaliyokusudiwa. Ningependa tupewe muda tucheki kama pesa hizo zilitumika vinginevyo, lakini Ofisi yangu haina taarifa ya matumizi kinyume na matumizi yaliyokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo suala la matatizo ya Afrika, Serikali ya Umoja wa Afrika tumeshawaeleza kwamba Serikali ile itakuwa ni Serikali ya *Sovereign Independent States*. Ni Serikali zile zitakazounda Umoja huo wa Afrika na itakapoundwa na itakapokaribia mchakato huo Mabunge yote husika na huu ndiyo ubishi mmoja tulionao wale wanaotaka Afrika iundwe leo. Ubishi wetu mkubwa mmoja ni kuwaambia wenzetu ambao wao wenyewe wana-*dictate* katika nchi zao, kuwaambia wenzetu ambao wao ndiyo Bunge, wao ndiyo Serikali na wao wenyewe ndiyo Mahakama. Tunawaeleza kwamba sisi wengine tunatoka kwenye nchi zeny demokrasia na uamuzi wa mwisho lazima utoke kwenye Bunge. Hatuwezi kupitisha uamuzi wa uundaji wa Serikali leo kwa kuliruka Bunge kama la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati muafaka utakapofika wa kuunda Serikali ya Umoja wa Afrika, Bunge litaelezwa sababu na tutajaribu kujenga hoja na mkikubali tutakwenda kuunda Serikali ya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hivi tunachokusudia kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni uundaji na ukamilishaji wa Ofisi za Kanda. Kanda zetu lazima ziimarike kwanza katika miundombinu itakayowaleta pamoja wananchi wa nchi hizi mbili kufanya *interaction* lakini pia itakayowezesha bidhaa katika nchi hizi kuja pamoja. Hatuwezi kuunda Serikali ya Afrika iwapo bado wananchi wetu, sio viongozi wetu; wananchi wetu hawawezi kuwasiliana kati ya wao kwa wao au nchi na nchi au bidhaa zao kwenda na kutembea katika Bara la Afrika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, shabaha moja ya kuimarisha Kanda kama vile Afrika Mashariki na *SADC* nia yetu ni kuliwezesha hilo kwanza kabla ya kutunga au kabla ya kuingia kwenye mchakato wa uundaji wa Serikali moja ya Afrika. Tarehe 30 Januari, 2009 tutakapokuwa tunakabidhi kofia ya Uenyekiti wa Afrika, Addis Ababa kutakuwa na mjadala maalum wa uundaji wa Serikali ya Umoja wa Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Palestina limeulizwa kwamba ule moto na nadhani alikuwa ni Mheshimiwa Paul Kimiti kwamba ule moto wa Palestina vipi mbona hatuuoni? Tangu miaka ya 1960 tulipopata Uhuru Tanzania ina uhusiano mzuri sana na mamlaka ya Palestina. Miaka yote ya 1960 - 1970 hadi leo tunaendelea kudumisha udugu ule. Sisi kinachotusikitisha ni mambo mawili tu.

La kwanza Palestina wenyewe wamegawanyika, kuna *Hamas* lakini pia kuna *Fatah*. Sasa ule mgawanyiko ulioko ndani ya chama chenyewe cha Wapalestina kinatufanya wakati mwingine tushikwe na butwaa ya tufanye nini katika kuwaunga mkono. Lakini la pili linalotusikitisha ni kwamba Palestina wapo kule karibu na Waarabu na wapo kwenye *Magrib countries* na kwa kweli wapo kwenye *Arab League*. Lakini nchi zenyewe za Uarabuni ambazo zilitakiwa ziwe kwenye *front line* kama tunavyofanya sisi Afrika kwa nchi ambazo zina matatizo zenyewe nchi za Kiarabu nazo zimegawanyika kuhusu Palestina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ndiyo tunawauliza wenzetu wa Palestina mnategema pipi Afrika iwe kwenye mstari wa mbele iwapo ninyi wenyewe mmegawanyika ndani, lakini pia kwenye *Arab League* hamjapata *full support* na wenyewe pia wamegawanyika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumewaambia na tumewapa changamoto Palestina tengenezeni nyumba yenu kwanza baadae misaada ya Afrika itakuja wala hatuna matatizo ya kuwa pamoja na wenzetu wa Palestina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mauritania ambalo aliuliza Mheshimiwa Kabwe Zitto, ni kweli wiki tatu zilizopita Mauritania walipinduana. Tatizo lilitotukuta ni kwamba Serikali iliyopinduliwa Mauritania ni Serikali iliyochaguliwa, *a truly democratic government* na kitendo cha nchi na hii ni *AU Charter* inasema; “Iwapo nchi ya Afrika au Serikali ya Afrika iliyochaguliwa inapinduliwa, hiyo Serikali iliyopindua imejitoa moja kwa moja kwenye Umoja wa Afrika.” (*Makofi*)

Kwa hiyo, nilipokuwa Tehran nimeambia Serikali ya Mauritania usoni ilipofika pale kwamba hatuwatambui kama ninyi mpo katika Umoja wa Afrika na muondoke mkafanye *rein statement* ya Serikali iliyopinduliwa ambayo ilichaguliwa na wananchi. Mkakae huko halafu baadae tutakuja kuwaarifu mje kwenye Umoja wa Afrika. Serikali ya Mauritania ya Kijeshi ya sasa hivi haitambuliwi ingawa imetuambia kwamba wanataka kufanya uchaguzi tukawaambia uchaguzi kama ile mliyoichagua nayo ilichaguliwa. Mkyamalize mezani na mrudisheni Rais aliyepinduliwa, malizeni matatizo yenu halafu mrudi kwenye *AU*. Ndiyo msimamo wa Tanzania, ndiyo msimamo wa *AU* na ndiyo uongozi unaotakiwa katika Afrika kutokuwaonea haya watu wanaopinduana sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Chuo cha Diplomasia. Chuo hiki ni Muungano wa Tanzania na Msumbiji. Taarifa tulizonazo na kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu ni kwamba wenzetu wa Msumbiji wameunda chuo chao kingine cha diplomasia na kwa hiyo ushiriki wa Serikali ya Msumbiji kwenye Chuo chetu cha Diplomasia ni mdogo sana na ushiriki huu unakuwa mdogo hasa katika mchangano unaotakiwa kwa sababu makubaliano ni kwamba kuwe na asilimia 50 kwa pande mbili kuchangia maendeleo na uendeshaji wa chuo chetu hiki. (*Makofi*)

Katika miaka ya hivi karibuni tangu wajenge chuo chao chuo chetu kinajitegemea chenyewe kwa kushirikiana na Wizara yetu. Lakini hilo lisitupe shida. Sasa hivi Mkuu

wa Chuo pamoja na Wizara tunatafuta nchi ambazo zitaleta wanafunzi pale kama nilivyoleza jana lakini pia Wizara zote za nchi yetu ambazo kwa namna moja au nyingine zinahusiana na masuala ya diplomasia ya uchumi, zinazopokea wageni wengi wa nchi, Wizara hizo tutazitaka sasa kwa ulazima zipeleke maafisa wake kwenye chuo hiki cha Diplomasia ili tusiangushane. Kusiwe na Wizara moja tu yenye wataalam wa diplomasia wakati Wizara nyingine ambazo pia zinashiriki katika masuala ya diplomasia hawapeleki wanafunzi wao. Kwa hiyo, nalo hilo tutalifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la utoaji viza na usumbufu unaopatikana katika hili, Mheshimiwa Ramadhani Maneno na baadhi ya Wabunge wengine, ni kweli tumepokea malalamiko kwamba baadhi ya Balozi zinasumbua sana wananchi wetu katika upataji wa viza. Tumewaandikia baadhi ya Balozi hizo ikiwemo Canada, Uingereza na Marekani kujaribu kuliangalia hilo. Taarifa zisizo rasmi ambazo nimezipenda sana zinatoka Marekani kwamba sasa hivi Wamarekani wako kwenye mchakato wa kuwapatia Watanzania viza sasa ya miaka sita kwa mpigo. Hilo likitekelezwa tutakuwa tumevuka kipengele kimoja cha matatizo ya viza kwamba ukipata leo mpaka baada ya miaka sita ndiyo urudi ukaombe. Tunaliendeleza hili na ziara ya Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambayo anaifanya wiki ijayo nchini Marekani moja ya ajenda tunayoichukua ni kwenda kukamilisha hili ambapo Balozi wa Marekani ameshatutonya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Balozi nyingine ambazo zina malalamiko tumeziandikia na kuwaomba wenzetu pia wawashughulikie Watanzania wenzetu. Lakini napenda pia kutahadharisha baadhi ya Watanzania ambao wanatumia vibaya nafasi hizi za kuomba viza kwenda nchi za nje kwa kutoa taarifa za maandishi ambazo hazina ukweli wowote. Naomba kuwatahadharisha Watanzania tuwe wa kweli tunapokwenda kwenye Ofisi zetu za viza. Moja ya sababu inayofanya Watanzania wasumbuliwe wakati mwingine ni kutokuwa na takwimu sahihi au taarifa sahihi za safari unayotarajia kuifanya. Tuwe wa kweli na pale unapokuwa mkweli na unakataliwa nje kwenye Wizara yetu tutaona namna ya kukusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo suala la *economic diplomacy*. Nchi yetu inatangazaje utalii, uwekezaji na biashara duaniani na hapa napenda kuunganisha mambo matatu, la kwanza ni kweli kabisa kwamba mkakati wetu wa diplomasia ya kiuchumi unakwenda vizuri kwa maana ya kuwapata wawekezaji wengi, kuwapata wafanyabiashara wengi kutoka duniani na kuwaleta watalii nchini.

Napenda hapa hapa kujibu swalii la Mheshimiwa James Lembeli, kwamba je, shilingi milioni 600 ambazo zilitolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwenda London zimetumikaje, zimeingia kwenye akaunti gani? Napenda nikiri kwamba kwanza kauli ya kutoa shilingi milioni 600 za utalii London zilitolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Wizara yangu itawasiliana na Wizara ya Maliasili na Utalii kupata undani wa kauli ile, kupata undani wa matumizi ya pesa hizo na kupata undani wa namna inavyokwenda. (*Makofi*)

Lakini nilitonywa wiki iliyopita na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii alipokuwa amerejea kutoka London akinieleza jinsi mabango yalivyourekwa kwenye

mabasi maalum pale London kutangaza utalii wa Tanzania na hili hata maafisa wetu wa Ubalozi waliyaona. Lakini ni kiasi gani kimetumika na mpango unaendeleaje tutawasiliana na Wizara na tutatoa majibu baadae kama nilivyoahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo suala la matumizi ya *VIP* kwamba kwa kweli tulionayo ile sio *VIP*. Lakini nasema hivi hata kama ingekuwa *VIP* yapo matatizo tunajipalia wenyewe na hili tutalirekebisha, kwamba Membe ni *VIP* basi jamaa wote wa Membe ni ma-*VIP*? Tunakuza idadi sisi wenyewe tulipata nafasi hii ya kuingia mle kama *VIP's*, tunaleta ukoo mzima na ndiyo maana tunabakia tumesimama hata Waziri anaposafiri pale wakati mwingine anakuta watu amba kwa kweli hawafanani kabisa na hadhi ya kuingia kwenye chumba kile cha *VIP*. (*Makofi*)

Naomba ndugu zangu viongozi wote wenyе hadhi ya kutumia *VIP* kote nchini kuanzia Dar es Salaam tuzingatie miiko ile, tusifikishane mahala pa kupeana kadi maalum za kuingilia kwenye *VIP* tuaminiane. Wale wanaostahili kuingia waingine na wale ndugu zetu na koo zetu zingine ziende upande ule wa pili. Lakini nashukuru kwa ushauri huu nitaona namna ya kufanya ili kukaza kamba watu wasiostahili wasiingie kwenye vyumba hivi vya *VIP*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Watanzania waishio ughaibuni. Hawa Balozi zetu zingine zinasemwa zinawanyanya na hatuwathamini. Napenda nieleze kama ifuatavyo kwamba Tanzania sasa huu ni mwaka wa tatu tumeazimia kuwaheshimu na kuwaenzi na kuwashirikisha katika maendeleo ya nchi yetu Watanzania wanaoishi ughaibuni yaani *the diaspora* na tayari tumeshaona dalili London ambako Mheshimiwa Makamu wa Rais alivyokwenda kama nilivyoeleza kwenye kitabu kuzungumza na *diaspora* na mwezi wa kumi tutakuwa na Mkutano Afrika Kusini wa *diaspora* na kwenye AU yenyewe sasa hivi inasema badala ya kuwa na Kanda nane za Afrika zinazotengeneza Umoja wa Afrika tuwe na Kanda ya tisa ya *African Diaspora* yaani watu wenyе asili ya Afrika wanaoishi duniani wawe na Jimbo lao litakalotambuliwa na Umoja wa Afrika na hilo limepitishwa. Sasa kwa upande wa Tanzania tunataka tuige mifano ya baadhi ya nchi katika Afrika ambazo watu wake wanaoishi nje wanaingiza fedha katika nchi zao. (*Makofi*)

Lakini hawa wanahitaji kutambuliwa kwanza na ndiyo maana kuna suala la *dual nationality* kwamba tuweze kutekeleza na naliomba Watanzania walielewe tena vizuri tukiweza kupitisha pendekezo la kuwa na *dual nationality* hapo ndipo tutakapowenza kuwatumia kikamilifu Watanzania wenyе asili ya Tanzania waliopo ng'ambo na wanawenza kuchangia kikamilifu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Watanzania wanaoishi ng'ambo amba hawatambuliwa na nchi na amba wakifanya kosa la kuchukua uraia wa nchi nyingine anaondolewa uraia wake wa Tanzania hawezi kuwa mwana *diaspora* ambaye anaweza kulisiaidia Taifa kuleta maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunasema kwenye *dual nationality* na napenda Waheshimiwa Wabunge mlielewe tena suala la *dual nationality*. Kinachosemwa ni swali moja fupi na rahisi kulifahamu, je, inapotokea Mtanzania yeoyote kwa sababu yoyote ile akiwa ng'ambo anachukua uraia wa nchi nyingine aendelee kuadhibiwa kwa kuondolewa uraia wake wa kuzaliwa wa Kitanzania? Jibu lake likuwa hapana maana yake tuna *entertain*

dual nationality hakuna *definition* nyingine na jibu linatakiwa kuwa hivyo hapana; si vyema kumhukumu Mtanzania anayechukua uraia wa nchi nyingine na kumwondolea uraia wake hilo litachelewesha mkakati wa *diaspora*. Kumbukeni Watanzania kwamba katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita Watanzania sisi na Serikali yetu tumetoa uraia kwa watu wa nje nchini Tanzania 104.

Sasa kama sisi tunaweza kuwapa uraia watu wa nje kwa nini Mtanzania aadhibiwe kule nje anapochukua uraia kwa ajili ya afya yake, kwa ajili ya kupata elimu na kwa ajili ya kupata kazi kwa sababu ili upate mambo hayo matatu unahitaji kuwa raia wa kule. Kwa hiyo, lazima tubadilike na vita hii tunaichukua sisi Wizara ya Mambo ya Nje kupigania ili itakapofika Bungeni Waheshimiwa Wabunge mkubali tubadilike hakuna kibaya kitakachotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kauli ya kwamba inaweza kuwa ni jambo la kuhatarisha Usalama wa Taifa si kweli. Tumefanya utafiti katika nchi zingine zote kwa kweli ukiwa na *dual nationality* ndiyo wale jamaa hawakutumii kabisa. Taarifa zinaweza kutoka kwangu Membe hata kama nina *single nationality* kama watu wataamua kunitumia tu. Kwa hiyo, suala la kuhatarisha usalama halipo. Kwa hiyo, nasema suala hili limefika kwenye ngazi za juu za Serikali, tunalifanyia kazi na tunaomba litakapofika Bungeni tuliunge mkono ili Watanzania maelfu walioko nje ya nchi washiriki kuendeleza nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la *Organization of Islamic Conference (OIC)*. Mjadala huu ni mzuri lakini napenda niseme kwamba miaka karibu 17 iliyopita ni kweli kosa lilifanyika na kosa lililokuwa limefanyika wakati ule ni kwamba aliyekuwa mwenzangu Waziri wa Mambo ya Nje Mwenyezi Mungu amuweke mahala pema peponi Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria, binafsi alipeleka Azimio la kuitaka Zanzibar ijiunge *OIC* bila Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenyenye Mamlaka yaani *The Sovereign Instrument* kwenye Umoja wa Mataifa kuwa na taarifa. Hilo lilipotokea Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikataa pendekero lile na Umoja wa Mataifa ulikataa kutambua ombi lile.

Sasa ndiyo tukapewa kazi kwamba tulifanyie kazi kwa maana ya kuwashirikisha wananchi wa pande zote mbili ili tupime kama wapo tayari Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ijiunge na *OIC* na kwa maana hiyo Zanzibar iwe *member* wa *OIC*. Muda mrefu umepita naomba nikubali lakini mwaka huu tumefanya kikao cha kwanza na Baraza la Wawakilishi Zanzibar na ajenda hii imejitokeza na tuna mkutano wa pili tutakaokutana sisi Mambo ya Nje pamoja na Baraza la Wawakilishi Zanzibar kujadili suala la *OIC*. (*Makofi*)

Lakini kama ndugu yangu Mheshimiwa Manju Msambya alivyozungumza na sisi pia tumefanya utafiti kwa upande wa duniani tumegundua kwamba nchi 21 za Afrika ambazo zimejiunga na *OIC* zikuwepo nchi za Wakristu na zikiwepo nchi ambazo zina Mataifa yote kwa kweli hakuna athari yoyote ile inayoweza kupatikana kwa nchi kujiunga na *OIC*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama agizo lingekuwa kufanya tu utafiti nje ya nchi na kuamua ningetoa uamuzi hapa hapa, kwamba tumeshamshauri Mheshimiwa Rais, lakini kwa sababu linahusu wananchi sasa hivi tumeshakusanya takwimu za nje na tumeona hakuna athari, tunazungumza na Serikali ya Zanzibar kwenye kikao chetu cha pili na baada ya hapo tutaleta suala hili Serikalini pamoja na Bungeni ili sasa tuamue kwamba hakuna madhara yoyote kwa mujibu wetu sisi wa kuwa na *OIC* sasa bora tu tufuate utaratibu uliotakiwa kufuatwa na Jamhuri yetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, sasa suala la Balozi zetu, hili Wabunge wote mmezungumzia hali ya udhaifu, ukarabati na matatizo ya fedha kwenye Balozi zetu nashukuru sana. Lakini naomba niseme naishukuru sana Serikali yetu na namshukuru pia Katibu Mkuu Kiongozi wa Ofisi ya Rais na naishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwamba miaka yote ya nyuma Wizara yangu haikuwa inapokea Bajeti ya Maendeleo, lakini kwa mara ya kwanza tumepokea shilingi bilioni 10 na Bajeti hii ya Maendeleo itakuwa inaendelea. (*Makofit*)

Naomba sasa niseme kwamba kutokana na Wizara kupewa Bajeti ya Maendeleo tutajitahidi kutumia kwa kadri ya uwezo wetu fedha hizi kukarabati majengo yaliyoharibika na kujaribu kununua baadhi ya majengo na wakati huo huo kama tulivyosema tunabuni namna nyingine ya Wizara yetu kuingiza pesa hasa pesa za kigeni ili kuweza kusaidia kutatua kero zinazotukumba katika Balozi zetu na moja kati ya njia hizo kama zilivyosemwa ni kwamba tunanunua jengo *Washington DC*, tunanunua jengo New York na sasa hivi tupo katika mchakato wa kupata wafadhili ili waweze kutujengea pia Chuo cha Kimataifa Dar es Salaam. Yote haya yanalenga sio kwa mbwembwe tunalenga pia katika kukusanya pia fedha za kutosha ili *ku-complement* Bajeti hii ambayo mnatupitishia Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kuhudumia Balozi 32 tulizonazo lakini pili kuweza kuziongeza Balozi duniani kwa sababu kadri tutakavyokuwa na Balozi nyingi duniani ndivyo kadri nchi hii itakavyopata watalii zaidi, kupata wawekezaji zaidi jambo ambalo tunalihitaji. Kwa hiyo, tuombeane tu nadhani mambo yatakuwa mazuri nitakapokuwa natoa taarifa ya masuala haya kwenye taarifa yangu mwakani. (*Makofit*)

Sasa kuhusu suala la kubaini matapeli, hili ni jambo jema sana kwamba inawezekana kweli na si inawezekana imetokea na inatokea kwamba kuna watu wanakuja na *briefcase* akisingizia ni mwekezaji katika nchi hii. Anapofika na kwa vile ana rangi nyeupe au ya kizungu kuna dalili ya kumkubali haraka haraka kwamba inawezekana huyu ndiye. Sasa ombi limetolewa na ushauri tumeuzingatia. Tutatengeneza idara maalum katika Wizara yetu itakayoshirikisha wenzetu wa Wizara ya Fedha na Viwanda na Biashara zaidi na upande wa Utalii ili *desk lile lifanye kazi* kama alivyosema ndugu yangu kaka yangu Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko kwamba ni vyema tukawa na *desk* la makachero watakaokuwa wanapekua kulia na kushoto ndani na nje kama kweli hawa watu wanaokuja kuchumia Afrika ni kweli wanastahili kuja kufanya ubia na Watanzania au ni kampuni ya *briefcase*, kampuni ya mtu na mkewe tu kuja kuchumia Tanzania nadhani ni ushauri mzuri na tutauzingatia. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Sudan, Zimbabwe, nashukuru kwa michango yenu. Kwanza nataka tu kusema hivi kwamba kwa niaba ya Serikali tunalishukuru sana Bunge na

wananchi wa Tanzania kwa kuwa pamoja na Serikali katika misimamo yake kuhusu hali inavyoendelea Afrika. Kama mnavyopata habari na mlivyopata habari, mazungumzo sasa ya kupata ufumbuzi wa kudumu Zimbabwe bado yanalegalega. Sisi Tanzania tuko mstari wa mbele katika kuwasukuma wenzetu tukiwemo mle ndani na siyo kujiondoa, tukiwemo mle ndani kuhakikisha kwamba wenzetu wa Zimbabwe wanatatua matatizo yao ya kisiasa ili waweze kutatua matatizo yao ya kichumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Wazimbabwe hawali mikate kwa sababu bei ya mkate sasa ni bilioni 25 za Zimbabwe, hauwezi kubeba. Hakuna kinachoweza kununulika sasa dukani ukienda na makampuni yangali yanaondoka na *sanctions* zinaendelea. Tunaomba wenzetu wa Zimbabwe kufuata mfano wa Kenya kwa kuunda Serikali ambayo itajumuisha pande zote mbili. Lakini upo wasiwasi wa rafiki yangu alikuwa Mheshimiwa John Lwanji nadhani au Mheshimiwa Said Amour Arfi amba ni wasiwasi wa kweli kwamba tunakoelekea wapi Afrika iwapo chama kimoja kinashinda uchaguzi halafu chama kingine hakishindi, lakini huyu aliyeshindwa hataki kukubali kushindwa wala kushinda, badala yake tunasema waunde Serikali ya mseto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Tanzania tuliotoa Kenya na tunaendelea kuutoa Zimbabwe ni kwamba hii ni *transitional strategy*, ni mpango wa muda wa kupita, usiwe mpango wa kudumu kwa sababu hatari zake ndizo hizo. Huu uwe mpango wa muda na kwa hiyo, Kenya kwa mfano, hii *transition government* iliyoleta vyama vyote na kuunda Serikali ni mpango wa muda mfupi sana, utakapofika uchaguzi mwagine mkuu, tutataka mshindi aunde Serikali. Ni hivyo hivyo kwa Zimbabwe kwa sababu tukiliachia hili na anayeshinda kuambiwa hajashinda na anayeshindwa kusema ameshinda na baadaye kutengeneza mseto ni kweli tunaathiri demokrasia katika Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo suala la *diaspora*, hili suala la *diaspora* nilikosa kulisema kwamba pia Mheshimiwa Rais kwa kulipa uzito suala la *diaspora* ameagiza Wizara yangu ianzishe Idara Maalum ya kuzungumzia na kuwajua kwanza, Watanzania walioko kote duniani, halafu kuorodhesha vipaji walivyonavyo ili tuweze kuvitumia, lakini pia kuwashirikisha katika masuala kadhaa ya maendeleo nchini na kwa hiyo, Wizara yangu katika mwaka huu wa fedha na mwaka ujao tutaanza kuunda Idara Maalum ya Watanzania walioko Ughaibuni (*The Tanzanian Diaspora*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa nimalizie tu na suala la kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa hili suala la ziara la Mheshimiwa Rais. Mwaka jana nilisema na naomba niseme tena hapa, si viongozi wote wa Afrika, waliopo Afrika wanapata nafasi ya kutembea sana duniani, kwa nini, kwa sababu hawaalikwi na kwa nini hawaalikwi, kwa sababu wakati mwagine wale waalikaji hawaoni umuhimu wa kuwaalika. Rais wetu katika kipindi cha miaka miwili iliypita anaalikwa sana duniani siyo kwa sababu nyingine yoyote ile, anaalikwa sana duniani kwa sababu ya vipaji na uwezo wake wa kutatua migogoro na uwezo wake wa kuweza kujenga hoja zenye manufaa ya dunia, Afrika na Tanzania na ndio maana kunapokuwa na makongamano makubwa duniani, Rais huyu anaalikwa. Inapofika kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa AU wala hakugombania na mtu yejote, alipita bila kupingwa na haijawahi kutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba Watanzania wenzangu wote tukubali kwamba mzigo alioelemewa Rais Jakaya Mrisho Kikwete unatokana na *confidence* na imani kubwa ambayo dunia na Afrika wanayo kwake na mpaka hapo atakapoachia uongozi hatuna namna ya kufanya bali kumpa nguvu wote sisi aende kule, anapokwenda kujenga hoja hizi za Kimataifa anaheemea nchi yake na nchi yetu mabadiliko yake yataanza kuonekana siyo mara moja, lakini mbele ya safari yataanza kujionyesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa sana kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa hotuba yake nzuri sana ambayo vitabu vyake vitatoka na Mheshimiwa Spika na mimi naunga mkono hoja ya Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba hotuba ile sasa ikaliwe chini na Bunge lako Tukufu, kitabu chake kipatikane ili sasa tuende na miongozo ile na nina hakika na viongozi wenzangu tutasimama kidete kujenga *momentum* pale alipoachia Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete ili tuiongoze nchi hii bila kuwaruhusu watu kuivunja vunja wala kuipinda pinda au kupindisha matamko yaliyotolewa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Anafanya kazi nzuri, Serikali inafanya kazi nzuri na sisi kama Mawaziri tutafanya kazi kwa kujituma ili tutekeleze kwa kadri inavyowezekana Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja! Aah! Sasa... (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, kuna jambo unataka kulisema?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, nilidhani natakiwa kusoma kitu fulani, nashukuru ni mwisho utekelezaji! (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, naafiki! (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa Iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri wetu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambaye ndiye mtoa hoja. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na sasa tutaingia katika utaratibu wa Kanuni ya 100(1) ambayo nitaomba Katibu atusomee. Katibu! Tamka tu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kifungu 1001 – *Administration and General*.....Sh. 4,442,746,900/=

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Baada ya hotuba nzuri ya uhitimisho wa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, bila shaka

sina haja ya kwenda kwenye kifungu cha ngapi kwa sababu tuko wengi na tunaokoa muda bila shaka. Nina mawili madogo ambayo naomba ufanuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nimezungumza habari ya Kituo cha Kiswahili cha Addis Ababa ambacho Serikali yetu tulipewa Kiwanja tena kwenye *prime area* katika *Downtown* Addis Ababa na najua kwamba wenzetu wa *Foreign* walikuwa wanafuatilia jambo hili ili tujenge Kituo cha Kiswahili pale kama kuuza bidhaa ya Kiswahili pale Addis Ababa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilitembelea, Balozi Mangachi alinipelekea kutembelea Kituo hicho na kwa kweli likuwa ni jambo la faraja kweli kweli. Sasa najua Mheshimiwa Waziri hakupata fursa ya kusema lakini ninaomba ufanuzi kidogo tu kujua tu hatua gani zinafanyika na kama hatua hazijafanyika basi ni nini mkakati wa baadaye!

Mheshimiwa Mwenyekiti, na dogo la pili ni shughuli za *MONUC* pale Kigoma v/s Mashariki ya Kongo. Nimesema kwamba wenzetu wa *MONUC* wanatumia miundombinu na rasilimali za Mkoa wa Kigoma kuhudumia wenzetu wa *DRC* ambalo ni jambo jema kibinadamu. Swali langu ni dogo tu kwamba hawa wenzetu wa *MONUC* ambao chimbuko la *MONUC operations* katika *DRC* na kutumia *facilities* za Kigoma lilitoka *Foreign Affairs* wakati Mheshimiwa Rais akiwa Waziri wa *Foreign Service*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu Mheshimiwa Waziri au anifafulie sasa hivi au afuatilie ni kwa nini *MONUC* sasa kupitia *UN system* wasiweke lami Uwanja wa Ndege wa Kigoma wanaoutumia kwa ndege kubwa tena ndege za ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miundombinu ya Bandari ya Kigoma na barabara za kilometra nne, moja kutoka Ujiji kuja *Airport* na nyingine kutoka Mwanga kuja *Airport* na kwa kweli mchango wetu kama Taifa ni mkubwa, nilifikiri wenzetu hawa na wao wana *obligation* sasa ya ku-service miundombinu hii ili wote iwe ni *win win on humanitarian basis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufanuzi wa mambo mawili madogo hayo. Ahsante! (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kaka yangu Mheshimiwa Daniel Nsanzuganko kwa swali hilo. Ningependa kujibu kama ifuatavyo:-

Moja, kuhusu suala la *MONUC* ni kweli tutajaribu kuzungumza na Umoja wa Mataifa na mchakato huo tulishauanzisha, lakini tutafuatilia ili tuone *social responsibility* waliyonayo yaani kutoa huduma kwenye kiwanja pamoja na barabara za kilometra nne kama alivyozieleza, tutalipigania hilo na tutatoa taarifa baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kituo cha Kiswahili Addis Ababa, ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha mwaka wa fedha

uliopita Serikali kupitia Wizara yangu tumetoa dola 250,000 kwa ajili ya kuwezesha kituo hicho na mchakato huo sasa ungali unaendelea. (*Makofi*)

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza, naipongeza Wizara kwa juhudhi zake ilizofanya katika kufanya utafiti wa uwezekano wa nchi kuwa wanachama wa *OIC* na kwamba imethibitika kwamba hakuna madhara yoyote. Lakini sikufarijika sana baada ya Waziri kusema kwamba mchakato unaendelea ili Zanzibar iruhusiwe kuwa mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yangu ni kwamba nchi ya Tanzania itaingia kuwa mwachama badala ya ku-specify kwamba Zanzibar iwe mwachama. Natoa ushauri kwamba kama kunakuwa na uwezekano wa kuingia *OIC* basi tuingie kama Tanzania. Je, Waziri anaonaje wazo hilo? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ufanuzi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sikuelewaka tu vizuri, ni kwamba majadiliano yanatakiwa kushirikisha wananchi wa Tanzania, pande zote mbili inabidi zishirikishwe. Kwa hiyo, lengo hapa ni Tanzania kuingia *OIC* na siyo upande mmoja wa Muungano. Lakini tunachokifanya sasa hivi ni kujiridhisha tu na wenzetu wa Baraza la Wawakilishi kabla hatujaleta jambo hili humu ndani ili twende pamoja. (*Makofi*)

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nami nimponeze sana Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake wa kujibu hoja, lakini naomba tu kupata ufanuzi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1987 Tanzania kwa kushirikiana na Mozambique ilianzisha *Centre for Foreign Relations* na nafikiri au sina hakika sana, lakini nahisi Mheshimiwa Waziri alikuwa *member* wa bodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka leo hii *centre* hii haijasajiliwa. Sijui ni sababu zipi zinazopelekea *centre* hii isisajiliwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru! (*Makofi*)

MWENYEKITI: Inasajiliwa wapi? Inasajiliwa? Haya Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu kwa ufanuzi Mheshimiwa Rosemary Kirigini kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba *centre* hii ilipofunguliwa mwaka 1987 kile kiwanja na yale majengo sisi kama Tanzania kumbe tulikuwa tumeyatoa kwa Serikali ya Msambiji na kwa hiyo *registration* iliyopo kwenye viwanja vile na majengo yale yako kwenye hati ya Msambiji. Sasa baada ya Msambiji kuanzisha Chuo chake na kukosa sasa kuleta wanafunzi huku, sasa kuna suala la kisheria na tumepeleka kwa wanasheria ili

kuibadilisha ile hati ikiwezekana kwa sababu tunaweka *investment* yetu ili sasa iwe na usajili wetu badala ya kuwa na hati ya Msumbiji wakati wa Msumbiji hawatumii na sisi tunatumia, lakini hati ile si ya kwetu, inaweza kutuletea matatizo mbele ya safari. Mchakato huo wa kurekebisha hali hiyo unaendelea, ni mchakato mrefu, lakini utafikia hatma hivi karibuni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa jibu hilo na pia kwa swali lenyewe kumbe ni la msingi sana! (*Makofi*)

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika maswali yangu kwa maandishi, mojawapo nilikuwa lile linalohusu Ubalozi wetu India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimweleza Mheshimiwa Waziri jinsi ambavyo India inatumikia maeneo mengi na zaidi sana ambavyo Tanzania na India zimeingia katika makubaliano ya matibabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugeni unaokwenda India kwa ajili ya mahitaji ni mkubwa na mimi nilikuwa mmojawapo na nikaona jinsi gani kwa kweli wanajitahidi pale Ubalozini kutuhudumia. Zaidi ya hapo, unakuta kwamba siyo wote wanaokwenda pale kwenye ile hospitali ile ya Apollo ambayo iko New Delhi, wengine wanakwenda pia kwenye maeneo mengine ambapo kuna hospitali kama hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawa nimeomba tu Mheshimiwa Waziri anieleze kama inawezekana Ubalozi ule ukaangaliwa kwa jicho la huruma na kuongezewa Bajeti yake kwa sababu wakati naangalia Bajeti za nchi nyingine au za Balozi nyingine niliona ile iko katika hali ya chini tu inalingana labda na Ubalozi wa jirani zetu hapa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nilikuwa katika hali ya kuona kwamba hakuna ambavyo sasa hivi Watanzania wataacha kutibiwa India, siyo tu kwa ajili ya kupewa ruhusa au kupewa rufaa na hospitali zetu, hata wale ambao wanajiweza kidogo wanakwenda wenyewe. Lakini ukishafika pale, Ubalozi wenyewe unaanza kukuhangaikia toka siku ya kwanza na kukupitisha kwenye *platinum desk* na mengineyo mpaka kuhakikisha unaondoka nchi ile salama. Naomba ufanuzi. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu Mheshimiwa Shally Raymond kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Ubalozi wetu wa India unelemewa sana na wageni kutoka nyumbani wa viongozi na wananchi wengine wenyewe uwezo wa matibabu pale. Ukiilinganisha kasma tunayopewa na idadi ya wafanyakazi ni ndogo. Sasa hivi tunakusudia kufanya mambo mawili, la kwanza, kweli kuongeza Bajeti kidogo ili kuwawezesha watu wetu kufanya kazi, lakini la pili, tunajaribu sasa kuwasiliana na Wizara ya Afya ili wateue Daktari au Mganga Maalum awe *accredited* kwenye Ubalozi wetu aweze kushughulikia wimbi la wagonjwa ambao wanafurika kila mwezi nchini India. (*Makofi*)

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwanza, nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Bernard Membe jinsi anavyomudu hii Wizara. Swali langu dogo, mimi nilipokuwa Saudia nilipata malalamiko yanayosema kuna baadhi ya wawekezaji wanataka kuja Tanzania, wakifika kuomba viza, viza inaletwa huku, halafu inapelekwa Wizara ya Mambo ya Ndani, kisha inapelekwa katika *system* yetu ya usalama, majibu kuja inaweza kuchukua hata miaka miwili/mitatu, inawakatisha tamaa, wanakwenda kwingine. Hili suala nilimweleza Naibu Waziri, akasema atalifanyia kazi, je, naomba kujua bado inaendelea vivyo hivyo? Na kama inaendelea, kuna utaratibu gani ili tusipoteze *investors*? Ahsante!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu dada yangu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulikuwa na mtindo wa maudhi sana unaoitwa *Referred Visa System* kama alivyoieleza. Nasema ni mtindo wa maudhi sana kwa sababu hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu waliniambia tulishughulikie suala hili na Wizara ya Mambo ya Ndani. Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba tumeondolea mbali udhia huo kutoka Saudia, Iran na nchi zingine za Kiarabu. Sasa hivi wale wanaoomba viza wanakuja moja kwa moja Dar es Salaam na pale watapewa viza ili tuweze kuendelea badala ya kuwachelewesha chelewesha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa hatua hiyo, itasaidia sana mahusiano yetu lakini pia wageni wenye tija wanaokuja kwetu. (*Makofii*)

Waheshimia Wabunge, kwa kuwa sasa imebakia dakika kumi kufikia muda wa kuahirisha au kusitisha shughuli za Bunge, natumia mamlaka chini ya Kanuni ya 104(1) kuongeza kipindi kisichozidi dakika 30 ili shughuli za Wizara hii tuweze kuzikamilisha. Ahsante! Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge! (*Makofii*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza kabisa nimefarijika kama Mwenyekiti wa *Public Accounts Committee*, kuona kwamba Wizara hii sasa imepata *Development Budget* kwa sababu ilikuwa inatupa shida sana hata katika ukaguzi wetu wa mahesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nimemwomba Waziri ajaribu kutueleza ni uhusiano wetu na washiriki (*Development Partners*) ambao ni wengi, ni Ofisi za Balozi mbalimbali. Kwa sababu hata ukikumbuka hata Mheshimiwa Rais jana pamoja na kuweka mkazo ambao ulitufurahisha sisi Wabunge kwamba jambo la *CDF* Serikali imekubali, jambo ambalo linakuwa ni zuri sana. Lakini aliweka kaulakini, Mheshimiwa Rais kwamba tunazungumza na washirika wetu katika maendeleo ambao zaidi ni Mabalozi na karibuni pia Bunge lako Tukufu kupitia Kamati Ndogo limekuwa na mazungumzo na baadhi ya Maafisa wa Mabalozi kuhusu jambo hili na pametokea hata na

wakati ambao naona asasi zinazofadhiliwa na wafadhili zinafanya kongamano, zinapringa uamuvi wa Bunge, uamuvi ambao kama sasa hivi ni uamuvi wa Serikali juu ya jambo kama hili. (*Makofi*)

Sasa mtu unapata wasi wasi, upande mmoja tunapata misaada mizuri sana kutoka kwa wafadhili hawa wewe unaonekana kwamba kuna uhusiano mzuri kati ya ofisi yako na Tanzania na wafadhili hawa. Ni vipi basi watu hao hao wanataka kuingilia mpaka uamuvi wa Bunge, mpaka uamuvi wa Rais, wa Serikali? Ni mahusiano kweli ya kidiplomasia haya? Ningependa ufanuzi Mheshimiwa Waziri! (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana kwanza kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo kwa swali zuri ambalo wala nisingetegemea litoke upande ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu, ni aibu sana kwa asasi zetu au watu binafsi katika nchi hii kupingana na maamuvi ya Bunge au maamuvi ya Serikali hasa yanayohusu mazungumzo na mafanikio tunayoyafanya na *development partners* wetu, tunajiaibisha sana na kwa wakati mwininge tunawachanganya!

Mimi ningependa niungane mkono kabisa na Mheshimiwa Mbunge na nadhani na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba uamuvi wa kuwa na *CDF* ni uamuvi wa busara. Baadhi ya *development partners* ni kweli wameendelea kusita hadi leo kwamba pengine tukifanya hivi tutakuwa tunapendelea wakati mwininge pengine Chama Tawala tu kujipatia maendeleo. Lakini sisi tunacho sema hapa *emphasis* siyo Chama Tawala ni wananchi ndio wanaotakiwa kufaidika na *CDF*.

Kwa maana hiyo, jitihada zitaendelea kati ya Wizara yangu na Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Ofisi ya Rais kuhakikisha kwamba wale wachache ambao bado hawajatukubalia, wafanye hivyo na kuziomba taasisi na wenzetu nchini wanaopenda sana kuona sifa kupinga pinga kila kinachotakiwa na Serikali, waache kufanya hivyo, haya ni kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, safi sana! (*Makofi*)

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake wa kujibu maswali vizuri. Mimi nataka ufanuzi mdogo tu sana, suala la *OIC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri aliyo yaeleza, suala hili lina kipindi kirefu, limeshapita Mawaziri Wakuu wengi sana tangu aliyeanzia Mheshimiwa John Malecela, akaja Mheshimiwa Cleopa Msuya, akaja Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mheshimiwa Edward Lowassa na sasa yuko Mheshimiwa Mizengo Pinda. Nataka kujua tu, naye atamaliza muda wake bila kupata ufanuzi katika suala hili? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Limekwishajibiwa! Kwa mujibu wa Kanuni hatuwezi kuendelea kuuliza hilo hilo wakati majibu yamekwishatolewa! Itakuwa ni kuchukua

muda wa Bunge kwa sababu sidhani kama Waziri anaweza kuwa na maelezo yaliyotofauti. (*Makofi*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Nafurahi kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri. Jana wakati nahitimisha mchango wangu sikutamka kuunga mkono hoja, sasa naunga mkono hoja. Lakini napenda kupata ufanuzi kidogo tu kwa masuala mawili; moja ni hii *approach* ya *African Unity*, kuunganisha hizi nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nkrumah alipendelea *approach* ya kisiasa, Mwalimu akapendelea *approach* hii ya *Regional Integration*. Lakini vyote vinaonekana vinasua sua na tuna viongozi ambao ni vikwazo kwa sababu ya uchu wa madaraka na mambo mengine. Sasa sijui wanaweza ku-adopt *approach* ya George Washington ya *military approach* ili kuwabana hawa watu kuweza kuungana haraka? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine katika kitabu hiki kuna maneno yanayotumika wanasema *High Commission* pamoja na *Embassy*. Sasa ninavyofahamu mimi Balozi zetu zinazoitwa *High Commission* ni kwa nchi hizi ambazo zilikuwa chini ya himaya ya Uingereza kwa maana sasa zikaungana zikawa kwenye *Commonwealth*, tunasema *High Commission*. Lakini naona nchi tatu hapa ambazo zilikuwa katika himaya ya Uingereza tunatumia neno *Embassy*, *Embassy of Lilongwe*, *Embassy of Nairobi*, *Embassy of Kampala*. Ni kwa nini? Naomba ufanuzi! (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu maswali madogo ya kaka yangu Mheshimiwa John Lwanji kama ifuatavyo:-

La kwanza, kuhusu suala *African Union*, hii *approach* ya George Washington hatuikubali. *Approach* ambayo inategemea kushinda hapa ni ya *Nyerere Doctrine* kwamba Serikali ya Umoja wa Afrika lazima ianzie kwanza na kuimarisha *Regional Economic Group* kama *East Africa*, *SADC*, *IGAD*, *ECOWAS* na vitu kama vile na ndiyo vita tuliyonayo. Lakini napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba *Doctrine* ya Nyerere katika uundaji wa Afrika sasa hivi ina wajumbe zaidi ya theluthi mbili za Afrika na nadhani ndiyo ita-*prevail*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu *High Commission* na *Embassy* ni kweli kwamba *High Commission* ni *identity* ambayo Waingereza wameitoa kuashiria nchi zile ambazo wao wenye walikuwa koloni na zina Ubalozi pia kwenye nchi za *Commonwealth*. Kwa hiyo, Tanzania sisi ni koloni la Uingereza, tunapokwenda Afrika ya Kusini, utakuta pale imeandikwa *Embassy of Tanzania*. Lakini tunapokwenda Kenya ni *High Commission of Tanzania*. Sasa Malawi ilikuwa koloni la Waingereza pia na kwa hiyo, tunetakiwa kutumia *High Commission*, *High Commission*.

Tutafanya *checking* ya hiyo kuona kama kwa jazba tu za kidiplomasia tulikiuka maneno hayo. Lakini ni kweli kama ulivyosema, *High Commission* inatumika tu kwa nchi zile ambazo zilikuwa koloni la Waingereza na zina-*operate* kwenye koloni la

Waingereza na *Embassy* zinatumika kwa nchi zozote zila ambazo ziko kwenye nchi ambazo si koloni la Waingereza. Tutafanya marekebisho kama limejitokeza hilo. (*Makofi*)

MHE. FELIX C. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi pia nijiunge na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyojibu maswali vizuri sana, swali langu ni dogo tu na nafikiri ni kwa sababu ya ufinyu wa muda hakuweza kueleza hoja zile nilizozitoa katika Bunge lililopita na pia katika mchango wangu jana, nalo ni juu ya wapangaji wa nyumba za *AICC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yangu nilijaribu kuleta malalamiko ya hawa wapangaji wakisema kwamba pango la nyumba za *AICC* zimepandishwa kwa kiwango kikubwa mno kwa asilimia zaidi ya 55 mpaka 150, nilikuwa naomba Wizara iingilie kati katika kuliangalia tatizo hili ili haki ioneckane inatendeka kwa hawa wapangaji na wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu ambalo limepeewa kupitia kwa Mheshimiwa Naibu Waziri walisema kwamba siyo kweli kwamba kodi za nyumba zilipandishwa kwa kiwango hicho sasa mimi hiyo inanisumbua kwa sababu sipendi kushiriki katika kuleta maneno ambayo hayana msingi katika Bunge hili, nilipouliwa wapangaji wa hizi nyumba za *AICC* wamenihakikishia kwamba kodi kweli zimepandishwa kwa asilimia 50 mpaka 150.

Mheshimiwa Mwenyekiit, sasa napenda Wizara iangalie hilo, nani anayesema kweli hapa wapangaji wangu au huo uongozi wa *AICC* waliokuletea hiyo taarifa na kama mmojawao anasema uwongo mimi nielezwe kama ni wa kwangu niende nikawashughulikie watu wangu na kama ni watu watendaji wako Mheshimiwa Waziri washughulikie watu wako lakini kubwa zaidi ni kodi hizi ziangaliwe tena kupandishwa kodi za mkupuo mmoja kwa kiwango hiki siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi nyumba zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya wafanyakazi wa ngazi za chini, wanyonge hali zao ni ngumu sana katika miji yetu, naomba tusiendelee kuwabebesha mizigo ambayo kusema kweli inaweza ikashughulikiwa kwa njia nyingine ambayo ni nzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa mimi napenda kuamini *core business* ya *AICC* ijikite kwenye *conference tourism* kujaribu kupata mapato kwenye njia hizi za kuwafuata hawa wanyonge na hizi nyumba ndogo siyo njia endelevu ya kuisaidia *AICC* kujiendeleza ijiondoe huko, naomba ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Felix Mrema kwa maswali yake hayo, lakini ningependa kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema kubwa hapa si suala la nani kadanganya, siwezi kwa sasa hivi kujibu swali la nani amedanganya nadhani kubwa hapa

sasa ni kupata utatuzi wa matatizo yanayowakabili wapangaji wako na ningependa kuwaambia kama wanansikia wapangaji wa Arusha Mbunge wenu anafanya kazi nzuri sana ya kuwasemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba siku ya tarehe 5 Septemba, 2008 nitakapokuwa Arusha kikazi nitakutana na bodi ya *AICC* ili kuzungumza kero hizi na ningemwomba Mheshimiwa Mbunge awepo Arusha wakati huo ili baada ya mazungumzo yangu na bodi ya *AICC* niweze kumpa majibu muafaka na ninakutakia kila la kheri kwenye uchaguzi wa mwaka 2010. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Sh.414,930,300/=
Kifungu 1003 - <i>Foreign Affairsa Office Zanzibar</i>	Sh.164,756,700/=
Kifungu 1004 - <i>Policy and Planning</i>	Sh.532,077,300/=
Kifungu 1005 - <i>International Co-operation</i>	Sh. 766,085,200/=
Kifungu 1006 - <i>Europe and America</i>	Sh.176,140,400/=
Kifungu 1007- <i>Asia and Australia</i>	Sh.145,292,500/=
Kifungu 1008 - <i>Africa and Middle East</i>	Sh.3,390, 894,400/=
Kifungu 1009- <i>Regional Cooperation</i>	Sh.2044,254, 600/=
Kifungu 1010- <i>Protocol</i>	Sh. 7,152,336,700/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1011 - <i>Legal Services</i>	Sh.2.105,841,400/=
Kifungu 1012 - <i>Information, Education and Communication</i>	Sh. 95,305,000/=
Kifungu 1013 - <i>Middle East Division</i>	Sh.178, 686,000/=
Kifungu 2001- <i>Embassy of Tanzania -Addis Ababa</i> ..	Sh. 826,766,100/=
Kifungu 2002- <i>Embassy of Tanzania -Berlin</i>	Sh.1,494,193,800/=
Kifungu 2003 - <i>Embassy of Tanzania-Cairo</i>	Sh.612,323,000/=
Kifungu 2004 - <i>Embassy of Tanzania Kinshasa</i>	Sh. 779,603,300/=
Kifungu 2005 - <i>High Commission of Tanzania - Abuja</i>	Sh.809,817,000/=
Kifungu 2006- <i>High Commission of Tanzania - London</i>	Sh.1,567,901,300/=
Kifungu 2007 - <i>High Comission of Tanzania-Lusaka</i>	Sh.925,967,900/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2008 - <i>Embassy of Tanzania -Maputo</i>	Sh. 937,778,200/=
Kifungu 2009 - <i>Embassy of Tanzania -Moscow</i>	Sh.1,148,227,800/=

Kifungu 2010 - *High Commission
of Tanzania-New Delhi*.....Sh.1,523,672,700/=

Kifungu 2011 - *Permanent mission
to the UN-New York*.....Sh.2,896,236,200/=

Kifungu 2012 - *High Commission
of Tanzania - Ottawa*.....Sh.1,218,605,700/=

Kifungu 2013 - *Embassy of Tanzania -Paris*.....Sh.1739334,00/=

Kifungu 2014 - *Embassy of Tanzania Beijing*.....Sh.113,148600/=

Kifungu 2015 - *Embassy of Tanzania -Rome*.....Sh.1438,790,400/=

Kifungu 2016 *Embassy of Tanzania-Stockholm*....Sh. 1,179,227,800/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko
yoyote*)

Kifungu 2017 - *Embassy of Tanzania-Tokyo*Sh. 1,285719,100/=

Kifungu 2018 - *Embassy of Tanzania Washington*....Sh. 1892101400/=

Kifungu 2019 - *Embassy of Tanzania Brussels*.....Sh. 1,473,131,400/=

Kifungu 2020 - *Permanent Mission
to the UN-Geneva*.....Sh. 1731,668,300/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko
yoyote*)

Kifungu 2021 - *Embassy of Tanzania -Kampala*.....Sh.736,813,100/=

Kifungu 2022 - *High Commission
of Tanzania-Harare*.....Sh.753,735,400/=

Kifungu 2023- *Embassy of Tanzania -Nairobi*Sh.1474,597,600/=

Kifungu 2024 - *Embassy of Tanzania - Riyadh*Sh.819,932,000/=

Kifungu 2025 - *Embassy of Tanzania -Pretoria*.....Sh. 948,607,300/=

Kifungu 2026 - *Embassy of Tanzania -Kigali*.....Sh.597,599,300/=

Kifungu 2027 - *Embassy of Tanzania- Abu-dhabi*...Sh.1,221,784,900/=

Kifungu 2028 - *Embassy of Tanzania-Bujumbura*....Sh.752,897,600/=

Kifungu 2029 - *Embassy of Tanzania-Muscat*.....Sh.717,087,400/=

Kifungu 2030 - *Embassy of Tanzania- Lilongwe*.....Sh.718186,600/=

Kifungu 2031 - *Tanzania High
Commission-Kual Lumpur*.....Sh.133137,600/=

Kifungu 2032-*Embassy of Tanzania- Brasilia*Sh.1,027,105,500/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko
yoyote*)

MATUMIZI YA MAENDELEO

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kifungu 1004 - *Policy and Planning*.....Sh. 10,500,000,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko, hivyo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2008/2009 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kusitisha shughuli za Bunge napenda kutoa matangazo yafuatayo;

Kwanza niwakumbushe ile semina ya *TICTS* kuhusu shughuli za bandari, ingawa wengine watakuwa wameanza shughuli za ibada saa saba na nusu lakini semina inaendelea kwa hiyo, mijisikie huru semina inaanza saa saba na nusu mchana watakaoingia saa nane mchana na wataendelea nayo hadi saa tisa, wote mnakaribishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ameomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo ya Nishati na Madini kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati siku ya Jumapili tarehe 24 Agosti, 2008 saa sita mchana katika ukumbi namba 219. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wakati nikitambulisha wageni, wengine ambao hawakupata nafasi wameweza kuingia, nafurahi kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa Shally Raymond ambaye ni Bwana Philip Nguma, wengine ni wanafunzi na walimu wa shule ya Sekondari Kikunde kutoka Wilaya Kilindi ambao ni wageni wa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, naomba wasimame pamoja na walimu, karibuni sana na tunawapa pole kwa safari ndefu kutoka Kilindi, karibuni sana Dodoma na sijui imekuwaje, leo ni sikukuu ya kuzaliwa kwa Mbunge wenu Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, sasa sijui ni mpango mkakati au ni kitu gani, lakini karibuni sana mfurahi naye. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, bahati mbaya sana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo pamoja na kuwa amenipa taarifa ya *birthday* yake lakini hakunialika kokote kwa hiyo, nadhani lengo ni kwamba asherehekee na mumewe na hawa wapiga kura na wanafunzi kutoka Kilindi, nakutakia *birthday* njema na Mungu aendelee kukupa uhai ili uendelee kuwatumikia wananchi wa Kilindi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kile kikao chetu cha Kamati ya Uongozi na Tume, kwa sababu ya mgongano na vitu mbalimbali, imebidi kiahirishwe, Jumatatu pia Mawaziri watakuwa na kikao chao, sasa tutatangaza muda muafaka siku hiyo ya Jumatatu, kwa hiyo, leo hakipo tena tunashughulikia mambo mengine. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna tatizo la mahudhurio humu Bungeni, tulikuwa hatupendi kuwa bayana sana lakini mjue kwamba tunayo rekodi ya kila anayehudhuria kila siku sasa mtanilazimisha niweze katika siku maalumu niwe natangaza wale watoro kabisa, wale ambaeo wala hawajali kabisa au anakuja kipindi cha maswali basi na hawana kazi zingine za Bunge, kwa leo ninafurahi kutamka kwa upande wa Serikali kwamba Waziri wa *cabinet* anayehudhuria kwa nidhamu kubwa sana humu Bungeni ni Mheshimiwa Celina Kombani. Rekodi zetu za Katibu zinaonyesha hivyo na anayemfuata ni Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, hayupo tu yupo safarini kwa hiyo inaelekea hawa Mawaziri wanawake wanandidhamu sana hawa, tunaomba Mheshimiwa Rais anapotazama tazama tena aongeze idadi ya wanawake katika Baraza la Mawaziri. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(*Saa 07.20 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 – Wizara ya Fedha na Uchumi

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, iliyowasilishwa hapa Bungeni leo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likae kama Kamati, ili likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2008/09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Naahidi kuwa, nitaifanya

kazi yangu kama Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa uwezo na ujuzi wangu wote katika kutekeleza majukumu niliyopewa. Pia napenda kuwashukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ushirikiano na miongozo mbalimbali wanayonipa ambayo ni msaada mkubwa kwangu katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Bunge la Jumuiya ya Madola (CPA). Hii inadhihirisha uwezo wake na jinsi Tanzania inavyothaminiwa Kimataifa katika suala zima la utawala bora. Napenda pia kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Kilosa, kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao na ninaahidi kuwa nao bega kwa bega katika shughuli za kuleta maendeleo katika Jimbo langu. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru mke wangu Halda na familia yangu yote kwa uvumilivu wao kwa miezi miwili na nusu ambayo nimekuwepo hapa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu kwako wewe, kwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati za Bunge, kwa umakini wenu katika kuendesha majadiliano ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/09, tangu yalipoanza tarehe 16 Juni, 2008 hadi sasa. Aidha, ninashukuru kwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati zote za Kudumu za Bunge katika kuchambua mapendekezo ya bajeti za Wizara, Idara, Mikoa na Serikali za Mitaa. Natoa shukrani za pekee kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Jimbo la Handeni, kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyyoyatoa kwa Wizara kuhusu bajeti hii. Napenda kuwapongeza na kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, Wizara inathamini sana michango na ushauri wao na umezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, jamaa na familia ya Mbunge mwenzetu, aliyefariki dunia kwa ajali ya gari tarehe 28 Julai, 2008, Marehemu Chacha Zakayo Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Tarime. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majanga mengi ya ajali yameikumba nchi yetu, hususan ajali za magari na kusababisha vifo, majeraha na athari nyingine kwa wananchi na mali zao. Napenda kutoa pole kwa Viongozi na Wananchi wa Mikoa ya Mbeya, Singida, Tanga na maeneo mengine nchini, kwa vifo vilivyosababishwa na ajali za magari. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina. Aidha, nawatakia afya njema na kupona kwa haraka, wale wote walioumia kutokana na ajali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, n apenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kujadili hoja mbalimbali kwa kina na umahiri na kutoa mapendekezo yanayochangia katika kuboresha utendaji wa Serikali. Mafanikio yanayoonekana katika ukuaji wa uchumi, ongezeko la mapato ya Serikali, ongezeko la uwekezaji, udhibiti wa matumizi ya Serikali na kadhalika ni vielelezo vya matunda ya ushirikiano mzuri kati ya Serikali, Bunge na Kamati zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na mambo mengine, itaendelea kuzingatia ushauri uliotolewa na Bunge wakati wa kujadili bajeti Kuu ya Serikali katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuyapitia kwa kina maeneo mapya ya mapato yaliyopendekezwa ili kuainisha yale yanayoweza kutekelezwa, pia kupitia baadhi ya maeneo ambayo hayana tija katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa lengo la kuyaboresha zaidi.

(ii) Kupitia upya misamaha ya kodi kwa lengo la kuipunguza ili kuokoa mapato.

(iii) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha kwenye Halmashauri kwa kupitia upya Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, kwa lengo la kuainisha marekebisho yanayostahili.

(iv) Kutatua tatizo la idadi kubwa ya akaunti za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kwa kuziainisha na kuzipunguza.

(v) Kuendelea kufuutilia kwa karibu eneo la ununuzi na utunzaji wa vifaa na huduma ili kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Umma.

(vi) Kuimarisha menejimenti ya uchumi Kitaifa ili kuhakikisha kuwa mafanikio ya uchumi mkuu yanatiririka hadi vijijini, ili kupunguza umaskini wa kipato mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara ililenga kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 3,502.58. Kati ya hizo, mapato ya kodi yalikadirwa kufikia Shilingi bilioni 3,189.27 na mapato yasiyokuwa ya kodi, Shilingi bilioni 313.31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara ilkusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi yaliyofikia Shilingi bilioni 3,634.58. Jumla ya makusanyo hayo yalifikia asilimia 3.6 zaidi ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani, hasa ya kodi ni matokeo ya sera sahihi za uchumi, jitihada za kuboresha mfumo wa kodi na usimamizi imara wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Mafanikio haya ni ya kuridhisha hasa ikizingatiwa kwamba, Taifa linakabiliwa na matatizo ya kupanda kwa bei za vyakula, mafuta ya petroli, malighafi za viwanda na pembejeo za kilimo katika soko la dunia na hapa nchini.

Nachukua fursa hii kuipongeza tena Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipa kodi wote, kwa kutimiza wajibu wao kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada na mikopo kutoka nje kwa mwaka 2007/08 ilifikia Shilingi bilioni 1,980.42, sawa na asilimia 85 ya makadirio ya mwaka mzima. Kati ya fedha hizo, misaada na mikopo ya Bajeti (*General Budget Support – GBS*), kwa mwaka huo ilikuwa Shilingi bilioni 983.10, ambazo ni asilimia 12 zaidi ya makadirio ya

mwaka. Ongezeko hili limetokana na fedha za Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), zilizokadiriwa katika bajeti ya 2006/07, lakini zikachelewa na kupokelewa mwaka wa fedha 2007/08. Misaada na mikopo ya ki-sekta na programu maalum kwa mwaka 2007/08 ilikuwa Shilingi bilioni 416.87 sawa na asilimia 53 zaidi ya makisio. Ongezeko hili limetokana na fedha za mkopo wa Benki ya Dunia kwa sekta ya elimu, zilizotarajija kutolewa mwaka 2006/07, lakini zikaingia katika akaunti ya Serikali mwaka 2007/08, pamoja na nyongeza ya misaada kutoka kwa wahisani kadhaa kwenye mifuko mbalimbali. Kwa upande mwingine, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilifikia Shilingi bilioni 533.96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/08, Wizara iliendelea kuboresha ufanisi wa upatikanaji wa misaada ili iweze kuchangia kuleta maendeleo na kupunguza umaskini kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Wizara ilianda na kukamilisha Mpango wa Utekelezaji na Ufutiliaji wa Tathmini ya MPAMITA (*JAST Action Plan and Monitoring Framework*), ambao ni mfumo wa kitaifa wa muda wa kati wa kusimamia ushirikiano wa maendeleo baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ili kufikia malengo ya maendeleo na kupunguza umaskini.

(ii) Wizara pia ilianda na kuendesha semina elekezi kwa Wakurugenzi wa Sera na Mipango, kuhusu mpango wa utekelezaji wa MPAMITA na kuwahamasisha kuhusu mchakato wa utoaji misaada kupitia Bajeti ya Serikali (*GBS*).

(iii) Wizara ilianda Mkutano wa mwaka wa mapitio ya mfumo wa utoaji misaada kwa njia ya bajeti (*GBS Annual Review 2007*). Mkutano huo ultathmini utekelezaji wa makubaliano yaliyomo katika *Perfomance Assesment Framework (PAF)* ya 2007. Matokeo ya tathmini hiyo yaliwawezesha Washirika wa Maendeleo kupitia *GBS*, kuamua viwango vya misaada watakayota kwa mwaka wa fedha wa 2008/09.

(iv) Wizara ilikamilisha rasimu ya mfumo wa majadiliano (*New Dialogue Structure*), kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine. Mfumo huu utaisaidia Serikali kuimariswa mifumo ya majadiliano katika ngazi zote, ikiwa ni pamoja na kuiwianisha michakato ya Bajeti ya Taifa na MKUKUTA.

(v) Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Kusimamia Misaada ya Kiufundi (*National Technical Assistance Policy*) yanaendelea. Kamati ya pamoja yenyewe wajumbe kutoka Serikali na Washirika wa Maendeleo imeundwa kwa ajili ya kuratibu uandaaji wa Sera hiyo. Kwa upande wa Serikali, kamati hiyo inajumuisha wajumbe kutoka Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa za awali za hesabu za matumizi ya Serikali hadi tarehe 30 Juni, 2008, mwenendo wa matumizi katika Mafungu yote manne (Fungu 22, 23, 45 na 50), yaliyoombewa fedha na Wizara ulikuwa kama ifuatavyo: Mtumizi ya Kawaida jumla ya Shilingi bilioni 766.50, ikilinganishwa na Bajeti ya jumla ya Shilingi bilioni 814.10; na matumizi ya Maendeleo (kwa Fungu 23, 45, na 50) Shilingi bilioni 15.95, ikilinganishwa na bajeti ya Shilingi bilioni 41.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea kuweka kipaumbele katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mambo muhimu yatakayozingatiwa ni pamoja na kuendelea kupanua wigo wa kodi na kuimarisha zaidi usimamizi wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inalenga kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi bilioni 4,728.59 katika mwaka 2008/09. Hili ni ongezeko la asilimia 31 ikilinganishwa na mwaka 2007/08. Kati ya hizo, mapato ya kodi yanayolengwa kukusanywa ni Shilingi bilioni 4,497.07 na mapato yasiyo ya kodi Shilingi bilioni 231.52. Ili kufikia lengo hili, hatua kadhaa zitachukuliwa, ambazo ni pamoja na: -

(i) Kupanua wigo wa mapato ya Serikali kwa kusajili walipa kodi wapya, kuongeza mchango wa uvunaji wa maliasili katika mapato ya Serikali na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika sekta zote za uchumi;

(ii) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa ushuru na kodi katika forodha;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tatu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA Third Corporate Plan*), kwa nia ya kuongeza uwajibikaji mionganoni mwa walipa kodi, watoza kodi na kadhalika; na

(iv) Kurekebisha sera na sheria zinazotoa misamaha ya kodi kwa sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), ilipewa lengo la kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 3,189.27 (trilioni 3.18) mwaka 2007/08. Makusanyo halisi ya kodi yalifika Shilingi bilioni 3,359.28 (trilioni 3.35), ambazo ni zaidi ya lengo kwa asilimia tano. Mwezi Juni, 2008, *TRA* iliweza kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 346.69 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 281.46 zilizokusanywa mwezi Juni, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya yamepatikana kutokana na jitihada za Serikali za kuboresha mfumo wa kodi na taratibu za kukusanya mapato kwa kufanya marekebisho ya aina mbalimbali katika mfumo wa utozaji Ushuru wa Forodha, Kodi ya Mapato, Kodi ya Ongezeko la Thamani, Kodi ya Ushuru wa Bidhaa, Uimarishaji na Uboreshaji wa Idara ya Ushuru na Forodha na Idara ya walipa kodi wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwezi Julai, 2008, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tatu (*TRA Third Corporate Plan*) wa miaka mitano baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Pili wa Mamlaka hapo tarehe 30 Juni, 2008. Malengo na matarajio ya Mamlaka kwa mwaka 2008/09 ni kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 4,497.07, ikiwa ni asilimia 29 zaidi ya lengo la mwaka 2007/08. Ili kufikia lengo hili, Mamlaka itatumia mikakati mbalimbali ambayo ni pamoja na kuwepo kwa maboresho katika usimamiaji wa ukusanyaji kodi

kutoka kwenye vyanzo mbalimbali chini ya Mpango Mkakati wa Tatu wa Mamlaka (*TRA Third Corporate Plan*) wa miaka mitano. Hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa ni pamoja na:-

- (i) Usimamizi na utekelezaji wa mfumo wa kodi uliopo pamoja na marekebisho yaliyopendekezwa, ikiwemo kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya;
- (ii) Kuziba mianya ya ukwepaji kodi;
- (iii) Kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali;
- (iv) Kuendelea kutoa elimu ya biashara na namna ya ukokotoaji kodi kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usimamizi wa asasi za umma, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, iliendelea kusimamia utendaji katika sekta ya umma, kwa kuyataka mashirika na taasisi za umma kuwasilisha taarifa za kila robo mwaka (*Quarterly Reports*), pamoja na kutoa maelekezo ya mara kwa mara. Aidha, Wizara inakamilisha kuweka mfumo wa kumbukumbu za Mashirika (*Data Base*), unaotarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha. Vilevile Wataalam Waelekezi wanachambua sheria mbalimbali zinazohusiana na majukumu ya Msajili wa Hazina, kwa lengo la kupendekeza marekebisho ya sheria husika ili kuhimiza uwajibikaji na kuleta ufanisi zaidi katika sekta ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, itaendelea kushirikiana na Kamati za Bunge za Fedha na Uchumi, Hesabu za Mashirika ya Umma (*POC*) na zile za kisekta, kuhakikisha Sekta ya Mashirika na asasi za umma, inasimamiwa kwa ukaribu zaidi ili kuleta ufanisi katika uendeshaji na utoaji wa huduma kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kuboresha mazingira ya kuwezesha Benki za Biashara kutoa mikopo zaidi. Lengo ni kuwezesha mikopo katika sekta binafsi ikue kwa kiwango kisichopungua asilimia 39.5, ambacho ni sawa na ongezeko la Shilingi bilioni 893, ikilinganishwa na mwaka 2006/07. Hata hivyo, kufuatia ongezeko la shughuli za uzalishaji nchini, mahitaji ya mikopo ya sekta binafsi yalikuwa ya juu zaidi. Kufikia mwezi Juni, 2008, mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa imeongezeka kwa Shilingi bilioni 1,008.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la mikopo kwa mwaka 2007/08, lilichangija pia na kuongezeka kwa wakopaji waaminifu, ushindani baina ya mabenki ya biashara, kuimarika kwa mazingira ya biashara nchini na kupungua kwa riba za dhamana za Serikali. Mifuko ya Dhamana za Mikopo (*Credit Guarantee Schemes*) nayo iliongeza upatikanaji wa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wale wa kati. Aidha, katika kipindi hicho, benki kadhaa za biashara ziliingia katika makubaliano ya kutoa mikopo maalumu ya pamoja kwa wateja wakubwa (*syndicated loans*), ambayo

imechangia katika kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi. Vilevile, riba za mikopo kwa jumla zilipungua kufikia wastani wa asilimia 15.44 katika kipindi cha Julai, 2007 hadi Juni, 2008, kutoka asilimia 16.45 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita, wakati zile za mikopo kwa wateja wakubwa zilifikia wastani wa asilimia 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha mwaka 2007/08, kilitawaliwa na kupanda kwa bei za vyakula na bidhaa za mafuta ya petroli katika soko la dunia. Mahitaji ya fedha za kigeni yaliongezeka sana kukidhi uagizaji wa petroli na chakula. Hata hivyo, ongezeko la misaada na mikopo yenyenye masharti nafuu, uwekezaji kutoka nje, pamoja na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, vilisaidia kuzuia akiba ya fedha za nje isiporomoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa mikopo, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu, imeendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mageuzi ya Kuboresha Sekta ya Fedha nchini kwa kusimamia utekelezaji wake. Mafanikio yaliyopatikana hadi sasa ni pamoja na:-

(i) Muswada wa sheria ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa njia ya Ukodishaji Vifaa na Majengo uliwasilishwa, kujadiliwa na baadaye kupitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2008;

(ii) Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ambao pamoja na mambo mengine, unaipa Benki Kuu mamlaka ya kutoa miongozo ya uwekezaji kwenye mifuko hiyo, ulijadiliwa na kupitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2008;

(iii) Kuimarishwa kwa Benki ya Rasilimali (*TIB*), kwa kuiongezea mtaji ambapo Serikali imetenga Shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuiongezea mtaji. Uamuzi huu wa Serikali ni wa makusudi kwa kutambua tatizo kubwa la ukosefu wa mikopo ya uzalishaji katika viwanda na kilimo. Pia Serikali imeamua kuiongezea *TIB* Shilingi 25 bilioni kama mtaji maalum wa kusaidia mikopo ya kilimo;

(iv) Serikali kupitia Benki Kuu kuanzisha utaratibu wa kukusanya na kusambaza taarifa za wakopaji (*credit information sharing system*), ili kuwawezesha raia wema kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha kwa urahisi; na

(v) Serikali itaendelea kuiboresha mifuko ya kudhamini mikopo ya mabenki kwa kuiongezea fedha na pia kurahisisha taratibu na masharti ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera nzuri ya fedha, ili kuchangia katika juhudhi za kudhibiti mfumko wa bei. Katika kutekeleza hilo, itahakikisha kwamba, kiwango cha ujazi wa fedha ni sahihi na hakitazidi asilimia 18 kwa mwaka; ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiopungua Shilingi bilioni 732 sawa na ongezeko la asilimia 22 kwa mwaka; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007, Benki ya Rasilimali Tanzania imeendelea kuimarishwa kintaji ili kuweza kutoa mikopo ya maendeleo ya muda wa kati na mrefu. Mikopo kwa wateja iliongezeka kutoka Shilingi milioni 27,968 mwaka 2006 hadi Shilingi milioni 40,457 mwaka 2007. Aidha, amana za wateja nazo ziliongezeka kutoka Shilingi milioni 34,283 hadi Shilingi milioni 69,792 katika kipindi hicho. Kutokana na ufanisi huu, mali za Benki zimeongezeka kutoka Shilingi milioni 76,268 hadi Shilingi milioni 135,349 na kuweza kupata faida kabla ya kodi ya Shilingi milioni 63.83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, katika mwaka 2008/09, Benki hii itaongezewa mtaji wa Shilingi bilioni 21.0 ili kuhakikisha mtaji unafikia kiwango cha zaidi ya Shilingi bilioni 50.0 zilizoahidiwa na Serikali. Lengo ni kuiwezesha TIB kushiriki katika kutoa mikopo ya kiuchumi kwa wateja wake. Inatarajiwa kwamba, mikopo na amana za wateja itaendelea kukua ambapo mikopo itakua kwa asilimia 73 kutoka Shilingi milioni 40,457 hadi Shilingi milioni 70,000 na amana itakua kwa asilimia 12 kutoka Shilingi milioni 69,792 hadi Shilingi milioni 78,000. Lengo la Serikali ni kuiwezesha TIB iendelee kubaki kuwa chombo muhimu katika maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *National Microfinance Bank (NMB)*, imeendelea kuonyesha mafanikio mazuri ambapo, hadi kufikia Desemba 2007, mtaji wa benki hii ulifikia Shilingi bilioni 121.98 ukilinganisha na Shilingi bilioni 91.15 mwaka 2006, ikiwa ni ongezeko la asilimia 33. Katika mwaka 2007, amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia 47 hadi Shilingi bilioni 1,012.82. Aidha, mikopo yenyenye thamani ya Shilingi bilioni 345.21 ilitolewa mwaka 2007 ukilinganisha na Shilingi bilioni 137.46 iliyotolewa mwaka 2006. Kwa ufanisi huu, NMB iliweza kupata faida baada ya kodi ya Shilingi bilioni 38.83, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 35.06 iliyopatikana mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuboreka kwa ufanisi wa NMB iliyo na matawi 120, baada ya Serikali kuuza asilimia 49 ya hisa zake kwa Kundi la Wawekezaji (*Consortium*), wakiongozwa na *Rabobank* ya Uhlanzi, mwaka 2005 imefuzu kuandikishwa (*listed*) katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (*DSE*). Serikali inauza hisa asilimia 21 kwa Wananchi na itaendelea kubaki na asilimia 30 na hivyo kuwezesha sekta binafsi kumiliki asilimia 70 kutoka asilimia 49 za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya NMB katika mwaka 2008/09 ni pamoja na kuendelea kuboresha huduma zake ili kuweza kuongeza amana za wateja kwa asilimia 10 pamoja na utoaji wa mikopo kwa asilimia 42. Aidha, Benki hii inatarajia kuongeza matawi yaliyopo kutoka 120 hadi 150. Hatua hizi zitatokana na kuongeza kwa mtaji wa Benki hadi kufikia Shilingi bilioni 158.54 na rasilimali za Benki hadi kufikia Shilingi bilioni 1,193.20. Kufuatia ufanisi huo, *NMB* imepanga kuongeza mashine za kuchukulia fedha (*ATM*), kwenye matawi yote na sehemu nyininge nje ya matawi ili kuwafikishia wateja wake huduma nzuri ya kuchukua fedha karibu na makazi yao au sehemu zao za kazi, pamoja na kuanza kutoa huduma za kibenki kwa wateja kwa njia ya mtandao (*internet banking*), kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Benki ya Posta Tanzania (*TPB*) iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kukusanya amana za wateja zenyetamani ya Shilingi bilioni 73.06, ikililinganishwa na Shilingi bilioni 63.07 mwaka 2006/07. Idadi ya wateja iliongezeka kutoka 1,178,525 hadi 1,220,956 katika kipindi hicho. Aidha, mikopo iliongezeka kwa asilimia 51.3 kutoka Shilingi bilioni 23.05 katika mwaka 2006/07 hadi Shilingi bilioni 34.88 mwaka 2007/08. Kwa sasa, *TPB* inatoa mikopo ya biashara, ya watumishi, midogo midogo (*micro loans*), na mikopo ya uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya vitega uchumi vyataga Benki ya Posta Tanzania, viliongezeka kwa asilimia 16.9 kutoka Shilingi bilioni 60.24 mwaka 2006/07 hadi Shilingi bilioni 70.40 mwaka 2007/08, ambapo thamani ya mikopo ilifikia asilimia 50 ya vitega uchumi vyote. Juhudi hizi ziliweza kuingiza mapato ya Shilingi bilioni 15.75 katika mwaka 2007/08, ukililinganisha na mapato ya Shilingi bilioni 13.40 katika mwaka 2006/07. *TPB* ilipata faida ya Shilingi milioni 215, ikiwa ni pungufu ukililinganisha na faida ya Shilingi milioni 926 iliyopatikana mwaka 2006/07, pamoja na mambo mengine, kutokana na uamuvi wa kufuta deni la Shilingi bilioni 2.20 lililotokana na matumizi ya mfumo wa zamani wa kutoa mikopo na kusimamia amana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, benki hii imelenga kuongeza ukusanyaji wa amana za wateja kwa asilimia 20 kutoka Shilingi bilioni 73.56 mwaka uliopita hadi Shilingi bilioni 88.28. Mikopo inatarajiwa kukua kwa asilimia 30, sawa na Shilingi bilioni 45.35. *TPB* itaendelea kuboresha huduma ya kutuma na kupokea fedha kwa kutumia *Western Union Money transfer*, kwa kuongeza vituo zaidi kwa kushirikiana na Mabenki na Taasisi za fedha kama Wakala wake. Aidha, itaimarisha ushirikiano na Shirika la Posta la Tanzania katika kusambaza huduma za Benki kwa kuunganisha Matawi yake katika mtandao wa kompyuta wa Benki, ili kufanya huduma kuwa za haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Sheria ya *The National Bank of Commerce (Reorganisation and Vesting of Assets and Liabilities) Act, CAP 404* ya mwaka 2007, Bunge lako liliridhia na kuliongezea Shirika la *Consolidated Holding (CHC)*, muda wa uhai wake kwa miaka mitatu zaidi hadi tarehe 30 Juni, 2011. Hii ni pamoja na kuhamishia *CHC* majukumu ya kusimamia shughuli za ubinafsishaji zilizokuwa zinafanywa na iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*); kusimamia Mali na Madeni ya Mashirika yaliyomaliza muda wake ambayo ni *Loans and Advances Realization Trust (LART)*, *Air Tanzania Holding Company (ATHCO)* na Simu 2000 Ltd.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2007, Shirika lilipata mapato ya Shilingi milioni 8,188 kutokana na uuzaji wa majengo, ukusanyaji wa madeni, riba kutokana na amana, ufilisi wa Makampuni yaliyokuwa chini ya *PSRC* na *LART*, gawio kutoka *NBC Limited* na huduma mbalimbali. Aidha, katika kipindi hicho, *CHC* ilitumia kiasi cha Shilingi milioni 4,847 kama matumizi ya uendeshaji yanayoju muisha malipo ya fidia na madai kutokana na kesi inazoendesha na hivyo kuwa na ziada ya Shilingi milioni 3,341.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayolikabili Shirika hili ni usimamizi wa kesi 236 ambazo limerithi, pamoja na ukusanyaji wa madeni sugu. Shirika limeendelea kutumia njia za kawaida za kimahakama, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa usuluhishi chini ya Mahakama na majadiliano nje ya Mahakama. Aidha, ukusanyaji wa madeni sugu umeendelea kuwa mgumu kutokana na madeni haya kutokuwa na dhamana au dhamana zilizopo kuwa hafifu ukilinganisha na kiasi cha deni lenyewe. Vilevile wadaiwa wengine hukimbilia Mahakamani na kupata zuio (*court injunction*) na hivyo kufanya zoezi la ukusanyaji kuwa gumu zaidi pamoja na kuchukua muda mrefu kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008, Shirika limekadiria kukusanya mapato ya Shilingi milioni 4,664 kutokana na uuza ji wa majengo, ukusanyaji wa madeni, ufilisi na mapato kutokana na riba. Aidha, Shirika litaendelea kutumia wataalam wake na mawakili binafsi katika kusimamia kesi zilizo Mahakamani, ikiwa ni pamoja na kukutana na wadaiwa katika majadiliano na usuluhishi. Katika kukamilisha sera ya ubinafsishaji, *CHC* imeandaa programu ya ufuatiliaji wa mashirika na makampuni yaliyobinafsishwa, yaani *post privatization monitoring and evaluation*. *CHC* kwa kushirikisha Wizara mama za mashirika husika, imekusudia kufuatilia mashirika yote yaliyobinafsishwa ili kuainisha faida na upungufu wote uliojitokeza katika zoezi la ubinafsishaji na kutoa mapendekezo yanayostahili ili kuboresha huduma zinazotolewa na mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Fedha ya *Twiga Bancorp Limited*, imeendelea kujiendesha kwa faida ambapo katika mwaka 2007, ilipata faida ya Shilingi milioni 298.7. Amana za wateja ziliongezeka kutoka Shilingi milioni 23,628.7 mwaka 2006 hadi Shilingi milioni 27,724.3 mwaka 2007 na kuwezesha kutoa mikopo yenyeye thamani ya Shilingi milioni 10,869.7 mwaka 2007, ikilinganishwa na Shilingi milioni 9,697.8 iliyotolewa mwaka 2006. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2007, Twiga Bancorp ilikuwa imewekeza Shilingi milioni 12,468.6 kwenye dhamana za Serikali na amana katika benki nyingine, ikilinganishwa na Shilingi milioni 11,223.5 mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine za kibiashara kama kufungua *Letter of Credit*, kutuma pesa, kutoa mikopo midogo midogo na nyingine ziliendelea kama zilivyopangwa. Aidha, Twiga Bancorp ilijiunga na mtandao wa kutoa huduma za fedha kwa kutumia ATM ujulikanao kama Umoja Switch, chini ya makubaliano yanayo jumuisha benki tano. Benki hizo ni *Azania Bank Ltd.*, *Akiba Commercial Bank*, Benki ya Rasilimali Tanzania na *Dar es Salaam Community Bank*. Kwa ujumla, ufanisi wa Twiga Bancorp umewezesha mtaji halisi wa Benki (*core capital*.) kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 3.30 mwaka 2006 hadi Shilingi bilioni 3.80 mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, *Twiga Bancorp* imekadiria kukusanya Shilingi milioni 34,025.8 kutokana na amana za wateja, kutoa mikopo ya Shilingi bilioni 17.16 na kuwekeza fedha zenyeye thamani ya Shilingi bilioni 11.5 katika dhamana na amana katika mabenki mengine kiasi cha Shilingi bilioni 12.46. Juhudi hizi zinatarajia kuongeza mapato ya Shilingi bilioni 6.33, ikiwa ni asilimia 30 zaidi ya mapato

yaliyokusanya mwaka 2007/08. Aidha, Taasisi hii inatarajiwa kupata faida ya Shilingi bilioni 1.05.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/07, Idara ya Usimamizi wa Bima (*Insurance Supervisory Department - ISD*), imeendelea kupata mafanikio makubwa. Sekta ya Bima iliendelea kukua ambapo pato la bima lilifika Shilingi bilioni 150.3, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 115.4 mwaka 2005/06. Idadi ya Makampuni ya Bima, madalali na mawakala wa Bima, yaliongezeka kutoka 474 hadi 516. Madalali 11 walifutiwa usajili kwa sababu ya ukiukwaji wa sheria na taratibu za bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kuongezeka kwa biashara ya bima, madai ya bima yaliyolipwa yaliongezeka kutoka Shilingi bilioni 27.1 mwaka wa fedha 2005/06 hadi Shilingi bilioni 30.3 mwaka 2006/07. Aidha, vitega uchumi vy'a bima pia viliongezeka kutoka Shilingi bilioni 133.7 hadi Shilingi bilioni 136.7 katika kipindi hicho. Vilevile mali za makampuni ya bima ziliongezeka kutoka Shilingi bilioni 183.7 mwaka 2005/06 hadi Shilingi bilioni 202.5 mwaka 2006/07.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, sekta ya bima imeendelea kuathiriwa na ukosefu wa wataalamu wazalendo. Wizara kwa kushirikiana na *ISD* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, imekamilisha mipango ya kuanzisha Chuo cha Masuala ya Bima kwa kutumia majengo ya kilichokuwa Chuo cha Bima Mikocheni, Dar es Salaam, ili kutoa kozi mbalimbali katika fani ya bima hadi ngazi ya shahada na kuendelea. Chuo hiki kinatarajiwa kuanza muhula wake wa kwanza ifikapo mwezi Oktoba, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara kwa kushirikiana na *ISD* iliendelea kuboresha mazingira ili sekta ya bima iendelee kukua na kuongeza pato kwa asilimia 15 na kuelimisha makampuni zaidi hasa ya madini na yale yanayojenga barabara kukatia bima mali zao hapa nchini. Katika mwaka 2008/09, *ISD* itaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa bima, ikiwa ni pamoja na kurekebisha Sheria ya Bima na Kanuni zake ili kuweza kwenda na mabadiliko yanayotokea duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mchakato wa ubinafsishaji wa Shirika la Bima la Taifa (*NIC*), unaendelea chini ya *CHC* kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Katika mchakato huo, Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa ili Shirika la Bima la Taifa lirekebishwe kwanza na baadaye libinafsishwe kwa njia ya kuuza hisa kwa wananchi na wawekezaji mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NIC* imeendelea na biashara ya bima kwa kuandikisha wateja wapya. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2007, makusanyo ya ada za bima yalifikia Shilingi bilioni 23.7 na mapato mengineyo Shilingi bilioni 3.5. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2008, makusanyo ya ada za bima yalikuwa Shilingi bilioni 8.4 na mapato mengine yalikuwa Shilingi milioni 511. Madai ya bima hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2007 yalikuwa Shilingi bilioni 8.86 wakati madai yaliyolipwa hadi mwezi Aprili, 2008 yalifikia Shilingi bilioni 1.49. Lengo ni kulipa angalau asilimia 47 ya salio la madai ya Shilingi bilioni 21.46 ifikapo tarehe 31 Desemba, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), imeendelea kusimamia kwa makini masoko ya mitaji na dhamana kwa lengo la kulinda maslahi ya wawekezaji. Mamlaka ilitoa idhini kwa Kampuni ya Uwekezaji ya NICOL ya kuuza hisa kwa wananchi, kuruhusu Kampuni ya *TOL Gasses* kutoa hisa za upendeleo (*rights issue*) na ipia kwa Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam (DCB), kutoa hisa za upendeleo. Aidha, idhini ya kutoa hisa za faida (*bonus shares*) kilitolewa kwa Makampuni ya East African Breweries Limited na Jubilee Holdings Limited. Mamlaka iliendelea kutoa na kuorodhesha Hatifungani za Serikali za miaka 2, 5, 7 na 10 katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mchango wa Wajasiriamali wadogo na Kampuni za Kati, Mamlaka imeanza mkakati wa kuanzisha soko lao, yaani *Enterprises Growth Market (EGM)*, ili kuwawezesha kupata mitaji ya masharti nafuu bila ya kuzingatia kuwepo kwa uzoefu wa faida. Aidha, Mamlaka imelenga kuboresha ukuaji endelevu wa masoko ya mitaji na dhamana, kuwaongezea utaalam madalali wa hisa na dhamana katika masoko ya Hatifungani na kuunganisha mfumo wa shughuli za masoko ya mitaji ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Mamlaka inatarajia kuanzisha Soko la Wajasiriamali na Kampuni za kati (EGM), chini ya Soko la Hisa la Dar es Salaam ili kuwawezesha makampuni madogo kupata mtaji, kupitia Sheria ya CMSA ya 1994 na kuboresha shughuli za Mamlaka kukamilisha maandalizi ya kuanzisha Hatifungani za Serikali za Mitaa (*Municipal Bonds*), ikiwa ni pamoja na kuweka sera, sheria na taratibu zinazohitajika. Aidha, Mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu faida za soko la hisa na dhamana katika ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka itaboresha zaidi biashara ya hisa na dhamana kwa kurekebisha kanuni za ushiriki katika Soko la Mitaji, ikiwa ni pamoja na kuongeza viwango vya mitaji kwa aina mbalimbali za Kampuni za udalali na ushauri; na kupimwa utendaji kulingana na shughuli za biashara kwa kampuni husika. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine, itasimamia uunganishaji wa mtandao wa biashara ya hisa na dhamana (*trading platform*) wa Soko la Hisa la Dar es Salaam na ule wa malipo wa mabenki (*payment system*), ili kuongeza ufanisi wa malipo na ubadilishanaji wa hisa na dhamana baada ya mauzo na hivyo kuvutia zaidi uwekezaji kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), liliorodhesha uuzaaji wa hisa za Kampuni ya Uwekezaji ya NICOL na *Dar es Salaam Community Bank (DCB)*. Aidha, DSE ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha kuorodhesha hisa za *National Microfinance Bank* baada ya kufuzu na kwa kushirikiana na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, imeendelea kuwahamasisha wajasiriamali wadogo na wa kati kupata mitaji kutoka Soko la Hisa, mara baada ya kurekebisha Sheria na kuweka taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na wadau wengine, litaendelea kuelimisha umma na kushawishi makampuni zaidi kuorodhesha hisa zake katika soko. Aidha, litaanzishwa dirisha jipya la kuweza kupata mitaji ya uwekezaji kwa makampuni ya wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs), baada ya kurekebisha sheria na kanuni za CMSA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2007, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT), ilikuwa imekwishaunda Mifuko miwili ya Uwekezaji wa pamoja (*Collective Investment Schemes*); Mfuko wa Umoja ulioanzishwa tarehe 16 Mei, 2005 na Wekeza Maisha ulioanzishwa tarehe 15 Mei, 2007. Mifuko hii imekuwa na mafanikio makubwa kwa kuvutia wawekezaji wengi na ukuaji wa mtaji uliowekezwa. Aidha, baada ya kipindi cha kizuizi (*lock in period*), vipande viliendelea kuuzwa na kupunguza ukubwa wa Mfuko kutoka Shilingi bilioni 120.0 hadi Shilingi bilioni 59.0. Hata hivyo, vipande vimeendelea kuuzwa na kununuliwa na wawekezaji waliopo na wapya na Mfuko kwa sasa umekua hadi kufikia Shilingi bilioni 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma kwa wateja, Dhamana ya Uwekezaji imelazimika kuimarisha mfumo wake wa Kompyuta, ikiwa ni pamoja na kuwa na mfumo wa dharura (*Fall Back Recovery System*), nje ya ofisi ili kuwezesha huduma kuendelea kutolewa endapo kutatoka majanga. Aidha, *UTT* imeendelea kuwekeza dhima zake katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na Hatifungani za Serikali na Makampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, *UTT* inatarajia kuanzisha Mifuko mingine miwili; Mfuko wa Maendeleo ya Watoto (*Children Career Plan - CCP*) na Mfuko wa Kuweka Akiba (*Regular Income Scheme - RIS*). Mfuko wa Maendeleo ya Watoto utawawezesha wananchi kupanga maendeleo ya elimu ya watoto wao kwa kuwekeza, wakati Mfuko wa Kuweka Akiba unakusudia kumpa mwananchi uwezo wa kuweka akiba na kupokea mapato ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za michezo ya kubahatisha hapa nchini zimeendelea kukua. Hadi kufikia mwezi Juni, 2008, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (*Gaming Board of Tanzania*), iliweza kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 3.968 ikiwa ni kodi ya michezo na mapato mengine ikilinganishwa na Shilingi bilioni 3.0 kwa mwaka 2007, sawa na ongezeko la Shilingi milioni 968.01. Katika kuboresha ukusanyaji wa kodi ya michezo ya kubahatisha, Bodi imeanza kutekeleza uwekaji wa mfumo wa kompyuta wa ufuutiliaji (*Central Monitoring System*) katika mashine za kamari (*slot machines*). Zoezi hili linatarajia kukamilika mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Bodi inatarajia kuanzisha leseni mpya za uendeshaji wa biashara ya *slot machine* ijulikanayo kama *40 - machine sites*, itakayoendeshwa katika mikoa ambayo kwa sasa haina biashara za Casino. Taratibu zote za kiufundi ikiwa ni pamoja na kuweka viwango vyta ada ya leseni na kodi vimekamilika. Leseni ya kwanza itakayolipiwa ada ya Shilingi milioni 15 kwa maeneo

ya Dar es Salaam na Shilingi milioni 10.0 kwa mikoani, inatarajiwa kutolewa mwanzoni mwa 2008/09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu (FIU), kimeanza kazi baada ya Kamishna kuteuliwa. Kazi za awali zilizofanyika ni pamoja na kutayarisha na kusambaza miongozo kwa mabenki ili yaweze kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Vilevile Kitengo kimebuni na kusambaza fomu maalumu za kutolea taarifa kwa wadau ili wazipitie na kutoa maoni yao kuhusu ukamilifu wake. Pia Kitengo tayari kimeanza kupokea taarifa kutoka kwenye taasisi za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Kitengo kitaendelea na kazi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuelimisha umma kuhusu masuala ya udhibiti wa biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Vilevile Kitengo kinatarajia kuanza uchambuzi wa taarifa mbalimbali kuhusu biashara zinazoshukiwa kuwa ni za fedha haramu, baada ya kukamilisha uwekwaji wa mfumo wa kompyuta na kuajiri wachambuzi wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi mwaka jana, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kwa kushirikiana na *Millenium Challenge Corporation (MCC)*, tayari imeanzisha Chombo rasmi cha kusimamia mpango huu kinacho julikana kama *Millennium Challenge Account Tanzania (MCA-T)*. Chombo hiki kipo chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi na kinatarajiwa kikamilishe kazi yake ndani ya kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali. Jumla ya miradi 143 ilikaguliwa katika Mikoa tisa kwa lengo la kufuatilia utekelezaji na matumizi ya fedha za umma kwa jumla. Taarifa za ukaguzi huo zimeandaliiwa. Matatizo makubwa yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika ni kuto kamili kwa baadhi ya miradi katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kwa kutoa mafunzo kwa Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Serikali za Mitaa, juu ya mfumo mpya wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti na utoaji wa taarifa. Aidha, Wizara itaendelea kujenga uwezo katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti, uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na uchambuzi wa miradi ya maendeleo. Pia itaendelea kukabiliana na changamoto zilizopo, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa nidhamu katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali na kutoa taarifa za utekelezaji wa bajeti hiyo kwa wakati kama kanuni zinavyo elekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha katika Sekta ya Umma (*Public Financial Management Reform Programme - PFMRP*), ilikamili kwa mwezi Juni, 2008. Katika awamu hii, Programu

ililenga katika kuimarisha maeneo ya Usimamizi wa Fedha kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya kiuchumi ili kuiwezesha Serikali kutekeleza mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara ilitekeleza malengo mengi ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha na kuhakikisha matumizi ya Serikali kwa ujumla hayavuki bajeti iliyopitishwa na Bunge.

(ii) Kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje.

(iii) Kujenga uwezo kwa watumishi wa Wizara kwa kugharamia mafunzo na vitendea kazi. Matokeo ya utekelezaji huu yameboresha utendaji kwa kuweka malengo ya vipaumbele yanayopimika na kuhakikisha shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia Mpango wa Pili wa *PFMRP*, ambao ulimaliza muda wake Juni, 2008, Wizara imehuisha Mpango Mkakati wa Programu hiyo, ambao umeanza kutekelezwa mwezi Julai, 2008. Katika awamu hii, Programu imepanga kuboresha maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na: -

(i) Uhusiano kati ya Benki Kuu, Benki za Biashara na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ili kuimarisha usimamizi wa fedha za Umma.

(ii) Ukaguzi wa Ndani na Ununuzi katika Wizara na Halmashauri kwa kutoa vitendea kazi na kuwapatia watumishi husika mafunzo juu ya kanuni za fedha na ununuzi.

(iii) Mtandao wa Mfumo wa malipo katika taasisi zote za Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa fedha za Umma.

(iv) Mawasiliano kati ya Wananchi na Taasisi za Serikali juu ya usimamizi wa Fedha za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara iliweza kupunguza Deni la Taifa kutoka dola za Kimarekani milioni 7,188.4 kwa mwezi Desemba, 2006 hadi dola za Kimarekani milioni 7,041.20 mwezi Desemba, 2007. Kupungua kwa Deni hili, kunatokana na misamaha iliyopatikana kupitia Mpango wa *Highly Indebted Poor Countries (HIPC)* na wa *Multilateral Debt Relief Initiative (MDRI)*. Aidha, Wizara iliendelea kusimamia kikamilifu mwenendo wa madeni ya ndani na nje kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada na mkakati wa kusimamia Deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara itaimarisha uchambuzi wa mikopo ili kuhakikisha kuwa, fedha zinazotokana na mikopo zinawekezwa katika miradi yenye tija na ya kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC), imeendelea kuchambua maeneo yaliyohitaji ufanuzi katika Ripoti ya Vigezo vya kugawana Mapato na kuchangia gharama za Muungano kwa ajili ya kuziwezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kufikia maamuzi.

Aidha, Tume imekamilisha Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) wa kwanza wa miaka mitano, ambao utekelezaji wake umeanza mwezi Julai, 2008. Tume imekamilisha Uchambuzi wa Masuala ya Fedha ya Muungano na kuanza kufanya Uchambuzi katika maeneo ya uhusiano wa kifedha baina ya SMT na SMZ katika masuala ya Misaada na Mikopo, Vyanzo vya Mapato ya Muungano, Mfumo wa Takwimu wa Tume na Uhusiano wa SMT na SMZ kwenye Sera za Bajeti na Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Tume ya Pamoja ya Fedha inakusudia kutekeleza majukumu yake ambayo yameorodheshwa katika mwaka wa kwanza wa Mpango Mkakati wa Tume ambayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kutafiti na kubainisha Mifumo ya Kodi itakayokubalika na pande mbili za Muungano;

(ii) Kuandaa na kupendekeza Mfumo wa Maandalizi ya Bajeti utakaohusisha pande mbili za Muungano;

(iii) Kuandaa na kupendekeza mwongozo kuhusu Akaunti ya Pamoja ya Fedha;

(iv) Kuendelea kutoa elimu kwa wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu masuala ya kifedha ya Muungano hususan majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Sura ya 140; na

(v) Kukamilisha uchambuzi pamoja na kuandaa ripoti kuhusu uhusiano wa SMT na SMZ katika masuala ya Misaada na Mikopo, Vyanzo vya Mapato ya Muungano, Mfumo wa Takwimu wa Tume na Uhusiano wa SMT na SMZ katika Sera ya Bajeti na Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara iliendelea kuimarisha mtandao wa malipo (*Integrated Financial Management System*). Wizara iliendelea kuunganisha Hazina Ndogo Mikoani na Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa. Vilevile Wizara imeunganisha Mtandao wa Mawasiliano kati ya Mkoa wa Pwani na Makao Makuu Dar es Salaam kwa majaribio na imefunga vifaa vya kuunganisha Makao Makuu na Mikoa yote. Katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea kuimarisha mtandao wa Malipo kwa kuendelea na kazi ya kuunganisha Mikoa na Makao Makuu na kuweka mtandao katika Kambi za Jeshi na Vikosi vya Polisi. Sambamba na hilo, Wizara itaimarisha kitengo cha Mifumo ya Kompyuta (*System Development Unit*), ili kupunguza utegemezi kutoka kwa Washauri Elekezi (*Consultants*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na akaunti nyingi katika Benki za Biashara zilizofunguliwa kutokana na programu mbalimbali zinazotekelozwa Mikoani. Ili kusimamia vyema fedha za Umma, Serikali imefanya uchambuzi wa akaunti zake zote na katika mwaka 2008/09, Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali wanaohusika na akaunti hizo wakiwemo wafadhili ili kubainisha akaunti zinazotakiwa kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara itaanza maandalizi kwa ajili ya kubadilisha utaratibu wa malipo kwa hundi na kuanza kulipa baadhi ya malipo kwa mtandao (*e-Payment System*). Utaratibu huu utaanza baada ya kukamilishwa kwa uunganishwaji wa mitandao ya malipo kati ya Benki Kuu na Wizara ya Fedha na Uchumi. Katika utaratibu huu wa malipo, fedha za mlipwaji zitahamishwa moja kwa moja katika akaunti yake kutoka akaunti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu utakapoanza, wote wanaolipwa au wanaofanya biashara na Serikali, watalazimika kuwa na Akaunti za Benki. Baadhi ya faida za utaratibu huu ni kuwapunguzia kero wanaolipwa na kupunguza gharama kwa Serikali. Aidha, utaratibu huu utawezesha kuondokana na tatizo la kuwa na hundi ambazo hazijalipwa katika Usuluuhishi wa Hesabu za Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuimarisha na kuboresha Sekta ya Ununuzi wa Umma, Serikali imeanzisha Kitengo Maalum (*Public Procurement Unit-PPU*), chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi kitakachosimamia, kuratibu na kuandaa sera na miongozo ya ununuzi wa umma. Aidha, Kitengo hicho kitakuwa na jukumu la kuendeleza, kuratibu na kusimamia kada ya ununuzi wa Umma. Katika kutimiza wajibu huo, Kitengo kitashirikiana na Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma (*PPRA*), Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (*PPAA*) na wadau wengine, kuhakikisha fedha za Umma zinatumwiwa na wahusika kwa kazi na utaratibu unaofuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kuimarisha Sekta ya Ununuzi wa Umma, Wizara kwa kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*), kwa mwaka 2007/08 imefanya yafuatayo:-

(i) Mafunzo ya ununuzi kwa Wafanyakazi 940 toka Taasisi mbalimbali za Serikali na Mashirika ya Umma yalitolewa;

(ii) Nyaraka mbalimbali za zabuni (*Standard Tendering Documents*), pamoja na miongozo mbalimbali vilitayarishwa na kuwekwa kwenye tovuti (*Website*);

(iii) Ukaguzi wa ununuzi (*Procurement Audit*) ulifanywa kwenye Taasisi 20 za Umma na uchunguzi wa kina kwenye tuhuma au malalamiko yapatayo kumi na tano. Aidha, Mamlaka ilikamilisha mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa Taarifa za Ununuzi (*Procurement Management Information System*); na

(iv) Taasisi za Umma 139 zilikaguliwa juu ya utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2008/09, Wizara kupitia Mamlaka ya Ununuzi wa Umma inatarajia kufanya yafuatayo:-

- (i) Kutekeleza Mkakati wa Kuzuia Rushwa katika ununuzi wa umma.
- (ii) Kutekeleza Mpango wa Ununuzi wa Umma kwa kutumia mfumo wa kompyuta.
- (iii) Kuandaa Taratibu na Kanuni za maadili katika fani ya Ununuzi na Ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2007/08, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (*PPAA*), ilipokea rufaa 12 zinazohusu ununuzi wa umma, kati ya hizo kumi zilitolewa uamuzi na rufaa mbili bado zinashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Mamlaka inatarajia kufanya yafuatayo:-

- (i) Kushughulikia mashauri 20 ya rufaa za Zabuni;
- (ii) Kuelimisha umma katika mikoa sita ambayo ni Kigoma, Tabora, Shinyanga, Rukwa, Singida na Kagera;
- (iii) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Mamlaka na Bodi, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo mbalimbali, ili kuwawezesha kufanya uchambuzi wa mashauri yanayowasilishwa kwa ufanisi na kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Bodi ya Rufaa za Kodi (*TRAB*), imeendelea na utatuvi wa migogoro ya kodi kati ya Mamlaka ya Mapato na Walipa Kodi. Bodi ya Rufaa za Kodi imesikiliza na kutolea uamuzi migogoro 81.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi imetua elimu kuhusu Sheria ya Rufaa za Kodi Sura ya 408 na taratibu za kukata rufaa, katika Mikoa ya Tanga, Morogoro na Pwani. Elimu iliyotolewa na Bodi imesaidia sana walipa kodi kujua kuwa kuna chombo kilichoundwa kisheria kushughulikia migogoro ya kodi kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipa kodi kujua haki zao. Vilevile Bodi ya Rufaa za Kodi ikishirikiana na Baraza la Rufaa za Kodi imekamilisha mchakato wa kuandaa *Tanzania Tax Law Reports*. Taarifa hizi zitaongeza ufahamu wa sheria za kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Bodi itaendelea kupokea, kusikiliza na kuamua Rufaa za Kodi kwa wakati. Ili kuhakikisha taratibu za kukata rufaa zinafahamika zaidi, Bodi itaendelea kutoa elimu kwa wadau wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Rufaa za Kodi (*TRAT*), katika mwaka 2007/08, ilipokea rufaa mpya 38 na kuendelea na rufaa 13 za mwaka 2006/07, ambapo jumla ya rufaa 45 zilisikilizwa na kutolewa uamuzi. Baraza pia limeendelea kuelimisha

umma kuhusu Sheria za Kodi na taratibu za kukata rufaa katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Mwanza na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Baraza litaendelea kusikiliza rufaa sita zilizobaki mwaka jana. Aidha, Baraza litasogeza huduma kwa wananchi kwa kufungua *Sub-Registries* katika Mikoa ya Mbeya, Arusha na Mwanza, ambazo zitafanya kazi kikanda kuliko sasa ambapo Wakata rufaa nchi nzima hulazimika kufungua rufaa zao katika Mkoa wa Dar es Salaam tu. Kadhalika, Baraza litandelea kueneza elimu kwa walipa kodi na wadau wote, kuhusu mchakato wa kufungua rufaa na maombi mbalimbali kwenye Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara iliendelea na uandaaji wa mfumo wa kiuhasibu wa kuratibu mali zilizothaminiwa kwa kuingizwa kwenye Mfumo wa Malipo ya Serikali (*IFMS*), ambao utarahisisha kufanya usuluhisho wa mali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea na zoezi la kuondosha mali chakavu katika Wizara na Idara za Serikali, zikijumuisha baadhi ya ofisi za Balozi zetu zilizoko nchi za nje. Jumla ya Shilingi milioni 264 zilikusanywa kutokana na mauzo ya magari na vifaa vingine chakavu. Aidha, Serikali ililipa fidia na kifuta machozi jumla ya Shilingi bilioni 1.4 kwa wadai 27 waliokuwa na madai mbalimbali. Serikali ilifidiwa jumla ya Shilingi milioni 21 kutoka kwa watu waliosababisha hasara kwa ajali na potevu za mali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea na zoezi la kuhakiki, kufuta na kuondosha vifaa chakavu vikiwemo samani, magari, mitambo, dawa na vifaa vingine katika Wizara, Idara, Mikoa na Wakala za Serikali. Aidha, Wizara itakamilisha Daftari la Mali ya Serikali (*Assets Register*), lenye kuonyesha idadi na thamani yake kwa ajili ya kufanya usuluhishi kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), katika mwaka 2007/08, imeendelea kusimamia viwango vya Uhasibu na Ukaguzi, mafunzo na miongozo inayotolewa kimataifa ili kuhakikisha hesabu na ukaguzi unaofanywa unakubalika kimataifa. NBAA iliendesa semina na kuratibu mafunzo kwa Wahasibu, Wakaguzi na Walimu wa Sekta hii ili kuhakikisha viwango vinavyokubalika vinazingatiwa. Aidha, NBAA iliendelea na mchakato wa sheria na majukumu yake ya kisheria ili kutofautisha majukumu yake kama Taasisi ya Wahasibu na ya Usimamizi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, NBAA kwa kushauriana na wadau wengine, imetayarisha mtaala mpya ambao umeanza kutumika kuanzia mwezi Mei, 2008. Madhumuni ya mtaala huu ni kukidhi mabadiliko ya sheria za kodi, pensheni, masoko ya hisa, mitaji na mabadiliko ya kitaaluma yanayotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, NBAA inaendelea kuhariri, kutoa na kusimamia mitihani ili kuhakikisha inaendana na wakati na mahitaji. Hadi Juni, 2008 watahiniwa

2,477 walikuwa wamefaulu ngazi ya CPA na 13,267 ngazi mbalimbali za utunzaji wa vitabu vya hesabu za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, *NBAA* itafanya shughuli zifuatazo:-

(i) Kuishauri Wizara kuhusu kutenganisha majukumu ya *NBAA* na kuwa na Taasisi ya Wahasibu wanachama (*Institute of Certified Public Accountants – ICPAT*) na Mamlaka ya Sera, Uendeshaji na Ukaguzi Fedha Tanzania (*Accountancy Regulatory Board*).

(ii) Kuendeleza uboreshaji wa mitaala ya ufundishaji uhasibu vyuoni ili iweze kuendelea kutambulika kwa vyombo vya kifedha na uhasibu duniani kama Benki ya Dunia, Shirikisho la Wahasibu Duniani (*IFAC*) na Shirikisho la Wahasibu Afrika Mashariki, Kati na Kusini (*ECSAFA*).

(iii) Kuendelea na ujenzi wa *Accountancy Professional Centre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2007/08, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeweza kukagua Mafungu 49 ya Wizara na Idara zinazojitegemea, Mikoa yote 21, Halmashauri 124, Wakala za Serikali 33, Mashirika ya Umma 90 na Ofisi 30 za Ubalozi. Aidha, Bunge lako Tukufu katika m Kutano huu, limepitisha Sheria mpya ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 (*Public Audit Act, 2008*). Sheria hii ni mojawapo ya hatua muhimu katika kuipa uwezo zaidi Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itakagua hesabu za Ofisi zote za Serikali ikiwa ni pamoja na Mafungu 49 ya Wizara na Idara zinazojitegemea, Mikoa 21, Halmashauri 132, Wakala za Serikali 33, Mashirika ya Umma 125 na Balozi 30. Aidha, Ofisi itaanzisha Kitengo cha Ukaguzi wa Kiuchunguzi (*Forensic Audit Unit*), kuendeleza ujenzi wa majengo mawili ya Ofisi katika Mikoa ya Lindi na Morogoro, kukamilisha na kuwasilisha Bungeni taarifa nne za ukaguzi wa ufanisi (*Performance Audit Report*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya wafanyakazi, katika mwaka 2007/08, Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Iliajiri jumla ya watumishi 296 (Wahasibu 20, Wahasibu Wasaidizi 139, Wasaidizi wa Hesabu 79 na kada nyingine Watumishi 58);

(ii) Watumishi 61 walithibitishwa kazini na Watumishi 53 walithibitishwa katika nyadhifa na vyeo walivyokuwa wameteuliwa;

(iii) Jumla ya Watumishi 17 walipandishwa cheo kwa njia ya ushindani; na

(iv) Watumishi 267 walipatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali zinazohusiana na majukumu yao;

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara itafanya yafuatayo:-

- (i) Itaaajiri watumishi wapya 74;
- (ii) Kuthibitisha watumishi ambao wamemaliza kwa mafanikio muda wao wa majaribio. Aidha, watumishi wenyе sifa watapandishwa cheo;
- (iii) Itatoa mafunzo endelevu ndani na nje ya nchi kwa watumishi kulingana na mpango wa mafunzo ulioandalialiwa; na
- (iv) Kuendelea kudhamini mafunzo kwa watumishi katika fani za Uhasibu, Teknolojia ya Habari na Ununuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara iliendelea na uratibu na usimamizi wa Asasi za Mafunzo zilizo chini yake. Asasi hizo ni Taasisi ya Uhasibu Tanzania (*TIA*), Chuo cha Uhasibu Arusha (*IAA*), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*), Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini – Dodoma na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika.

Mambo yafuatayo yalifanyika katika mwaka huo ambayo ni ujenzi wa majengo mbalimbali kama maktaba, mabwalo ya chakula, ofisi na majengo ya mafunzo; kusajili na kusomesha wanafunzi katika kozi za muda mfupi na mrefu; kufanya utafiti na kuchapisha vitabu vya taarifa mbalimbali; kuwadhamini wahadhiri katika mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*Ph.D*) na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Asasi hizo zinatarajia kuendelea na shughuli zao za msingi, ikiwa ni pamoja na kuajiri wahadhiri Waandamizi wenyе sifa na uzoefu kulingana na vigezo vya *NACTE*; kuendeleza ujenzi wa madarasa, kumbi za mihadhara, maktaba na mabwalo ya chakula. Aidha, baadhi ya asasi zitaanzisha programu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza jitihada za kupunguza kero za Wafanyakazi nchini, hususan ucheleweshwaji wa mishahara, Wizara inaendeleza mkataba wake na NMB wa kuwalipa Watumishi wa Serikali mishahara yao tarehe 20 ya kila mwezi. Wizara pia, inaendelea na mkataba na Kitengo cha *Expedited Mail Services (EMS)* cha Shirika la Posta, kusafirisha *pay roll* kwenda Ofisi za Hazina Ndogo katika kila Mkoa ili ziwafikie wahuksika na kufanya malipo mapema. Wizara itaendelea na utaratibu wa kufikisha hundi NMB, pamoja na orodha ya walipwaji kabla ya tarehe 20 ya kila mwezi. Utaratibu huu umeendelea kuleta ufanisi wa malipo na kupunguza kero kwa Watumishi. Aidha, Wizara italipa malimbikizo ya mishahara ya Watumishi wa Serikali (Januari hadi Juni 2008), kutokana na makubaliano ya nyongeza ya mishahara iliyotakiwa kuanza kutekelezwa tangu mwezi Januari, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Julai 1995, pensheni za Wastaifu zimekuwa zikilipwa kwa utaratibu wa miezi sita. Mwezi Julai, 2008, pensheni imelipwa kwa mwezi mmoja kupitia akaunti za Wastaifu. Kutokana na malalamiko ambayo yamejitokeza, Serikali itarejesha malipo ya miezi sita kwa kulipa Pensheni ya miezi mitano iliyobaki mwezi huu wa Agosti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2004/05, Serikali iliamua kuwarejesha wastaifu waliokuwa wamelipwa mafao kwa mkupuo. Lengo lilikuwa kuwarejesha wastaifu 26,536, ambao wanarejeshwa kila baada ya Mstaifu kutimiza miaka kumi tokea tarehe ya kustaifu. Hadi kufikia Juni, 2008, jumla ya wastaifu 21,152 wamerejeshwa katika daftari la wastaifu. Zoezi hili litaendelea katika mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna matatizo ya wananchi wengi kutoelewa taratibu za mirathi. Hii imesababisha malipo ya mirathi kutofanyika kwa wakati na kuifanya Wizara ionekane ndiyo inachelewesa malipo ya Mirathi. Madai ya mirathi yana wadau wengi, ikiwa ni pamoja na mke/mume, watoto wa marehemu, ndugu wa marehemu, Mahakama, Mwajiri, Taasisi za Dini na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Inatakiwa kila mdau atimize wajibu wake ili malipo haya yaweze kufanyika katika muda unaotakiwa. Matatizo yatokanayo na madai ya mirathi ni pamoja na Wasimamizi na Warithi kutoelewa taratibu za kufuata baada ya kifo cha mtumishi; migogoro katika familia kuhusu kuteua msimamizi wa mirathi na hivyo kuchelewesa ufunguaji wa mirathi mahakaman; waajiri kuchelewa kuwasilisha Hazina majalada yenye nyaraka zinazotakiwa, warithi kutochukua malipo yao katika mahakama walizofungua mirathi kutokana na ama kutopata taarifa au kutojua mchakato mzima wa malipo ya mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Serikali itaboresha utoaji huduma kwa wastaifu na malipo ya mirathi, ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vy ya habari. Aidha, Wizara itaendesha semina za kikanda zitakazowahusisha waajiri hasa maafisa wanaoshughulikia mafao katika Wizara na Mikoa kuhusu wajibu wao wa kushughulikia mafao ya kustaifu na mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwezi Septemba, 2004, Serikali iliteua Kamati ya Muafaka (wawakilishi wa Serikali na wawakilishi wa wastaifu), kuangalia upya mafao ya wafanyakazi wa Jumuia ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977. Kamati ilimaliza kazi yake na hatimaye mapendekezo ya Kamati ya Muafaka yalipitishwa na Baraza la Mawaziri Juni, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusainiwa kwa makubaliano hayo (*Deed of Settlement*), zoezi la kukokotoa na hatimaye kulipa mafao hayo lilifanyika kuanzia mwezi Septemba, 2005. Wizara ililipa mafao hayo kwa mujibu wa makubaliano ya pande mbili na Wastaifu wote waliostahili kulipwa malipo hayo, walilipwa kwa kufuata taratibu za malipo. Kinachoendelea sasa ni kutatua matatizo ya Mstaifu mmoja mmoja pale kunapojitokeza malalamiko ya upunjwaji wa malipo. Kwa sababu ya muda, sitawenza kusoma yote kwa hiyo nachagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*), mwaka 2007/08, uliendelea kutekeleza jukumu lake la ulipaji mafao kwa mujibu wa sheria. Mfuko pia uliendelea kusajili wanachama, kuhifadhi kumbukumbu sahihi za wanachama, kukusanya michango na kuiwekeza. Katika jitihada za kuondoa tatizo la ukosefu wa kumbukumbu za watumishi, Mfuko umeendelea kukusanya kumbukumbu hizo wakati wa zoezi la usajili na wakati wa utoaji wa semina mbalimbali kwa wadau nchini kote. Hadi Juni, 2008, Mfuko ulikusanya jumla ya Shilingi bilioni 211.40; michango ya wanachama ikiwa ni Shilingi bilioni 152.00 na mapato yatokanayo na vitega uchumi Shilingi bilioni 59.40. Aidha, Mfuko ulifungua ofisi katika mikoa minane ili kusogeza huduma karibu zaidi na Watumishi. Mikoa hiyo ni Mbeya, Arusha, Mwanza, Mtwara, Iringa, Morogoro, Shinyanga na Kigoma. Jumla ya Shilingi bilioni 116.10 zilitumika kulipa mafao, ikiwa ni pamoja na kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi. Aidha, jumla ya Wanachama 2,784 walistaifu katika mwaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 236.03, michango ya wanachama ikiwa ni Shilingi bilioni 178.63 na mapato yatokanayo na vitega uchumi Shilingi bilioni 57.40. Mfuko utawekeza katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Ujenzi huu utajumuisha madarasa, mabweni maktaba, zahanati na viwanja vya michezo. Mfuko pia utashiriki katika ujenzi wa makazi ya polisi na nyumba za gharama nafuu. Mpaka sasa Mfuko umepata viwanja katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Mtwara, Tabora, Shinyanga na Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi huo. Mfuko unatarajia kulipa kiasi cha Shilingi bilioni 172.62 kwa ajili ya mafao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi.

Aidha, jumla ya wanachama wapatao 3,033 wanatarajia kustaafu kwa mujibu wa sheria. Vilevile Mfuko unatarajia kufungua ofisi katika Mikoa yote iliyobakia. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2009, Mfuko unatarajiwa kufikia thamani ya Shilingi bilioni 638.62, sawa na ongezeko la asilimia 9.47 kutoka Shilingi bilioni 583.40 mwishoni mwa mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Mfuko wa Akiba ya wafanyakazi Serikalini (*GEPF*), uliendelea kuboresha huduma kwa wanachama, kukusanya michango kutoka kwa wanachama, kuwekeza fedha za wanachama katika vitega uchumi vilivyo salama na kulipa mafao kwa wanachama wastaafu. Katika kipindi hicho, Mfuko ulikamilisha zoezi la kuweka kumbukumbu za wanachama katika mfumo wa kompyuta. Zoezi hili limesaidia kuboresha huduma zake kwa wanachama na kuweza kulipa mafao yao kwa wakati. Vilevile Mfuko umekamilisha kutengeneza Tovuti yake ili kurahisisha mawasiliano na wanachama wake. Hadi Juni, 2008 Mfuko ulikusanya jumla ya Shilingi milioni 39,179.68. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 116 ya malengo ya mwaka. Hivi sasa Mfuko umesajili jumla ya waajiri 34 wanaojiri kwa njia ya mkataba na kufanya idadi ya wanachama waliosajiliwa na Mfuko kufikia jumla ya 29,888.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Mfuko utaendelea kupanua wigo wa wanachama wake kwa kuwafikia waajiri wengi zaidi. Mfuko unategemea kukusanya jumla ya Shilingi milioni 49,713.69 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo ongezeko la wanachama wapya 3,000 wanaotarajiwa kusajiliwa katika

mwaka 2008/09. Inakadiriwa kuwa Mapato yatokanayo na vitega uchumi yataongezeka kwa asilimia 4.85 kutoka Shilingi milioni 4,857.91 mwezi Juni, 2008 hadi Shilingi milioni 5,093.4 mwezi Juni 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*), ulikusanya michango yenye thamani ya Shilingi bilioni 83.58 katika mwaka 2007 kutoka kwa wanachama wake, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 62.04 zilikusanywa mwaka 2006. Mapato kutokana na uwekezaji yaliongezekwa kwa asilimia 33 zaidi ya lengo la Shilingi bilioni 27.3 na kufikia Shilingi bilioni 33.74 mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007, Mfuko ulilipa mafao kwa wanachama wake ya jumla ya Shilingi bilioni 24.83, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 21.65 zilizolipwa mwaka 2006, ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.7. Thamani ya Mfuko katika mwaka 2007 ilikua kwa asilimia 26.56 hadi Shilingi bilioni 390.31, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 317.15 mwaka 2006. Ongezeko hili limetokana na ziada ya Shilingi bilioni 73.16 lililotokana na ukusanyaji wa michango na mapato ya uwekezaji. Katika mwaka 2008, *PPF* inategemea kuwa, thamani ya Mfuko utakua hadi kufikia Shilingi bilioni 477.52 kutokana na ukusanyaji wa michango na uwekezaji. Aidha, Mfuko unatarajia kuandikisha wanachama 29,752 kutoka katika sekta ya umma na binafsi, pamoja na kulipa mafao yenye thamani ya Shilingi bilioni 24.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (*NBS*), katika mwaka 2007/08, iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu zinazohitajika na wadau mbalimbali. Zoezi la ukamilishaji wa marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2001 kwa kutumia mfumo mpya wa Umoja wa Mataifa (SNA 1993) lilifanyika. Utayarishaji wa Takwimu za Hali ya Uchumi kwa mwaka 2007, ulikamilika kwa kutumia takwimu zilizorekebishiwa. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kutayarisha Takwimu za mfumko wa bei kila mwezi na takwimu za ajira kwa mwaka. Kazi ya kutenga maeneo kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, inaendelea na imekamilika katika Mikoa miwili ya Pwani na Kilimanjaro. Ofisi ya Taifa ya Takwimu imehakikisha kuwa, tafiti mbalimbali zinaendelea kufanyika ipasavyo kama zilivyoainishwa katika MKUKUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendeleza shughuli zote zilizotajwa hapo awali. Aidha, itahakikisha kuwa tafiti mbalimbali zitaendelea kufanyika ipasavyo kama zilivyoainishwa katika MKUKUTA, ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo ya kuhesabia watu kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Takwimu za Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa mwaka 2008/09 zitatayarishwa, ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa Takwimu za Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2001 kwa sekta za Fedha na Utawala. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kutayarisha takwimu za mfumko wa bei kila mwezi, takwimu za ajira na utayarishaji wa takwimu za Hali ya Uchumi kwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kujenga uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kuhakikisha kuwa ukarabati wa jengo lake unakamilika na kuipatia vitendea kazi. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea na mchakato wa Mpango Kabambe wa Kuimarisha Takwimu Tanzania (*Tanzania Statistical Master Plan - TSMP*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea kuratibu utekelezaji wa MKUKUTA kupitia Mfumo wa Ufutiliaji wa MKUKUTA (*MKUKUTA Monitoring System - MMS*). Kupitia mfumo huu, Serikali hupima matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA kwa kukusanya takwimu, kufanya tafiti na chambuzi mbalimbali na kufanya mawasiliano na wadau mbalimbali ili kupata maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara iliandaa na kuchapisha Taarifa ya Utekelezaji wa MKUKUTA (*MKUKUTA Annual Implementation Report*) na Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu (*Poverty and Human Development Report - PHDR*). Taarifa hizi, pamoja na kutoa hali halisi ya utekelezaji wa MKUKUTA, zinabainisha pia changamoto mbalimbali katika vita dhidi ya umaskini. Aidha, taarifa hizi huainisha maeneo na vipaumbele vya kufanya kazi ili kuharakisha kufikiwa kwa malengo ya MKUKUTA. Mfumo mpya wa utoaji taarifa za utekelezaji wa MKUKUTA kwa njia ya kompyuta (*RIMKU II*) umeandaliwa. Mfumo huu utawezesha wadau husika kuandaa taarifa kwa wakati na kuzitumia katika maamuzi na mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaratibu ukamilishaji wa mchakato wa kuandaa Mpango wa Kulinda Makundi yaliyo katika hatari ya kutumbukia kwenye dimbwi la umaskini (*Tanzania Social Protection Framework*). Matarajio ya Serikali ni kuwa mara mpango huu utakapokamilika, utatoa mwongozo kwa wadau wote ikiwa ni pamoja na Serikali, Wahisani na Asasi Zisizo za Serikali (AZISE), kuhusu jinsi ya kushughulikia makundi maalum ili yaweze kunufaika katika uchumi wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea kuratibu mpango wa ufuutiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA kwa kufanya tafiti na uchambuzi; kuandaa taarifa mbalimbali zinazolenga kupambana na umaskini; kuendelea kutoa mafunzo juu ya utayarishaji wa Ripoti ya Utekelezaji wa MKUKUTA kwa kutumia mfumo mpya wa RIMKU; kukamilisha na kusambaza Mwongozo wa Kulinda Makundi yaliyo katika hatari ya kutumbukia kwenye dimbwi la Umaskini, kuendesha mijadala ya kisekta inayohusu mwingiliano wa sekta katika maeneo ya utekelezaji wa MKUKUTA; kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano wa MKUKUTA kwa nia ya kuhamasisha kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea kuwezesha Wananchi Kiuchumi kupitia Miradi ya *Small Entrepreneurs Loan Facility (SELF)*, Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato (*National Income Generation Programme - NIGP*); na Mfuko wa Uwezeshejani Wananchi Kiuchumi. Mradi wa *SELF* hutoa mikopo ya jumla kwa Asasi zinazotoa mikopo midogo midogo (*Microfinance Institutions*) ili ziweze kuwakopesha wajasiriamali wadogo wadogo katika Mikoa ya Pwani, Dodoma, Lindi, Morogoro, Mtwara, Singida, Mwanza, Mara, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Ruvuma, Mbeya na Iringa; na Mikoa ya Tanzania Visiwani. Hadi tarehe 30 Juni 2008, *SELF* imekwishatoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 15.43 kwa asasi za kifedha 186.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato iliendelea kutekeleza miradi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi katika sekta za kilimo, miundombinu na biashara ndogo ndogo. Katika kipindi cha mwaka 2007/08, Programu ilitekeleza jumla ya miradi saba kupitia Jumuiya za walengwa. Miradi iliyohusika ni ya uzalishaji chumvi Unguja na Pemba; ufugaji nyuki Rufiji, Chamwino na Bahi; mradi wa mamalishe na mradi wa vijana wa Kambi ya Madale - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea kuwesehsa wananchi kiuchumi kupitia Miradi ya *SELF*, *NIGP* na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kuhusu Mradi wa *NIGP*, shughuli kubwa zitakazoendelea kutekelezwa ni uhamasishaji na kutoa mafunzo kwa walengwa wa miradi, ununuzi wa vifaa mbalimbali vyta miradi, kuimarisha na kupanua miundombinu na kukamilisha ukarabati wa Ofisi ya Jumuiya ya Wazalishaji Chumvi Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *SELF* utasambaza huduma zake katika mikoa saba ya Kigoma, Manyara, Rukwa, Kagera, Shinyanga, Dar es Salaam na Tabora ili kukamilisha huduma za Mradi nchi nzima na kusogea huduma za Mradi karibu na walengwa baada ya kuunda baadhi ya ofisi ndogo za kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (*NEEC*), katika mwaka 2007/08, liliendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ambapo Mpango Mkakati wa Baraza (2008/09 – 2012/13) uliandaliwa. Aidha, Baraza liliratibu maandalizi ya mipango mbalimbali ya kusimamia na kuhimiza utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji, pamoja na kutayarisha mfumo wa ufuutiliaji na tathmini. Vilevile Baraza liliendelea kutoa mafunzo na kuhamasisha kuhusu Sera na Sheria ya Uwezeshaji, ambapo katika kipindi hicho mikoa saba ilipatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwawezesha Wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwenye Mfuko wa Uwezeshaji, hali ambayo imeongeza ajira. Katika awamu ya kwanza, mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 32.3 ilitolewa kwa Wajasiriamali 38,000 kufikia tarehe 3 Machi 2008. Fedha hii ilitokana na Shilingi bilioni 10.5 zilizotengwa na Serikali, pamoja na fedha kutoka kwenye mabenki yaliyohusika na kusimamia utoaji wa mikopo hiyo. Katika awamu ya pili ya Mpango huu, Serikali imetenga Shilingi bilioni 10.5. Benki na Taasisi ndogo za kifedha 13 zimeteuliwa kutoa mikopo katika Wilaya ambazo hazikufikiwa kabisa au zilipata mikopo yenye thamani isiyozidi Shilingi milioni 200. Pamoja na mikopo, wananchi walipewa mafunzo ya ujasiriamali na kuzijengea uwezo asasi mbalimbali za kiuchumi za wananchi kama vile *SACCOS* na *SACAS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kuelimisha na kuhamasisha wadau mbalimbali katika Mikoa 14 iliyobaki na kutafuta vyanzo vingine vyta fedha kwa madhumuni ya kutunisha mfuko wa uwezeshaji. Aidha, Serikali itaendelea kuipitia mifuko mbalimbali ilioanzishwa, kwa lengo la kuiwianisha ili iweze kutumika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu ambayo nimekwishayaeleza na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara inaomba Bunge lako liidhinishe kwa Fungu 50, kiasi cha Shilingi 29,690,337,000 kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 78,370,450,000 kwa matumizi ya maendeleo; kwa Fungu 21, Shilingi 733,709,524,800 kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 30,083,799,000 kwa matumizi ya maendeleo; kwa Fungu 22, Shilingi 675,699,758,000; kwa Fungu 23, Shilingi 97,042,056,000 kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 8,237,469,000 kwa matumizi ya maendeleo; kwa Fungu 45, Shilingi 12,280,798,000 matumizi ya kawaida na Shilingi 5,600,000,000 kwa matumizi ya maendeleo.

Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Uchumi, matumizi ya kawaida Shilingi milioni 29,690.0. Kati ya hizo mishahara ni Shilingi milioni 1,638.16 na matumizi mengine ni Shilingi milioni 28,052.18. Miradi ya Maendeleo Shilingi milioni 78,370.45; kati ya hizo fedha za ndani ni Shilingi milioni 6,697.0; na fedha za nje ni Shilingi milioni 71,673.45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 21 – Hazina; jumla ya matumizi ya kawaida Shilingi milioni 733,709.5; kati ya hizo Shilingi milioni 410,168.5 ni kwa ajili ya Matumizi ya Fungu hilo, pamoja na Marekebisho ya Mishahara ya Watumishi wote wa Serikali kuanzia Januari hadi Juni, 2008, fedha za Matumizi Maalum Shilingi milioni 197,157.9 na fedha kwa ajili ya TRA Shilingi milioni 126,383.1; Miradi ya Maendeleo Shilingi milioni 30,083.7; fedha za ndani Shilingi milioni 11,286.6; na fedha za nje Shilingi milioni 18,797.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 22 - Deni la Taifa. Deni la Taifa ni Shilingi milioni 675,699.8.

Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali; Matumizi ya kawaida Shilingi milioni 97,042; kati ya hizo mishahara ni Shilingi milioni 2,191 na matumizi mengineyo Shilingi milioni 94,851; Miradi ya Maendeleo Shilingi milioni 8,237.5; fedha za ndani Shilingi milioni 1,772.5; na fedha za nje Shilingi milioni 6,465.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ulaguzi; matumizi ya kawaida Shilingi milioni 12,280.8, kati ya hizo mishahara Shilingi milioni 10,442.5 na matumizi mengineyo Shilingi milioni 1,838.3; miradi ya maendeleo Shilingi milioni 5,600.0; fedha za nje Shilingi milioni 2,800.0; na fedha za ndani Shilingi milioni 2,800.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu kinaleza yote, lakini mengine sikuweza kuyasoma kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yako ya makadirio. Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati, Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwatambue wageni wa Wizara hii, ambao ilibidi niwatambue kabla hatujaanza, lakini si mbaya nikiwatambua sasa hivi.

Wageni waliopo jioni hii ni watano kutoka Wizara ya Fedha, ambao ni Ndugu Alphonse Kihwela, ambaye ni *CEO* wa Benki ya Posta, nafikiri yupo hapa ndani. Halafu tunaye Ndugu Kapelega, Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Posta, tunaye Ndugu Bernadetha Gogadi, Mkurugenzi, tunaye Ndugu Mystika Mapunda, Mkurugenzi na Ndugu Pascal Nkuba, Mkurugenzi pia.

Halafu tunao jumla ya wanafunzi 40 na walimu kutoka Shule ya Msingi Valentine iliyopo Dar es Salaam na wameambatana na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, ambaye ni Ndugu Fidelis Manga. Ningombwa wasimame nao kama wako hapa ndani. Tunashukuru sana asanteni sana, kaeni na karibuni sana na siku nyingine mkipata nafasi mje kushirikiana nasi. (*Makofii*).

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho; Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, ameomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, kesho Jumamosi, tarehe 23, wasisahau kwamba, watakuwa na kikao kinachohusu shughuli za *UNESCO* kuanzia saa 02:30 asubuhi katika Ukumbi wa VETA. Baada ya matangazo hayo, namwomba Mheshimiwa Job Ndugai, aje anisaidie kuendelea na shughuli za Bunge na mimi nikafanye shughuli nyingine.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ili tuweze kuendelea tumalizie tangazo moja la mwisho la mgeni wa Mheshimiwa Lucy Owenya, Ndugu Beatrice Muhone, mwimbaji wa kimataifa wa nyimbo za injili. Karibu sana Bungeni. (*Makofii*)

Baada ya hapo, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, karibu sana.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009: Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Uchumi, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 – Deni la Taifa, Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuiletea Kamati ya Fedha na Uchumi, kazi ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, Kamati ilikutana tarehe 24 na 30 Juni, 2008 na kupokea maelezo ya muhtasari wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo na ufungu wake kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia, ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha. Ni matumaini ya Kamati kuwa, katika mwaka huu pia Wizara itajitahidi kufikia malengo yake kwa wakati na usahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyofahamika, Wizara hii majukumu yake yameunganishwa na iliyokuwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, baada ya Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri. Hivyo basi, wakati Kamati inapitia na kujadili Bajeti ya Wizara hii, ilipata fursa ya kujielimisha kuhusu kazi na majukumu mbalimbali yanayotekelawa na Wizara hii mpya ya Fedha na Uchumi, pamoja na Taasisi zilizo chini yake. Katika hatua hiyo, Kamati ilipata fursa ya kujifunza mambo muhimu yafuatayo: Dira na madhumuni ya Wizara; Uongozi na Muundo wa Wizara; Majukumu ya Idara na Vitengo vya Wizara; Taasisi zilizo chini ya Wizara; na utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati ilipokuwa inafanya uchambuzi wa kina kuhusu majukumu na vitengo chini ya Wizara hii, Kamati ilipata wasiwasi kuwa uzoefu unaonyesha kuwa eneo la mipango huwa halipati usimamizi unaostahili wakati Wizara ya Fedha inapounganishwa na shughuli za mipango. Dalili za hali hii zimeanza kujionyesha, kwani hata tathmini timilifu ya utekelezaji wa MKUKUTA katika kipindi kilichopita haikufanyika. Bila ya mipango tunaweza kushindwa hata kuchagua, hususan maeneo yetu yanayohitaji kupewa kipaumbele ili kuibua uchumi wetu, kwa maana ya kukua kwa uchumi kunakoendana na maendeleo ya kiuchumi, hasa kwa jamii. Aidha, hata udhibiti wa upandaji wa gharama ya maisha umekuwa ni changamoto kubwa, kwa sababu kwa kawaida tu mfumo wa Wizara unaangalia zaidi uamshaji wa mapato badala ya Menejimenti ya Uchumi, ili kuleta uchumi tulivu katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo moja lilijidhihirisha wakati Waziri wa Fedha na Uchumi alipowasilisha Mpango wa Maendeleo bila kuwepo kwa maeleo ya Dira ya Taifa 2025, kwa maeleo kuwa, eneo hili halipo katika majukumu aliyokabidhiwa. Kwa mantiki hii, Kamati yangu inampongeza Mheshimiwa Rais, kwa uamuza wake wa Kuunda Tume ya Mipango. Chombo hiki ni muhimu sana na hivyo ndicho kitakuwa kitovu cha fikra na dhana zote za jinsi ya kuandaa mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu (*think tank*). Kamati inashauri kuwa, Chombo hiki kitakachokuwa chini ya Ofisi ya Rais ni vyema kikawa chombo huru, ambacho hakitaingiliwa katika utendaji kazi wake. Tume ya Mipango inatakiwa iwajibike tu moja kwa moja kwa Rais. Katika nchi zilizopata mafanikio makubwa katika uchumi chini ya matumizi ya Tume ya Mipango, kwa mfano, China, India na kadhalika; Tume imekuwa ndio Wizara mtambuka (*Focal and Central Ministry*), ambayo maagizo yake ndio matokeo ya utekelezaji katika Wizara nyingine zote, kimsingi ndio maagizo yatokayo Ofisi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchakato wa kuunda Tume ya Mipango ni vyema vile vile kubuni utaratibu mzuri wa kuunganisha chombo hiki na Bunge letu

Tukufu. Ni vyema utaratibu wa kuunganisha chombo hiki na Bunge kama Kamati ya Mipango uwekwe vizuri. Katika kipindi hiki, Kamati imeshuhudia shughuli za Tume ya Mipango kuwajibika kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na hata Kituo cha Uwekezaji Tanzania nacho kikiwekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Tume ya Mipango na Kituo cha Uwekezaji vinapaswa kutumia Kamati ya Fedha na Uchumi kama kiungo chake na Bunge. Kamati yangu ina jukumu la kuyaoanisha majukumu ya Sekta za Kiuchumi, kwa hiyo, Tume na *TIC* inapaswa kuwajibika kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, hasa ikizingatiwa kuwa suala la Mipango na Uwekezaji ni maeneo muhimu katika kukuza uchumi (*Planning and Investment Drive*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, yakiwemo matarajio ya Matumizi na Mpango wa Maendeleo. Aidha, Kamati ilifahamishwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2007/2008, Kamati ilitoa maoni na ushauri juu ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali. Katika kupitia Taarifa ya Wizara, Kamati iliridhika na utekelezaji wa baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati. Aidha, kwa maeneo ambayo utekelezaji wake haukufanyika kwa ufanisi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa utekelezaji katika maeneo hayo ufanyike kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ulikuwa mzuri na mambo yafuatayo yalitekelezwa: Kusimamia na kuendeleza uchumi; ukusanyaji mapato; kujenga uwezo na ujuzi (*Capacity Building*); kusimamia matumizi; usimamizi wa Mashirika/Taasisi za Umma; ukaguzi wa miradi; usimamizi wa fedha za ndani na nje; manunuzi ya umma na rufani za zabuni; rufaa za kodi; uhakikimali ya Serikali; habari; elimu na mawasiliano; ukaguzi wa ndani; huduma za kisheria; Deni la Taifa; pensheni na ukaguzi wa hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha mwaka 2007/2008, hususan katika ukusanyaji wa mapato, bado Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (i) Kupanda kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia;
- (ii) Misamaha ya Kodi, Sheria ya Madini na Sheria ya Uwekezaji, pamoja na Mikataba inayotokana na Sheria hizo inatoa misamaha ya kodi katika miradi kwenye maeneo hayo. Misamaha hii imekuwa ikiikosesha Serikali mapato;
- (iii) Upatikanaji wa fedha za kigeni, kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha kutoka kwa Wafadhili hata pale ambapo fedha hizo zimekubaliwa na pande zote (Wafadhili na Serikali), na kuingizwa kwenye Bajeti; na

(iv) Viwango vya Pensheni vimeendelea kuwa vidogo. Wastaafu wengi wanaathiriwa na viwango hivyo ambavyo vinaathiriwa na mfumko wa bei na kusababisha kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, ilikuwa na changamoto zifuatazo: Utunzaji mbovu wa nyaraka katika Taasisi zinazokaguliwa; ucheleweshaji wa ufungaji wa hesabu katika Halmashauri, Serikali Kuu na Taasisi zake; upungufu wa vitenda kazi; na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutumia baadhi ya majengo ya wateja wao, jambo ambalo linaathiri utendaji wa wakaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa maoni na mapendekezo kwa Wizara ya Fedha na Uchumi katika utekelezaji wa bajeti yake ya mwaka 2008/2009 na katika kupanga mipango ya baadaye ya Wizara. Serikali ina mashirika mengi ya umma, ambayo kimsingi mmiliki wa mashirika hayo ni Msajili wa Hazina. Mashirika haya yanatakiwa kurejesha gawio kutoka kwenye faida yake kwa mwenye mali kila mwaka. Hata hivyo, imebainika kuwa, mashirika mengi hayatoi gawio la kutosha kulingana na faida yanayopata. Kwa kuwa kuna kitengo cha kiintelijensia ya kifedha, Kamati inashauri kitengo hiki kiyachunguze mashirika haya, kubaini jinsi Serikali inavyoweza kuongeza mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Maboresho ya Mashirika ya Umma yanayoendelea, Kamati inashauri kuwa hisa zinazobakizwa kwa ajili ya Serikali ziwe nyingi ili wananchi wapate kuzinunua kwa bei nafuu, pale shirika linapoboreka na uamuzi kufikiwa kulimilishwa shirika hilo kwa asilimia mia. Hii itasaidia kuwaongeza wananchi wazawa kumiliki uchumi wao wenye. Halmashauri zimekuwa zikichelewa kukamilisha taratibu zao za bajeti kwa maeleo kuwa, mwongozo wa bajeti huwa unacheleweshwa. Kamati inaisitiza Wizara kuwa, ucheleweshaji huu hukwamisha sana shughuli za maendeleo; hivyo, ukomeshwe mara moja. Ili kuongeza mapato ya nchi, Kamati inarudia kuisisitiza Wizara kurejea maeneo yote ya misamaha ya kodi na kupunguza zile sehemu ambazo hazina ulazima sana wa kupata misamaha hiyo. Katika Muswada wa Fedha (*Finance Bill*) ujao, Kamati inategemea kuona mabadiliko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Twiga (*Twiga Bancorp*), ni mali ya Serikali kwa asilimia mia. Hata hivyo, Benki hii mtaji wake ni mdogo; hivyo, kimsingi si benki kamili. Mtaji wake kwa sasa ni bilioni 3.8 tofauti na bilioni tano, ambacho ni kiwango kilichowekwa na Benki kuu kwa taasisi ya fedha kufikia hadhi ya kuwa benki ya kibashara (*Commercial Bank*). Tofauti ni ndogo (*Shilingi bilioni 1.2*).

Kamati inajuliza, kuna ugumu gani kwa Serikali kutoa Shilingi bilioni 1.2 kuongeza benki hii ili iwe benki kamili? Ni dhahiri kama nia ipo, kiasi hicho ni kidogo. Vile vile Kamati inaishauri Serikali kuitumia Benki hii katika shughuli zake za kifedha; badala ya kurundika fedha nyingi kwenye Benki nyingine, baadhi ya akaunti zaweza kuhamishiwa katika benki hii ili kuiendeleza na kuipa uwezo zaidi. Kwa kuwa bado bajeti yetu ni tegemezi na Wizara hii ndiyo inayosimamia deni la nje, pamoja misaada ya kibajeti, Kamati inaishauri Wizara ijielimishe sababu za kuchelewa kwa misaada ya

kibajeti iliyoahidiwa ili tusije kukwama tena kama ilivyozoleka huko nyuma. Kama misaada hiyo ina masharti, basi Serikali ione ni vipi yaweza kutimiza masharti hayo kwa wakati ili pesa hizo zipatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza Serikali kwa hatua zilizofikia mpaka sasa kuhusu maboresho ya Shirika la Bima la Taifa. Hata hivyo, bado Kamati inasisitiza kukamilika mara moja kwa taratibu zilizosalia kuhusu hatma ya shirika hilo, hasa malipo ya wafanyakazi. Kwa kuwa Fedha zilikwishatengwa toka bajeti ya mwaka jana, vikwazo vya malipo hayo vitatuliwe mara moja ili shirika hili linusuriwe. Kamati inapenda kuona Shirika hili likiboresha huduma zake na hivyo kusaidia kukua kwa uchumi wa nchi yetu. Kamati inapenda kuikumbusha Wizara ya Fedha na Uchumi kuwa yenye ndio kitovu cha Wizara zote. Kushindwa kuwajibika vyema kwa Wizara hii, mwisho wa siku kutapelekea kushindwa kufikia malengo kwa Wizara nyingine. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Wizara kutekeleza mipango yake kwa umakini na uangalifu ili kufikia malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati inapenda kuisisitiza Wizara ya Fedha na Uchumi, kuzingatia ushauri uliotolewa nayo wakati wa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti. Maeneo ya matumizi bora ya fedha (*expenditure tracking unit*), uainishaji wa akaunti nyingi za Halmashauri za Wilaya, uratibu wa mifuko zaidi ya 20 inayoelekezwa kwenye maeneo hayo, udhibiti wa bei za mafuta hususan katika kipindi hiki tunachoanza kushuhudia kuteremka bei za mafuta, uwajibikaji, kujali muda na utoaji wa maamuzi ya haraka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Naibu Mawaziri wa Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Omari Yusuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Katibu Mkuu, Ndugu Gray Mgonja, Naibu Makatibu Wakuu, pamoja na Wataalamu wao, kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na Ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara hii, kwa Ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha mwaka wa Fedha uliotangulia. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii, kuwatambua Wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Anthony

M. Diallo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Andrew J. Chenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashillilah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii, kwani sote kwa pamoja tumeweza kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na wala sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru sana wananchi ninaowawakilisha wa Jimbo la Handeni. Inanipa moyo sana, sote kwa pamoja kuelewa kuwa subira yavuta heri na mambo mazuri hayataki haraka, ahsanteni sana wananchi wa Handeni. Mwisho, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, Waziri wa Fedha na Uchumi, muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Sasa kabla hatujaendelea, nitamke tu kwamba, baada ya maoni ya Upinzani kwisha, tutaanza na mchangiaji ambaye hajachangia toka *session* hii ya bajeti ianze, naye ni Mheshimiwa Joseph Mungai na wengine wajiandae.

Kwa hiyo, moja kwa moja ninamwita atakayetao maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naye ni Mheshimiwa Fatma Fereji. (*Makofii*)

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenezi Mungu, kwa kunijaalia uzima na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu na pia kwa uwezo wake na si mwengine, tunamshukuru kwa kutujaalia kukaribia kumaliza shughuli zetu za Bunge hili kwa amani na utulivu. Pili, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ambaye pia ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kutoa Maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa mwaka 2008/2009, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 96(7), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitakishukuru Chama Changu cha CUF, kwa kunitfea kuwa Mgomea kwa tiketi ya Chama hicho na ushirikiano kilioutoa kuhakikisha nashinda. Aidha, sitaweza kuwasahau Wananchi wa

Jimbo la Mji Mkongwe, kwa ushirikiano wanaonipa katika kazi zangu ndani na nje ya Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha imepanuliwa na kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi. Tume ya Mipango bado haijaundwa, kwa hiyo, kwa sasa Wizara ya Fedha inasimamia sera za fedha na sera ya mipango ya uchumi. Hivi sasa ni mwaka wa tatu wa kutekeleza MKUKUTA. Hata hivyo, kwa sababu ya kutokuwa na fedha za kutosha na gharama kubwa ya utekelezaji wa MKUKUTA, Mpango huu haujatekelezwa. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kushirikiana na vyama vyaa upinzani, taasisi zisizokuwa za kiserikali na wananchi kwa ujumla, kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo na MKUKUTA ili kuibua dira mpya ya maendeleo na mpango wa muda mrefu unaotekelzeza, utakaoongoza mipango na bajeti ya serikali. Ni vizuri kazi hii ikaanza mara moja. Aidha, tunatoa wito maalum kwa Rais kuunda Tume ya Mipango, isiyojikita katika hisia za kuunga mkono chama tawala; ikabidhiwe kazi hii ili nchi iwe na dira inayotokana na mjadala wa kitaifa wa maendeleo ya nchi yetu. Hatari iliyopo hivi sasa ni kwamba, Wizara ya Fedha na Uchumi itashughulikia matatizo ya kila siku ya bajeti bila kuwa makini katika maandalizi ya mipango mizuri ya muda wa kati na muda mrefu. Kama tulivyoona katika mjadala wa bajeti, kwa muda mrefu utekelezaji wa bajeti ya maendeleo umekuwa chini ya viwango vyaa bajeti

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, naomba nitoe pungezi kwa kazi nzuri inayofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na watumishi wake wote. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini bado kuna upungufu ambaao tulijaribu kuubainisha wakati Bunge lako lilipopitisha Sheria ya *CAG* ya mwaka 2008 na baadhi ya kasoro zinazosababisha Ofisi hiyo kukosa kile kinachotarajiwa toka kwa wananchi ni pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuwajibika kwa Bunge badala ya Rais, kama ilivyo sasa. Pia Ofisi ya *CAG* kuwa na bajeti inayojitegemea, pamoja na kuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza, ili kuwa inajitegemea kiutendaji badala ya kuwa chini ya Wizara ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri wa Fedha ya mwaka 2007/08, katika ukurasa wa 40 kifungu cha 57 kinaeleza kuwa, malengo ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka huo ni kuimarisha shughuli za ukaguzi. Ofisi inatarajia kufanya *Surprise Cash Audit* angalau mara nne kwa kila mwaka katika ofisi zote inazozikagua. Kambi ya Upinzani, inapongeza juhudhi za Serikali katika kuanzisha Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kambi ya Upinzani inakubaliana na wazo hili, kwani ni njia mojawapo ya kuweza kudhibiti wizi na matumizi mabaya ya fedha za umma katika Ofisi za Serikali. Kwa kuiunga mkono hoja hii, tunaitaka Serikali itupe ufanuzi wa kina juu ya utekelezwaji wa ukaguzi huu; ni ofisi ngapi husika mpaka sasa zimekaguliwa na ni maendeleo gani yamepatikana kutokana na mpango huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imejaribu kuweka wazi ni wapi Serikali inapoteza fedha nyingi kutokana na upungufu ambaao kwa njia moja ama nyingine umewaaagiza wahusika wautolee ufanuzi

wa kina. Kwa maono ya Mdhibiti, upotevu mkubwa unasababishwa na mambo makuu matatu ambayo ni kutokufuata Sheria za Manunuzi; usimamizi dhaifu wa fedha na mali; na kutotekeleza mapendekezo ya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu uliotajwa hapo juu, umelisababishia Taifa hasara ya kiasi cha shilingi bilioni 25. Hizi ni fedha nyingi sana, kwa kuangalia hali halisi ya uchumi wetu. Asilimia kubwa kati ya hiyo, unatokana na kutokuzingatia Kanuni na Sheria ya Manunuzi. Sambamba na hilo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kubadilisha vifungu nya sheria vinavyomzuia *CAG* kufanya ukaguzi kwa makampuni ambayo Serikali inamiliki hisa chini ya asilimia 50. Kambi ya Upinzani inauliza pale ambapo Serikali inamiliki hisa kidogo ni nani anaangalia kama kweli gawio linalotokana na hisa hizo ni sahihi na stahiki? Hii inatokana na ukweli kwamba, makampuni mengi yamekuwa yakidai kupata hasara wakati zinaendelea kuwekeza, jambo ambalo kwa hali ya kawaida ni uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inasisitiza tena kuwa, upungufu huu ambao moja kwa moja unawahuusu watendaji/wahasibu na kama Sheria ya *CAG* ya mwaka 2008 ingelikuwa imempa uwezo *CAG* ya kutoa adhabu kwa watendaji ni dhahiri upungufu anaoubainisha angeweza kuurekebisha tofauti na sasa. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani bado inasisitiza Ofisi hii ya *CAG* kupewa meno ili kupambana na masuala kama haya yanayofanywa na Watendaji Serikalini. Kambi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa, Serikali inatakiwa kuifanya Ofisi hii ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa taasisi huru na hivyo kutimiza majukumu yake kwa ufanisi, basi ni lazima kufanya mabadiliko ya vifungu vilivyotakiwa ndani ya Katiba ili kuruhusu uhuru huo wa Ofisi kama ilivyo kwa Mchi Wanachama wa *INTOSAI* na *AFROSAI-E*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu ya Tanzania ni chombo kinachomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa asilimia 100, chini ya Wizara ya Fedha. Benki hii ni chombo muhimu sana na ndio nguzo mama ya uchumi wetu kwa sababu ndio kitengo pekee chenye mamlaka ya kuangalia, kudhibiti na kuratibu uchumi wa nchi kwa kuratibu na kudhibiti mfumko wa bei na kulinda thamani ya fedha yetu. Benki Kuu ndio yenye jukumu la kusimamia uchumi na uimara wa Shilingi yetu. Thamani ya Shilingi ya Tanzania inawekwa kwa nguvu ya soko, kwa hiyo ni vyema Benki Kuu ilekeze zaidi nguvu zake katika kujenga soko imara, lenye uwezo wa kuweka thamani ya Shilingi inayoendana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uchumi wa nchi umekuwa ni mbaya kwa kulinganisha na kipindi chochote ambacho nchi yetu imekipitia. Hii ni dhahiri kwa kuangalia hali halisi ya maisha ya Watanzania ambapo hadi sasa mfumko wa bei umefikia asilimia 9.7 kwa kulinganisha na asilimia 6.1 mwezi Aprili, 2007. Kambi ya Upinzani ilitoa angalizo hili pale Serikali ilipopandisha bei ya bidhaa za mafuta, jambo lililosababisha upandaji wa bidhaa zote muhimu kwa matumizi ya kila siku ya Mtanzania. Bei za vyakula hasa unga, kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania kilo moja ya unga imefikia Sh. 1000 kwa Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofî*)

Pamoja na angalizo hilo, Serikali iliishia kutubeza, hatimaye kutumia zaidi ya milioni 172, sawa na kilo 172,000 za unga wa mahindi kwenda nchi nzima kuelezea Bajeti ya Serikali kana kwamba, wananchi hawakuisikia na kuilewa. Kila siku ukweli haukubali kukaa chini, ni vyema tujifunze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ina uhakika kabisa, mbali na kupandisha bei ya bidhaa za mafuta, lakini bado Serikali haina uwiano katika matumizi na mapato ya fedha zake kama ambavyo tunapitisha bajeti yake. Hii imewekwa wazi zaidi pale ambapo Mawaziri na Manaibu wao walizunguka nchi nzima kuitangaza bajeti.

Swali la kuuliza ni je, bajeti yao ya kufanya ziara hizo ilitengwa kwenye bajeti gani? Jambo hili lilisababisha nakisi katika matumizi ya Serikali na kupelekea kukopa pesa kutoka nje (*foreign sources*), kiasi cha 100.4 bilioni na kupunguza akiba yake katika mabenki kwa 37.3 bilioni (*BoT Monthly Report March, 2008*). Hiki ni kichocheo kikubwa cha kuongezeka kwa mfumko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika kitabu hicho hicho cha mwaka 2005/06, ripoti inaonyesha kwamba, benki ilipata faida ya kiasi cha shilingi bilioni 210.076, lakini gawio kwa Serikali lilikuwa ni kiasi cha shilingi bilioni 37.110.

Mheshimiwa Mwenyekiti, BoT ni chombo muhimu sana kwa Taifa hili maskini, ambapo mapato ya Benki hii kwa kiasi kikubwa yanatokana na biashara inayofanywa baina ya chombo hiki na Serikali yenye. Katika hotuba yangu ya mwaka jana, niliulizia juu ya vigezo vinavyotumika katika gawio la faida (*net profit*), inayopatikana kutokana na biashara hiyo, kwani katika Ripoti ya BoT ya mwaka 2004/05, inaonyesha kwamba, benki hii ilipata faida kiasi cha shilingi bilioni 127.5, lakini cha kushangaza zaidi ni kwamba, Serikali ilipata kiasi cha shilingi bilioni 5.0 ambacho ni sawa na asilimia 3.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi haya mabovu ya Serikali, ambayo kwa kila siku tumekuwa tukiyapigia kelele, yamethibitishwa pia na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kuwa, yameongezeka kutoka shilingi bilioni 844, ambayo ni sawa na 21% mwaka 2005/06 hadi shilingi trilioni 1.098, ambayo ni sawa na 30% mwaka 2006/07. Hali halisi ni kuwa, kada ambayo inanufaika na matumizi hayo ni kada ya viongozi walio Serikalini. Ushahidi wa hayo ni kuendelea kukopwa kwa walimu na kutokulipwa wafanyakazi viwango vipyta vya mishahara na wazabuni mbalimbali kutokulipwa, pamoja na kwamba, Serikali bado inatumia *Cash Budget*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kusikitisha na ya kutia huzuni zaidi, katika hesabu za BoT mwaka 2006/07, kunaonekana kwamba, kuna ujisadi mwingine wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 4.7 ulibainika. Hii inaonyesha dhahiri kwamba, bado mizizi ya ujisadi haijifikia na kuna haja ya kuchukua hatua madhubuti zaidi kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Bunge kilichofanyika mwaka jana, Kambi ya Upinzani iliishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha, juu ya kuundwa kwa

Tume itakayochunguza ujenzi wa majengo ya BoT (*twin tower*). Jambo la kusikitisha, ushauri huu ulikataliwa kwa sababu zisizojulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Benki Kuu uliofanywa mwaka 2006/07, imebainisha matumizi ya Shilingi milioni 551 kwa ajili ya kununua picha zenyenye sura ya Marehemu Daudi Ballali kwa ajili ya kutundikwa katika jengo jipya la ghorofa pacha (BoT *Twin Tower*) na majengo mengine yenye Ofisi za Benki Kuu. Uchunguzi unaonyesha kwamba, picha hizi zote zilikuwa na ukubwa sawa na hazikuwa na tofauti yoyote na zile picha zilizonunuliwa kwa kiasi cha Shilingi milioni 4.76 kwa kila moja. Vile vile Ripoti inaeleza kwamba ni picha 43 tu zilizo katika Hifadhi ya Benki Kuu ndizo zilizolipiwa na Benki Kuu kwa kampuni iliyotengeneza picha hizo ambayo ni *Zahr Ramj of Mediapix International*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika huu ndio uharibifu na ufisadi wa fedha za walipa kodi, zinazotumika bila ya kuzingatia mambo ya msingi yenye kuleta faida katika kunyanya na kukuza uchumi wa taifa hili. Fedha iliyotumika katika kutengeneza picha hizi, ingelitosha kabisa kama ingelitumika katika ujenzi wa vituo vya afya vya kisasa vipatavyo saba, kwani kila kituo kimoja kinagharimu kiasi cha Sh. 80 milioni. Kutokona na ubadhirifu huu wa fedha na ufisadi uliokithiri ndani ya taasisi hii, Kambi ya Upinzani inapata wasiwasi kama kweli malengo ya Benki Kuu ya kuondoa umaskini yatafikiwa ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inajuliza kama picha za kuweka BoT zimetumia fedha hizo; je, picha za Mheshimiwa Rais, ambazo zipo kwenye ofisi zote za Serikali Tanzania nzima; zimetumia kiasi gani? Tunamtaka Mheshimiwa Waziri, atupe gharama halisi za picha za Mheshimiwa Rais ambazo zimesambaa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokona na takwimu zilizomo ndani ya Taarifa ya Mkaguzi na Mdhhibitii Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni kwamba, hadi sasa Tanzania inadaiwa Sh. 1,832,420,666,865 kama deni la ndani na Sh. 3,642,581,417,898 kama deni la nje. Kati ya deni hilo, likigawanywa kwa idadi ya Watanzania milioni 40 ; kila mmoja atakuwa anadaiwa Sh. 4 5,810.51 katika deni la ndani na Sh. 91,064.54 katika deni la nje. Hivyo basi, hadi sasa kila Mtanzania anadaiwa jumla ya Sh. 136,875.05.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunatumia *Cash Budget*; kwa nini tunadaiwa madeni ya ndani? Ukweli ni kuwa, kila huduma ya ndani tayari inatakiwa fedha zake ziwe tayari kwenye bajeti. Tukitumia maana yake fedha zipo, deni linatoka wapi? Swali hili linahitaji majibu ya kina ; vinginevyo, Bunge hili lielezwe faida hasa ya *Cash Budget*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyobaini Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, hakika ubadhirifu wa fedha katika mashirika na taasisi mbalimbali za Serikali, umekithiri nchini na tatizo hili kwa kiasi kikubwa, linaongeza mzigo kwa Serikali na kudumaza maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Mkataba wa Ajira wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mamlaka ya Tumbaku (*TTB*), ulisainiwa tarehe 28 Julai, 2005 lakini ulirejeshwa nyuma na kusomeka tarehe 29 Aprili, 2005 kwa mshahara wa Sh. 2,700,000 kwa mwezi, ambao ni sawa na ubadhirifu wa Sh. 8,100,000. Kwa muda wa miezi mitatu na huu ni mfano wa taasisi moja tu, lakini kuna nyingi zaidi ya hii na hali hii inaonyesha jinsi gani taasisi zinavyoendeshwa nchini kwa ubabaishaji na ubadhirifu mkubwa ambao ndio unaochangia uchumi wetu kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika taarifa hiyo ya Mkaguzi wa Fedha, ilionyesha katika makubaliano ya malipo ya kodi ya kuendesha Mradi wa Songosongo kulikuwa na makubaliano ya kupunguzwa kodi kulingana na mauzo, lakini jambo la kushangaza na kusikitisha ; ukaguzi wa taarifa za Hesabu unaonyesha kiasi cha Sh. 1,887,186,871 kilipunguzwa kutoka katika mapato hayo ambayo yalitakiwa kuwasilishwa serikalini. Mkataba huu hauinufaishi serikali wala wananchi, zaidi ya yote unaongeza mzigo kwa serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na vitendo hivi vyta ubadhirifu wa fedha vinavyoendelea kufanywa na taasisi hizi nchini na mwanzo mzuri ulioonyeshwa na kitengo hiki cha ukaguzi wa fedha, ndiyo maana Kambi ya Upinzani tukashauri kwa nini Serikali isiwape mamlaka mbali ya kutafiti na kukagua, lakini pia kudhibiti ubadhirifu huu ili kuweza kuwapa onyo na kukomesha hali hii ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipengele cha ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, maduhuli ambayo yalikuwa hayajakusanya hadi tarehe 30 Juni, 2007 ni malipo ya Sh. 7,942,247,030 kutoka kwa wawekezaji kwa ajili ya ununuzi wa mashirika, yalikuwa bado hayajapokelewa ingawa hatua za uuzaaji zilikuwa zimeshakamilika. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atuelezee ; je, fedha hizi zimeshalipwa na kulikuwa na jambo gani lililosababisha hata kutolipwa malipo hayo kwa muda wa makubaliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kilichopita, Serikali kupitia Hazina, imetoa udhamini wa asilimia 100 kwa makampuni binafsi. Hili linafanyika kwa Serikali kuzaigiza asasi za fedha kutoa mikopo hiyo. Mbaya zaidi, baadhi ya makampuni hayo yanaonekana kushindwa kulipa na riba imezidi kuwa kubwa mno, mfano, *NSSF* wanakidai Kiwanda cha Sukari Kagera Sh. 100 bilioni, kutokana na dhamana ya Serikali. Baadhi ya Makampuni binafsi ambayo yamepata udhamini wa asilimia 100 toka Serikalini mbali na Kagera Sugar ni Kiwanda cha Maua cha Arusha, Kiwanda cha Nyama cha SAFII cha Sumbawanga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, pale ambapo Benki inatoa mkopo mkubwa kwa kampuni, kuna taratibu za makubaliano ambazo zinafanywa kuhusiana na uendeshaji wa kampuni ili benki iweze kurejesha fedha zake. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, imeweka mkakati gani wa makusudi, kuhakikisha viwanda hivyo vinarejesha fedha hizo? Tukumbuke hizi ni fedha za Watanzania walipa kodi na dhamana ni kwa viwanda binafsi; je, hii ni haki kwa walipa

kodi wa nchi hii kulipa madeni ya makampuni binafsi kwa kodi ya wananchi pale ambapo makampuni hayo yanaposhindwa kulipa madeni hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (*TRA*) ni ndicho chombo husika cha kukusanya mapato, ambacho kipo chini ya Wizara ya Fedha, kilichoanzishwa mwaka 1996. Ingawa kimuono wa juu juu, idara hii inaonekana kana kwamba, imefanikiwa kwa hali ya juu, lakini kwa undani kitengo hiki bado kabisa hakijafanya kazi hasa inayotakiwa na kama ingelifanya hivyo basi leo hii tungejitosheleza kwa bajeti yetu na wala tusengelihangaika na kuwategemea Wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkutano wa Bajeti uliopita, tulisema sana juu ya jambo hili la kutegemea wafadhili katika maendeleo yetu. Kambi ya Upinzani inaipongeza *TRA* kwa kukusanya mapato kwa kiwango maradufu kulingana na miaka iliyopita. Pia tulisema kuwa, uwezo wa Serikali kukusanya mapato ni mkubwa zaidi, ila kuna uzembe mkubwa na kutojali (*laxity*), ubadhirifu na ufisadi kama inavyodhihirishwa na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna makampuni mengi ambayo yapo na yanaendesha shughuli zake nchini na hata bila ya kulipa kodi au kwa kulipa kiwango kidogo sana kisichoendana kabisa na mapato yao; mfano nzuri ni makampuni yanayofanya biashara ya chai na katani Wilayani Korongwe Vijijini. Makampuni haya hayalipi ushuru wa asilimia tano, kiasi cha kuchangia kipato kidogo cha Hamashauri na hivyo kushindwa kabisa kuendeleza shughuli zake za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inapoteza mapato mengi sana na kama hali itaendelea hivi, basi licha ya kutegemea Wahisani kwa asilimia 34 kwa bajeti ya nchi, baada ya miaka mitano inayokuja, kuna uwezekano utegemezi kuongezeka kwa asilimia 100. Hii inatokana na makampuni mengi ambayo yanakwepa kulipa kodi inayosababishwa na mikataba feki na mibovu, ambayo moja kwa moja inaathiri Idara ya Mapato nchini na hivyo kuongeza wimbi la umaskini na uchumi tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika inaumiza na inasikitisha sana, leo hii Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, ilikuwa inaruhusu ukusanyaji wa kodi kwa Serikali za Mitaa kwa makampuni ya machimbo kiasi cha asilimia 0.3, lakini la kushangaza ni kuwepo kwa makubaliano ya kukusanya si zaidi ya US dola 200,000 kwa mwaka. Makubaliano hayo yanakataza kutoangalia mapato, faida, kiwango kinachopatikana cha fedha na kadhalika, hapa pana uwezekano mkubwa wa kupotea mapato kwa kisi kikubwa, kwani thamani ya sarafu inabadilika siku hadi siku; huwezi kuweka kiwango maalum cha fedha badala ya asilimia hii ni kuikosesha serikali mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004, inaitaka kampuni inayoenetsha shughuli zote za machimbo, kulipa kodi ya asilimia 30 kulingana na pato lake. Jambo la kusikitisha ni kuwa, zaidi ya miaka mitano sasa hakuna kampuni yoyote ya dhahabu iliyotangaza pato lake nchini na kufanya taasisi husika kushindwa kukusanya kodi hiyo kulingana na pato husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Alex Stewart (Assayers) ASA, inaonyesha kuwa, kitengo cha ukusanyaji mapato nchini kinapoteza fedha nyingi sana na hasa katika kampuni za madini. Hii inatokana na kitengo hiki kutokuwa na wafanyakazi wenye uwezo, taaluma, uzoefu na ujuzi wa kuchambua *financial statements* za makampuni ya madini. Pia imechunguzwa na kuthibitika kuwa, kitengo hiki kina uwezo mdogo mno wa kugundua na kuona kwa macho ya kitaalamu, jinsi gani makampuni ya madini yanavyoendeshwa nchini. Mfano mzuri, imegundulika kuwa, makampuni mengi ya madini nchini hayatoi taarifa sahihi za rekodi ya fedha, ambayo ni kinyume kabisa na kifungu cha 99(3) na *paragraph* ya 2(iii) ya Mining Act ya 1998, ambayo inayalazimisha makampuni haya kurekodi na kutunza mahesabu kwa mpangilio ulio wazi na unaoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (*CAG*), katika Wizara na Idara za Serikali tulizochambua, mathalani tumbaini kuna upungufu wa makusanyo ya mapato, mrabaha usiokusanywa kutoka makampuni ya almasi ya Williamson Diamond Ltd ni Shilingi 841,137,251 na Tansort Sh. 206,662,556. Aidha, misamaha ya kodi nayo imekuwa ya kutisha, kwani hadi kufikia mwezi huu wa Juni, 2008, kiasi cha Sh. 819.9 bilioni zilikuwa zimesamehewa kama kodi, huku misamaha hii mingi ukiondoa ya mashirika ya dini ikiwa haijamnufaisha mwananchi maskini. Hiki ni kiasi kikubwa kwa nchi inayoomba misaada kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ya madini yamesamehewa kodi kwa asilimia 100 katika uingizwaji wa mafuta kutoka nje kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao. Kwa mfano, katika mwezi Aprili, 2007 ilielezwa kwamba, kuanzia mwaka 2004 mpaka 2006, makampuni sita ya migodi ya dhahabu yameingiza zaidi ya lita milioni 178 za mafuta ghafi, ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 62.8 kilikosekana kutokana na kuondoa kodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile makampuni haya yamepata punguzo la asilimia 100 kwenye ushuru wa bandari (*Custom Duty*). Mwanzoni makampuni haya yalikuwa yanalipa kiasi cha asilimia tano, lakini kwa sasa hakuna ushuru wowote unaotozwa kwa makampuni haya. Kambi ya Upinzani inaona huu ni upungufu mkubwa wa mapato ya wanyonge wa Watanzania kwa kuyatupa bila utaratibu wa wazi na unaoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile sheria hizi zimeyapa madaraka makubwa makampuni haya kwa kumiliki haki za madini, kiasi ambacho wana nguvu kamili ya kufanya wanavyotaka; kwa mfano, wamepewa uwezo wa kununua na kuuza makampuni haya kwa makampuni mengine ambapo shughuli hizi zinayapatia makampuni faida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2003, kampuni kutoka Australia inayojulikana kwa jina la *East Africa Gold Mines*, ilipata kiasi cha US\$ milioni 252 kwa kuuza mgodi mmoja wa dhahabu ndani ya Tanzania kwa Kampuni ya *Canada Placer Dome*, ambayo baadae iliuzwa kwa *Barrick*. Vile vile katika mwaka 1999, Barrick

ilinunua mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu kutoka Kampuni ya *Canada Sutton Resources* kiasi cha dola za kimarekani milioni 280.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kustaajabisha ni kwamba, katika mauzo yote yanayofanyika na makampuni haya si Serikali ya Tanzania wala raia wa kawaida wa nchi hii, ambaye ananufaika na mabilioni ya fedha hizi. Hii ni dhahiri kuwa, Serikali yetu haina uchungu na mali zetu, kwani tunaamini yanayotokea wanayatambua lakini kwa sababu ya kuzingatia maslahi ya wachache, ndio maana leo hii wanatufikisha hapa. Je, huku ni kuwavutia au kuwahonga mali zetu wawekezaji hawa? Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge hili, Taifa letu limefaidika kwa kiasi gani na mauzo haya na fedha hizo ziliingia kasma ipi kama zipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukusanyaji huu mbovu wa mapato, makisio yaliyofanywa juu ya upotevu wa mapato yanayotokana na *Royalty Rate* (kiwango cha mrabaha), *Corporation Tax* (Kodi ya Makampuni) isiyolipwa na ukwepajji wa ulipaji kodi kwa muda wa miaka saba sasa ni zaidi ya Shilingi bilioni 480. Kiasi hiki cha fedha hakijajumuisha makampuni yote ya madini wala pungozo la kodi nyinginezo ambapo ni vigumu kuweza kukisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho makubwa yaliyofanywa kwenye sheria za kodi, lakini inaonyesha dhahiri kuwa, marekebisho haya yametoa kipaumbele zaidi kwa wawekezaji kutoka nje na kuwakandamiza wazalendo wa nchi hii. Hii inaonyesha dhahiri kuwa, viongozi wetu hawana uchungu na wananchi wao wala hawatambui umuhimu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na ukwepajji huo, kuna aina nyingine ya ukwepajji inayofanywa na wafanyakazi wa kigeni, walioajiriwa katika makampuni mbalimbali. Ukwepajji huu wa kodi ni ule unataka kutokulipa kodi ya *PAYE*. Kwa sasa tunakadiria kuna wafanyakazi hao karibu 500 nchi nzima na wengi wao wanapokea kati ya shilingi milioni tano na ishirini, tuchukulie wastani wa shilingi milioni kumi. Hivyo basi, *PAYE* kwa mwezi mmoja shilingi bilioni 1.5, ambazo kwa mwaka mmoja ni shilingi bilioni 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, sheria za kodi zinasemaje kuhusiana na wafanyakazi hao wageni kulipwa mishahara yao moja kwa moja kwenye nchi wanazotoka na kulifanya Taifa kukosa takriban kiasi tajwa hapo juu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 73A cha Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli, kinatoa msamaha kwa wafanyabiashara wakubwa kwa kusema Sheria ya Hotels Act, Cap 105, Re 2002, inatoa msamaha wa kutolipa kodi ya ushuru wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mtu yejote au Jumuia yoyote ya watu ambao wamesajiliwa chini ya sehemu ya (iv) ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kuanzia siku ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msamaha huu ni sawa na kuwapa nafasi wafanyabiashara hawa kutolipa kodi ambayo kimsingi kila mtu anayeuzza bidhaa na kutoa huduma zinazopaswa kulipwa kodi hii, analazimika kuilipa kwa mujibu wa kifungu cha 3(1) na 4(1) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1998.

Kwa kuwa wamesajiliwa; je, hiyo inahakikishaje kwamba wafanyabiashara hawa watalipa kodi ya ongezeko la thamani inayohusu huduma za hoteli wanazozitoa au wafanyabiashara hawa hawapaswi kulipwa kodi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya ushuru wa hoteli ya asilimia 20 inayotakiwa kulipwa chini ya kifungu cha 26(1), imekuwa kero kubwa hasa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo katika sehemu tofauti za miji, majiji, manispaa na nyinginezo. Hii ni kwa sababu kiwango cha asilimia 20 ni kikubwa na hakizingatii gharama za uendeshaji kwa biashara hiyo. Mfano, tarehe 10 Januari, 2008, Umoja wa Wafanyabiashara wa Nyumba za Kulala Wageni Mwanza (UWANZA) ulimwandikia barua Waziri wa Fedha, yenye Kumbukumbu Namba UW/MZ/06, wakilalamikia kodi hii na manyanyaso wanayoyapata kwa sababu ya kodi hii. Malalamiko haya yalijibowi kwa barua yenye kumbukumbu namba TYC/R/160/32 ya Waziri wa Fedha kwamba, atalishughulikia jambo hili lakini hadi leo hii halijashughulilikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia jambo hili kwa makini na kuchukua hatua zinazofaa ili kupunguza usumbufu kwa wafanyabiashara hawa. Aidha, kifungu hiki cha sheria kinawaondoa Watanzania wenye mitaji midogo katika biashara na kuwapa fursa wafanyabiashara wakubwa kuendelea kwenye biashara hii; dhana ya ushindani iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ya Fedha ndio Sekta muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi kwa ujumla wake, kwani ndio inayotakiwa kuwa chachu ya Sekta nyingine za Uchumi kwa kuziwezesha kimtaji. Kwa hali ya kawaida, mabenki ndio yanayotakiwa pamoja na kutoa mikopo, pia yatoe ushauri na kusimamia mkopaji hadi aweze kusimama na kuwa mshindani katika biashara. Katika mchakato huo wote, benki itapata riba yake na mkopaji atapata kile alichokusudia kukifanya.

Mwishiuni mwa Desemba, 2007 wastani wa riba za amana za akiba ilikuwa asilimia 2.75, wakati mfumko wa bei ni asilimia 9.7. Mtanzania mlala hoi aliyejikusuru na kuweka akiba ya shilingi 10000 tarehe 31 Desemba, 2007, thamani halisi ya akiba yake itapungua kwa asiliamia saba, sawa na shilingi 700 ifikapo tarehe 31 Desemba, 2008. Mfumo mzima wa mabenki na taasisi zetu za fedha, hazitoi motisha na msukumo katika kukusanya akiba ya Watanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa riba ya mikopo ni asilimaia 15.25. Tofauti kati ya riba ya mikopo na riba ya amana za akiba ni asilimia 12.5. Ni wazi mfumo wetu wa fedha ni dhaifu katika kukusanya amana za akiba na unatoza riba kubwa kwa wanaokopa. Makampuni madogo na ya kati hayapati mikopo. Makampuni na wafanyabiashara 200 - 250 ndio wanaochukua zaidi ya asilimia 80 ya mikopo yote inayotolewa na mabenki ya Tanzania. Sekta ya Kilimo ndiyo inayonyimwa mikopo

kabisa. Hatuwezi kujenga uchumi wa kisasa ikiwa wajasiriamali wadogo na wakati hawana vianzio vya mitaji na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti umeonyesha kuwa, upatikanaji wa huduma za benki na fedha (*financial services*), kama vile kuweka akiba, kukopa, kununu bima na kulipia bidhaa na huduma bila kutumia fedha taslimu ni muhimu katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, imeongeza fursa za kusambaza huduma za fedha, kwa mfano, kwa kutumia simu za mkononi. Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kushirikiana na Benki Kuu, iandae mkakati wa kuwapatia wananchi wote huduma za fedha (*financial services for all*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pamoja na hilo, taratibu za mikopo na zenyewe zinakatisha tamaa sana, pale mkopaji anapotakiwa kuweka dhamana ya mikopo yenye thamani ya 125% ya mikopo anaotaka kukopa. Ili sekta ya fedha iweze kuchangia katika uchumi wetu ni lazima masuala yafuatayo yaamuliwe:-

(a) Suala la riba liamuliwe kama lilivyoamuliwa Kenya (*Central Bank Intervention*).

(b) Benki kuu ipunguze kiwango cha riba kwa mikopo yake inayoitaoa kwa mabenki ili mabenki nayo yapunguze riba kwa wateja.

(c) Serikali ilete sheria mahususi ya utumiaji wa mtandao katika malipo na manunuzi ya Benki, ili kurahisisha na kuharakisha ulipanaji wa fedha, ikiwa ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi.

(d) Pamoja na maelezo yanayotolewa na Serikali juu ya *Dollarisation*, Serikali itoe tamko rasmi kwamba ni makosa kutumia *Dollar* katika biashara ambayo haikuidhinishwa na BoT kutumia fedha za kigeni.

(e) Benki Kuu ifuatilie kwa makini fedha zinazotoka nje kwa matumizi ya Serikali na ziwekwe Benki Kuu na Benki za Biashara. Serikali ilieleze Bunge ni kiasi gani cha riba kimelipwa kwa mabenki hayo katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji walazimishwe kukopa katika mabenki yetu na kama mabenki yetu hayana fedha za kutosha, Benki Kuu iingilie kati kusaidia kupatikana kwa mikopo hiyo, ili tuepukane na kuwa na mzunguko mdogo wa fedha na akiba yetu kuwa ndogo. Aidha, tutaweza kudhibiti mserereko wa fedha yetu. Kwa njia hii, Taifa litawenza pia kusimamia mwenendo mzima wa uwekezaji katika nchi yetu, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kusimamia viwango vya uwekezaji, yaani *plough back effects*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeiongezea mtaji Benki ya Rasilimali (*TIB*) na kufikia shilingi bilioni 50 ili kupunguza ukosefu wa mikopo katika viwanda na kilimo. Ukizingatia yaliyotokea katika akauti ya *EPA* ya Benki Kuu, taasisi ambayo ndiyo inayosimamia mabenki; serikali inaweka mfumo gani wa kiutawala kuhakikisha kuwa,

Benki ya Rasilimali haitoi mikopo kisiasa na fedha za walipa kodi zilizowekwa kama mtaji katika benki hiyo hazipotei. Utawala (*Governance*) ya Benki ya rasilimali unahitaji kuimashwa, ikiwa ni pamoja na kuteua watendaji makini wenye utaalami wa hali ya juu. Bodi ya Wakurugenzi iteuliwe bila kuzingatia hisia za kichama na iwe na mamlaka ya kusimamia Watendaji wa Benki hii ili isitoe mikopo kisiasa au kifisadi bila kuzingatia kanuni na uwezo wa wakopeshwaji kufanya shughuli za kiuchumi kwa ufanisi na kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na bajeti nzuri na inatakayoweza kuondoa kero na matatizo kwa wananchi, takwimu sahihi ni muhimu sana. Serikali imeshindwa kuwa na takwimu muhimu na sahihi katika upangaji wa vipaumbele vyake na vipaumbele vinapangwa kwa kuelewa ni watu wangapi wanatarajiwa kutumia huduma husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala wa usajili, ufilisi na udhamini (RITA) ni taasisi pekee na ya uhakika ambayo ina uwezo wa kutoa takwimu sahihi ambazo zinaweza kutumiwa katika shughuli za mipango ya maendeleo iwe ni kwa Nchi, Mikoa, Wilaya hadi Kata. Aidha, Wakala huyu anaweza kwa kiasi kikubwa, kupunguza mwingiliano wa shughuli zinazofanana kama zinavyofanywa na taasisi mbalimbali katika Wizara mbalimbali mfano, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Usajili wa Makampuni, Bodi ya Mikopo, Vitambulisho vya Taifa vya Uraia, Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (*TIN Number*), Leseni za Udereva, *Pay Roll* za watumishi wa Serikali na Msajili wa hati; sehemu hizo zote takwimu sahihi zinaweza kupatikana kutoka kwa wakala huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mlolongo wa asasi za serikali zinazofanya kazi zinazofanana ni kuiongezea Serikali matumizi yasiyokuwa ya lazima. Wakala wa Vitambulisho vya Uraia (*NIDA*), ili kufanya kazi zake ni lazima apate takwimu kutoka RITA. Kambi ya Upinzani inauliza; kwa nini uundwe wakala mwingine wakati kuna wakala anayefanya kazi hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Hazina wa Serikali, ambao upo chini ya Wizara ya Fedha, ndio wenye jukumu la kutoa fedha kwa Wizara zote, baada ya Bunge kuitisha matumizi ya fedha kwa Wizara husika. Kwa hiyo, kama Wizara imepanga kuendeleza na kutekeleza miradi yake ya maendeleo kama vile ujenzi wa shule, barabara, zahanati na kadhalika, hawawezi kuifanikisha miradi hiyo kama Mfuko wa Hazina haujatoa fedha hizo. Hii inaonyesha ni jinsi gani Mfuko huu ulivyo muhimu kwa maendeleo ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kushangaza, tunaona kwamba, karibu Wizara zote wanapoulizwa kwa nini Wizara imeshindwa kukamilisha miradi iliyopanga kutekeleza kwa muda ulioainishwa; cha kusikitisha majibu yanayotoka ni kwamba, kutohana na kucheleweshwa au kupewa nusu nusu kwa fedha kutoka Mfuko wa Hazina wa Serikali. Maelezo kuwa fedha zilichelewa kutoka kwa wahisani na ishara tu ya kutokuwa na mipango makini na hivyo siyo sababu inayokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, huu ni uzembe wa makusudi, unaofanywa na wahusika wa kitengo hiki; hivyo ni lazima Waziri atupe

maelezo ya kina na yenye kuridhisha; kwa sababu gani imekuwa ni kawaida kwa ofisi hii kuchelewesha fedha hizi na hivyo hawaoni kuwa Serikali ndio wanakwamisha shughuli za maendeleo na hivyo kushindwa kufikia malengo waliyopanga ya kuondosha umaskini na kukuza uchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Fereji, kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani vizuri. Kama nilivyosema mwanzo ni kwamba, kwa ujumla nina wachangiaji 14, tutakwenda na wale amba muda wetu utaturuhusu. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Joseph James Mungai, atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa. Mheshimiwa Mungai karibu.

MHE. JOSEPH J. MUNGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi na bila kuchelewa napenda kutamka kwamba, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Napenda pia nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mwanasheria msomi Mheshimiwa Mizengo Kayanza P. Pinda, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Hongera sana.

Pia nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote wa Serikali walioteuliwa katika Serikali ya sasa, pamoja na Naibu Mawaziri. Nawatakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara hii, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuiunda upya au kuipa jina jipya kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi na kuondokana na kuwa na Wizara ya Mipango. Mimi naamini kabisa, hali ya uchumi wa sasa inahitaji kuwa na Wizara inayosimamia kwa pamoja mambo ya fedha na uchumi kwa ujumla. Kuwa na Wizara ya Mipango mahali tofauti ni mfumo wa uchumi wa dola, lakini Tanzania ya leo ni ya uchumi wa soko na wengine huuita uchumi wa soko huria, lakini mimi naona jina sahihi ni uchumi wa soko. Tumeondoka na uchumi wa Mashirika ya Umma. Uchumi wa Soko huendeshwa na wanasoko wenywewe, haihitaji kuwa na Wizara ya Mipango, inatosha tu kuwa na Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, Wizara hii mpya ya Fedha na Uchumi, inahitaji kujipanga upya katika majukumu yake hayo, isibakie *business as usual*, mambo yasiwe kama yalivyokuwa. Uchumi wa Soko Huria ni wa kasi kubwa, unakwenda kwa *speed* kubwa na ni muhimu Serikali nayo katika kusimamia na kuelekeza iwe ni kwa kasi. Ni uchumi wa ushindani, unahitaji kuwa *regulated*, ile *role* ama fursa ya Serikali ku-*regulate* uchumi lazima nayo ifanywe kwa makini.

Uchumi unahitaji uelekezwe kwa vivutio sahihi; vivutio sahihi kwa mfano Sera sahihi ya kodi, kuwa na Sera sahihi ya kodi ambayo inavutia uwekezaji kwenye maeneo muhimu hasa maeneo kule ambako umaskini umekithiri. Kuwa na Sera sahihi ya kodi

katika nchi kama yetu inayovutia uwekezaji katika kilimo huko vijiji kwa vivutio vya kodi. Jambo hili ni muhimu lipewe *emphasi*, na *emphasis* iwe katika *taxation policy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono hoja hii, naomba nichukue nafasi hii kutoa ushauri katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, nashauri Wizara iongeze kasi ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma yaliyobakia. Tulisikiliza asubuhi hii Mheshimiwa Waziri wakati akijibu swali namba 455 akiliambia Bunge hili kuwa, yamebaki mashirika 37. Mimi najaribu kuangalia katika *record* ya utekelezaji wa ubinafsishaji katika maisha ya Bunge hili la 2005 – 2010 ni kampuni moja tu, yaani Twiga Cement au Tanzania Portland Cement, ndiyo imefanyiwa ubinafsishaji. Mheshimiwa Rais, ametukumbusha kwamba, tupo nusu ya kipindi na hili Shirika la NMB ambalo linabinafsishwa sasa litakuwa la pili. Tukienda kwa *speed* hii ya Mashirika mawili katika miaka miwili na nusu hatutamaliza. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, atuambie tatizo liko wapi; kwa nini *speed* ya ubinafsishaji inakuwa ndogo?

Kwa mfano, yapo makampuni ambayo yapo tayari kwa mfano, *National Bank of Commerce (NBC)*, ubinafsishaji wake hautekelezwi na hali yake ya kifaida ni nzuri na imekuwa nzuri kwa miaka mingi?

Jambo la pili, nashauri Wizara ichukue hatua za dhati kuimarisha Soko la Hisa la Dar es Salaam, inafaa itengenezwe ratiba maalum itakayohakikisha kwamba, hayo makampuni 37 ambayo hayajabinafsishwa, yanabinafsishwa katika kipindi kilichobakia cha Bunge hili, yaani ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia mojawapo ya kulisaidia Soko la Hisa la Dar es Salaam ni kuhakikisha kwamba, wakati wa ubinafsishaji hisa nydingi zinapelekwa sokoni. Kusiwe na kigugumizi katika kubinafsisha. Kwa mfano, katika ubinafsishaji unaoendelea wa *NMB*, mimi nashangaa kwa nini ni 21%? Kwa nini haibinafsishwi 42% na Serikali ikabakiwa na asilimia 9%? Hatua kama hizo zitakuwa za kuli-*support* Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Eneo la tatu, katika ubinafsishwaji wa *NMB* unaoendelea, nashauri Mheshimiwa Waziri azingatie maamuzi ya Bunge hili kupitia Sheria Namba 23 ya mwaka 2003, iliyopewa Kibali cha Rais Benjamin William Mkapa tarehe 30 Juni, 2003. Katika Sheria hiyo, Bunge lilielekeza kuwa 21% ya hisa wauziwe *Citizens of Tanzania*, yaani Raia wa Tanzania au Mashirika yenye maslahi ya Watanzania au Makampuni yanayomilikiwa na Watanzania kwa 100%. Kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa na ushauri uliotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Mipango kuwa, ile 5% wanayopangiwa wafanyakazi wa *NMB* ni afadhali itokane na zile 30% za Serikali ili Serikali ibakiwe na 25%. Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa haivunji Sheria ya Bunge, bali itakuwa inatekeleza kama Bunge lilivyoelekeza kwenye Sheria hiyo niliyoinukuu. Kwa hiyo, nashauri kabisa, kama pendekexo la nne kwamba, 5% ya wafanyakazi zitokane na ile 30%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema hivi si kwamba napinga wafanyakazi wa *NMB* kuuziwa 5%, mimi napenda niipongeze Serikali na Wafanyakazi wa *NMB* kufikia muafaka kwamba, wafanyakazi wauziwe hiyo 5%. Ushauri ni kwamba, itoke kwenye zile 30% za Serikali. (*Makofi*)

Pia ningependa kuchukua nafasi hii, kushauri kwamba, siyo sahihi kuendelea kuwauzia mwaka mzima ni afadhali Serikali iwatafutie mkopo zinunuliwe mara moja, kwa sababu kuendelea kuuza mwaka mzima kutaathiri bei ya hisa za *NMB* katika Soko la Hisa, kutaleta *price distortion* kwa sababu kila wakati zitakuwa zinajulikana zipo nyingine ambazo zinaendelea kununuliwa kwa shilingi 600, jambo ambalo si sahihi hata kidogo. Nashauri Mheshimiwa Waziri, hili nalo alitazame upya.

Jambo la tano ni kuhusu utekelezaji wa bajeti. Nashauri suala la *cash budget* au mkakati wa *cash budget* utazamwe upya. Kunakuwa na shida sana huko Mikoani kuanza utekelezaji wa mipango, kwa sababu fedha zinachelewa. Mimi nashauri Waziri wa Fedha, atumie madaraka aliyonayo katika sheria ya kuweza kukopa kutoka mahali popote ili fedha za bajeti zitoke mwezi wa Saba mara baada ya kupitishwa na Bunge, halafu katika kipindi cha mwaka zinapokusanywa, zirudishwe kule ambako Mheshimiwa Waziri amekopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la sita, napenda kuchukua nafasi hii kupongeza sana ongezeko la kujitegemea lililo katika bajeti ya mwaka huu. Naipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo waliyochukua, lakin ningependa kunukuu maneno ya Kiingereza yanayosema kama ifuatavyo: “*Take care of pennies, pounds will take care of themselves.*” Pia kuna mengine yanayosema usiwe *penny wise and pound foolish*. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri, atafute *balance* ya hayo mawili kwa mfano, kule kwetu msitu wa Sao Hill mara baada ya kupandisha bei mara saba wananchi wapasua mbao wanashindwa kuununua

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemueleza Mheshimiwa Rais alipotutembelea katika Wilaya yetu ameahidi kwamba, ataielekeza Wizara husika kulitazama jambo hili upya. Nashauri Wizara hii ya Fedha na Uchumi nayo itoe mchango wake. Ni afadhali kupunguza bei ya msitu ukavunwa zaidi mara nne au tano zaidi kwa sababu mapato ya Serikali yanaweza kuongezeka zaidi ya mara difu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia tuepukane na matumizi yasiyo muhimu, kwa mfano, katika bajeti ya mwaka huu yamepangwa mamilioni ya fedha kuiwezesha Serikali kuendesha mjadala wa kitaifa utakaoshirikisha wadau mbalimbali kuhusu Makao Makuu kuhamia Dodoma kwa lengo la kutunga sheria. Nimeshangazwa kwamba, tunataka kutumia fedha nyingi namna hiyo katika jambo hili

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikumbushe kwamba, jambo hili lilikwishafanyiwa kazi mwaka 1974. Mikoa yote ililizwa na tulipiga kura katika vikao vya Chama na wakati ule ulikuwa ni mfumo wa Chama kimoja tukatoa maoni. Nakumbuka kabisa kuna Mikoa iliyosema hakuna kuhamia Dodoma: Mikoa yote ya Zanzibar ilisema hapana, Mkoa wa Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Tanga ilisema

hapana. Mikoa ya Magharibi walisema tuhamie, tukafikia uamuzi; sasa tena tunataka kuulizana juu ya jambo hili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumeiona hali halisi, miaka thelathini na tano tumeshindwa kutekeleza jambo hili; lakini pia tumeona hali halisi, Chuo Kikuu cha Dodoma kinajengwa na kinajengwa katika eneo ambalo lilikuwa limepangangiwa Makao Makuu. Kwa hiyo, Mradi huu ni kama umekwishajibomoa wenyewe, tusitumie mamilioni ya fedha kuulizana kuhusu jambo hili. Nadhani kama ni kuulizana, itafutwe njia ya mkato isiyotumia fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikumbushe kwamba, jambo hili pia limewahi kuletwa hata katika Bunge miaka ya 60, Marehemu Mheshimiwa Joseph Nyerere alileta hoja binafsi kwamba, Makao Makuu yahamie Dodoma, ukawa mjadala Bungeni, Waziri wa Fedha wa wakati huo akatishia kujiuzulu Sir Ernest Varsey, lakini baadaye mleta hoja akaondoa hoja. Sidhani kama kuna haja ya kulileta tena jambo hili; jambo hili lifanyiwe kazi. Tufanye kilicho sahihi. Bajeti yetu haina uwezo wa kufanya jambo hili, imeshindikana miaka thelathini na tano, kama tunataka kuulizana lakini tusitumie mamilioni mengi ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii pia, kuwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, kwa fursa wanayoendelea kunipa kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kumalizia kwa kusema, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na nawatakia kila la kheri katika utekelezaji. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Mungai, kwa mchango wako, lakini niseme tu kwamba, tupo waumini wa kuhamia Dodoma; inawezekana. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuiweka hoja yake kwa makini, pamoja na kwamba kwa mujibu wa kanuni zilivyo, muda haujamtendea haki lakini nampongeza sana. Pia napenda kuipongeza Serikali, kama walivyotangulia kusema wenzangu, kwa kuanzisha Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006, katika Bunge lako Tukufu, tulitembelewa na Waziri Mkuu mwanamke wa Ireland, ambayo haina matatizo. Katika hotuba yake alisema kwamba, miaka ya 70 urchumi wa Ireland ulikuwa kama Tanzania, lakini sasa hivi urchumi wa nchi hiyo ni katika zile chumi ambazo zinaongoza Ulaya. Alisema siri kubwa ni kwamba, waliunda Tume ya Mipango, wakawachukua wasomi mtambuka wakawaambia waiambie nchi ifanye nini na baada ya hapo wakafuata ushauri wa wasomi hao na sasa hivi ni nchi ambayo ina urchumi unaongoza Duniani na Ulaya. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha Tume ya Mipango, naomba sana Mheshimiwa

Waziri, ikiwa kamili Tume hiyo iwe mtambuka ili wawaweke wasomi, pamoja na wachumi waingie na waweze kuitendea haki nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nikisimama nitakuwa naongelea manunuzi tu, nimeamua hoja yangu iwe ya manunuzi. Wakati nikichangia katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, mwezi wa sita, nilisema katika bajeti nzima ya trillioni zote ambazo alizitaja Mheshimiwa Waziri, asilimia sabini ya matumizi ya kawaida na asilimia themanini au asilimia mia ya matumizi ya maendeleo ni manunuzi. Sasa manunuzi yasipoangaliwa, ina maana fedha zote zitakuwa zinakwenda chini ambako kuna panya buku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutambua manunuzi kwamba, ni kitu muhimu, hapo awali ilikuwa Wizara mbili au tatu zinashughulikia manunuzi. Ilikuwa Wizara ya miundombinu, kuna kitengo cha manunuzi, kuna bohari halafu Wizara ya Fedha kuna taasisi ya kudhibiti manunuzi na taasisi ya rufaa. Kwa hiyo, haikuwa Wizara moja, mradi Serikali imeamua kwamba, manunuzi sasa yahamie Wizara ya Fedha, ambayo ni Wizara moja, naipongeza sana Serikali.

Naomba baada ya kuamua uamuzi huo ikamilishe uhamisho, kitengo kizima cha manunuzi kiwe kwa Waziri wa Fedha, sio kama ilivyo sasa, kwenye Wizara ya Miundombinu kuna bohari hii inashughulikia manunuzi na kuna *NBMM* inashughulikia manunuzi. Kwa hiyo, naomba vyote hivi avihamishe ili akamilishe kufanya manunuzi kuwa katika Wizara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapo Wizarani aimarishe vizuri Kitengo cha Manunuzi alicho sema *PPU*, akiimarishe kwa kuajiri wataalam waliobobe na kuweka Mkurugenzi anayeshughulikia sera. Sasa hivi Wizarani hakuna Mkurugenzi anayeshughulikia Sera ya Manunuzi, kwa hiyo, aweke Mkurugenzi na Wataalam waliobobe katika Kitengo hicho cha *PPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara ilifanya jambo zuri mwaka 2006, kwa kupeleka wataalam wa fedha katika kila Halmashauri. Wataalam wa manunuzi wanalegalega na huko ndiyo fedha nyingi za *D by D* zinakwenda. Kuna *DEDs* wengi sio wote, lakini wengine wakiwa huko Wilayani na kwenye Halmashaurini kama miungu wadogo, wanatumia fedha za umma bila kujali Sheria ya Manunuzi. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, sasa hivi aimarishe na wataalam wa manunuzi katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitazungumzia nidhamu ya matumizi. Nitatoa mifano ambayo inaonekana; mwaka 2006 nilikwenda *International Motors* kutembea, nikakuta kuna magari mawili *Lexus Saloon*; nikauliza ya nani haya, wakasema kuna Wizara imeagiza kutoka Japan. Nikauliza ya kutumia nani? Wakasema Wakurugenzi na watu wengine, sio Waziri wala si Naibu Waziri, *Lexus* ambayo wakati huo moja ilikuwa Sh. 120m.

Sasa hayo si matumizi mazuri ya fedha, *Lexus* unakwenda nayo wapi? Hata nikiziona Dar es Salaam, nasema kuna watu wengine hawana nidhamu kweli katika kutumia fedha za walipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri aangalie jambo hili; jambo lenyewe dogo tu, utakuta katika Wizara Waziri ananunuliwa VX na wataalam, sawa na Naibu Waziri pia ananunuliwa VX; kuna sababu kweli kwa nini Naibu Waziri asinunuliwe GX? K

Katika hilo, napenda nimpongeze Mheshimiwa mtoya hoja, kwa sababu katika Wizara yake, Waziri anatumia VX na Manaibu Waziri wawili wanatumia GX, wamesevu fedha hapo; maana yake tofauti kati ya VX na GX ni karibu Sh. 30m.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naye anatumia VX lakini Naibu wake anatumia GX. Waziri wa TAMISEMI naye nampongeza vilevile mwenyewe anatumia VX na Naibu wake anatumia GX. Pia nampongeza Waziri wa Ulinzi yeye anatumia VX Naibu wake anatumia GX, lakini Mawaziri wengine, Waziri VX Naibu Waziri VX. Hapo naona nidhamu ya matumizi kidogo inakuwa si nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004. Tumesikia jana, Mheshimiwa Rais akiiongelea Sheria hiyo kwamba, kuna upungufu mkubwa sana na amesema Serikali ipo katika mpango wa kuidurusu sheria hiyo.

Namwomba sana Mheshimiwa mtoya hoja, asiwe na haraka katika kuidurusu aangalie marefu na mapana, aangalie mahusiano kati ya *PPU*, *PPRA* na *PPAA* na wadau wengine katika kuidurusu sheria hiyo ili yasije kutokea matatizo mengine kama yaliyotokea kwenye *Richmond* na kwenye vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba waidurusu sawasawa ili izibe mianya yote, ifike mahali ambapo kwa mfano, kwenye *Ministerial Tender Board* sawa kuna Mawaziri, kuna wengine ni Maafisa wa Serikali sawa, lakini hakuna Wataalam wa Manunuzi. *PPRA* ikipeleka ushauri wake, inapeleka ushauri na si amri, sasa ile *Tender Board* inaweza kukubali au kukataa ushauri wake kama ilivyokataa kwenye *Richmond*.

Kwa hiyo, naomba katika kuidurusu sheria hii, angalau kuwepo na kitu ambacho kikitoa ushauri uwe ni wa lazima, iimarishwe hii *PPU* ili ikitoa ushauri kwenye *Ministerial Tender Board* uwe ni wa lazima kwa sababu kutakuwa kuna Wataalam wa Manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba katika kuidurusu sheria hii, waangalie na *disposal*, maana yake Sheria ya Manunuzi si ku-*acquire* tu hata *disposal*; nitazungumza hapa, tumenunua magari ya Serikali magari sitini, sawa tumetangaza tenda

halafu tumenunua magari hayo, tunayatumia miaka minne au mitano, je, tunapoyauza tunayaauza vipi, nayo lazima iwepo katika *procurement*.

Unaamua tu kwamba, namuuzia Mkurugenzi yule pale au namuuzia karani yule pale hapana, lazima ufuate utaratibu. Kwa hiyo, naomba itakapokuwa inadurusiwa sheria hii, mambo yote hayo yaangaliwe kwa upana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nizungumzie kuhusu misamaha ya kodi. Mheshimiwa Mungai amesema kwamba, anaipongeza Serikali kwa kupunguza utegemezi kwa wahisani. Kwa mwaka huu, utegemezi umekuwa asilimia thelathini na nne, lakini mapato ya nchi yanayokusanya misamaha ya kodi ni asilimia thelathini, utegemezi thelathini na nne, misamaha ya kodi asilimia thelathini. Mheshimiwa Waziri alipoteuliwa tu alionyesha nia, alipotembelea taasisi zake mbili, tatu katika hotuba zake. Nilimfuatilia, alionyesha nia ya kuliangalia suala hili la misamaha ya kodi, ifike mahali ambapo *incentives* za *FDIs* ziwe nyingine si lazima ziwe misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri aangalie katika nchi nyingine, zipo nchi ambazo hazina misamaha ya kodi na zina-*manage* uchumi wao vizuri. Nchi zenyewe ni kama Uganda na Ghana kama sijakosea. Kwa hiyo, naomba *drive* yake ambayo alikuwa ameanza nayo Mheshimiwa Waziri katika kuiangalia upya misamaha ya kodi aendelee nayo ili katika bajeti zijazo, iwe imepungua kabisa au kufutwa kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu fedha za *EPA*. Sitaki kuiongelea Hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa sababu Mheshimiwa Spika amesema leo asubuhi kwamba, itabidi tupange siku maalum ya kuiongelea. Ilinifurahisha sana pale Mheshimiwa Rais aliposema kwamba, fedha hizi sasa ziende kwanza kuongeza Mfuko wa Ruzuku ya Mbolea na nyingine ziende kwenye mikopo ya wakulima.

Kwa hiyo, naomba hilo Mheshimiwa Waziri alichangamkie haraka sana ili lianze katika msimu huu ambao unaanza mwaka huu wakulima wetu waweze kufaidika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza sana Serikali kwa kuuza hisa zake katika Benki ya *NMB* kwa asilimia ishirini na moja. Nami naungana na wenzangu kwamba, hizi asilimia ishirini na moja ziende kwa wananchi na zile asilimia tano zitoke kwenye asilimia thelathini za Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kipindi hiki ambacho *IPO* imeshatangazwa, zimetoka taarifa kutoka kwenye Mabenki ya Biashara na kwa Mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam kwamba, Benki Kuu imetoa agiza kwa Mabenki ya Biashara kwamba, Mabenki ya Biashara yasitoe mikopo kwa wateja wake ili wakanunue hisa hizo, kwa sababu wateja wakikopa kwenye hizo Benki za Biashara wanatumia *collateral* kama hisa. Kwa hiyo, imeagiza Benki za Biashara zote zisitoe mikopo kwa wateja wake ili wanunue hisa.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie hilo kwa sababu kama itakuwa hivyo, ina maana watakaofaidika na *IPO* hii ni makundi haya ya jamii yetu, ambao wana fedha taslimu ambao ni jamii moja kama Waasia. Watafaidika wale ambao wamepata fedha zao kwa njia isiyo halali, wanaogopa kuzipeleka benki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni kweli tunawahukumu hawa wafanyakazi, wakulima na wafanyabiashara, ambao ni waaminifu (si mafisadi) kwamba, wasiweze kununua hisa bali inunue tu jamii moja.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa mto hoja atakapokuwa anahitimisha hoja yake, aliambie Bunge hili je, atakuwa anatenda haki hapa kama ni kweli Benki Kuu imetoe amri hiyo ya kutotoa mikopo kwa wateja wake bali wakanunue *share NMB?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nampongeza sana mto hoja na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. Nikuhakikishie ulipokuwa unaorodhesha mashangingi watu wengi walishangaa sana.

Mheshimiwa Dr. Gama, ndiye atakayekuwa mzungumzaji wetu wa mwisho.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Labda nami mwanzo wa yote, naomba kusema naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Vilevile napenda niwapongeze Mawaziri, jinsi wanavyofanya kazi yao vizuri katika Wizara hii na kusimamia mapato. Nawapongeza sana na hasa Mawaziri ambao wapo karibu na Wabunge na Wananchi kwamba, wakipata tatizo wanawaendea na wao huwasaidia bila kigugumizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze *TRA* chini ya kaka yetu Kitilya, kwa makusanyo mazuri. Jana Mheshimiwa Rais alipokuwa anasema mwili ulinisisimka jinsi wanavyokusanya vizuri. Naomba niwapongeze na nawaambia wasikate tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi *TRA* kuna watu wazuri lakini kuna wengine hawafanyi vizuri, mfano wangu na naomba nitaje *openly* na nitakapotakiwa kutoa ushahidi nipo tayari ku-*present*. Kwa mfano, kuna baadhi ya *assessors* hasa Kibaha wana-assess lakini wanatoa taarifa ambayo si sahihi. Mtu anaandika ripoti na ninayo ripoti anasema, nimepata ushahidi huu na huu lakini ushahidi ule ukiutazama si wa kweli ni wa uongo. Nitampalekea ndugu yangu Kitilya na nilishamwambia kuna *assessor* ambaye anahujumu watu na kwa hili nitaleta ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba nikubaliane na Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na Wizara hii, ucheleweshwaji wa miongozo ya bajeti. Hili lisichukuliwe kiurahisi rahisi, tumesema bajeti yetu ni shirikishi; nikisema bajeti shirikishi si tu kwa

Madiwani na Wabunge bali ni kuanzia kule ngazi ya chini. Mwaka huu nimepata uthibitisho na *experience* ambayo nimeona niizungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeandaa kuzunguka katika Kata zangu mwezi wa tatu, lakini katika mwezi wa Pili nilitaka kukaa na Mkurugenzi, kaundaa ratiba akasema ameitwa Dodoma kwenda kupata miongozo ya bajeti. Mwezi wa Tatu wakati nafanya ziara yangu sikupata wataalam kutoka katika Halmashauri yangu, nikaambiwa wanatengeneza bajeti, nikauliza wanatengeneza bajeti wameshirikisha wananchi lini kutoka kwenye mitaa yangu, kwangu kuna mitaa. Nikaambiwa wameshirikisha. Nikasema kama miongozo wamepewa mwezi wa Pili na nakwenda mwezi wa tatu, nimezunguka ukiacha Kata moja tu, lakini Kata ya Kibaha nilikuta hawajakwenda kupeleka mapendekezo yao katika *WDC* ili iende huko kwenye Halmashauri wakati huo Halamshauri inapanga bajeti, wataalam wako pale, wengine walishindwa kuja katika ziara yangu kwa sababu ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikafikiri kwamba tatizo lipo kwenye Halmashauri yangu tu, bahati nzuri nikapata bahati kwenda katika Kata moja ambayo inaitwa Machochwa, ipo katika Jimbo la kaka yangu hapo, Naibu Waziri wa Mifugo kama sikosei, Mheshimiwa Wanyancha, nimekwenda Kata ile na ni Kata ya Mwenyekiti wa Halmashauri, katika kuzunguka kwenye masuala ya siasa (*NEC*) nikawa na *interest* kuona wananchi wameshirikishwaje. Mwenyekiti wa Halmashauri akasema sijaizungumza hata katika *WDC* lakini wakati huo ni mwezi wa Nne maandalizi yameshaanza. Kwa hiyo, naomba kusema hili suala la kupeleka miongozo inavyocheleweshwa inawafanya wananchi wasishiriki katika kupanga bajeti. Hilo nilikuwa nataka nisaidie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu *expenditure tracking system*. Kuna *NGOs* zimejitokeza kusaidia kuelimisha Madiwani, Viongozi wa kwenye Mitaa na wengine Vijijini. Hawa wanasadida kuwaelimisha wananchi jinsi ya kufuatilia, lakini inatokea bahati mbaya baadhi ya Halmashauri hawawapi nafasi; wamepata fedha, wanakuja na semina ili kuwaelimisha watu lakini baadhi ya Wakurugenzi wanakataa kwa sababu wanajua wananchi wakipata habari watafutilia. Naomba hizi *NGOs* zipewe msaada ili ziisaidie Serikali katika suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi. Vitabu hivi vinatoka kwa Wabunge tu ni vidogo, Madiwani hawapati na wananchi hawapati, wengine kuweza ambao ni watu wa mijini wanapata magazeti lakini kule vijijini yakifika wengine hawana hela, magazeti hayafiki huwa wanatoa taarifa ya mkaguzi.

Sasa naomba tuwe na utaratibu, hivi vitabu sijui tufanyeje hata ikiwezekana basi itokee ile *page* tu inayohusu Wilaya au Halmashauri husika ili wananchi wapewe. Nashauri kama hatuwezi kupeleka katika kila Kata tufanye hivi. Siku ya magilio basi nasi tunaweka bango letu tunawaeleza watu, mtu akija kununua vitu gulioni anawenza kusoma. Nilikuwa naomba nitoe ushauri huo katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la *value for money audit*, wanasema eti mpaka mkubaliane na Halmashauri ili mwende kule katika Kitengo cha Mdhibiti na Mkaguzi kisha waje wakague hapana, ningeomba mtu kama una jambo Halmashauri wakikataa mtu binafsi aweze kuomba audit hii kufanya mfano wa kwanza mkubwa katika hili ni barabara zetu.

Fedha nyingi zinatumika katika barabara, lakini utakuta haijapita hata gari moja barabara hizo zimeshaharibika. Sasa naomba hiki kitengo kisingojee hadi Halmashauri wakubali, kuna wakati mwingine wao ndio wahusika wanaweza kukataa. Basi mtu akiwa na dukuduku au hana uhakika, akawaombe waje kutazama na hii itawasaidia sana kuliko kungojea watu wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye suala zima la Sheria ya Manunuzi. Naomba idara hii isaidiane na TAMISEMI, fedha nyingi zinapelekwa kwenye Halmashauri, lakini sheria hii ya mikataba na nini nafikiri ina upungufu. Unaambiwa kuna Bodi, Madiwani wasishiriki nakubaliana nayo sina tatizo, lakini Madiwani wasishiriki unamwambia Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti asaini umeshamshirikisha, lakini anasaini katika jambo ambalo hakukaa na ye ye akajua na kuchambua, anambiwa tu saini naye anasaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku alichosaini hajui, ukiacha wachache ambao kweli wanaweza kufuatilia. Unakuja wakati sasa shughuli zinatendeka unacheka naye; anajiuliza hivi ilikuwa hili? Unamwambia wewe si ulisaini. Hili siliendelezi kwa sababu hata Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI analijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mtindo uliopo sasa hivi ndani ya mabenki. Bahati nzuri wameanzisha kitu kinaitwa *credit card*, nashukuru sana. Sasa badala ya wananchi kubeba fedha kuna *credit card*, lakini ni maduka mangapi au sehemu ngapi za biashara zinatumia *credit card*, kule vijijini hakuna kabisa. Sasa tutafute mtindo mzuri; ni aibu mtu hata ukiwa unasafiri nje huku umebeba dola zako elfu tatu mkononi. Sasa tuutafute mtindo mzuri ili suala hili la *credit card* liweze kutumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la *credit card* nakubaliana nalo sana, lakini mabenki yetu nayo ni machache na yapo mijini tu. Tunazungumzia *money laundering*, huyu mtu yupo kijijini anaweza kupata fedha zake akazichukua na kuziweka hakuna benki, akaanza kununua. Wananchi wetu mpaka sasa bado wanaweka pesa zao katika mitungi, kwa sababu hakuna benki, abebe fedha zake aende mpaka mjini, benki nyingi zipo huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili tulirekebishe kwa sababu ni kama tumewarudisha nyuma kidogo wananchi wetu. Naomba niulize zile shilingi bilioni moja ambazo wanaziita pesa za JK; kwa sababu muda wa Mheshimiwa Waziri utakuwa mchache, anieleze kwa maandishi ni wakulima wangapi wamefaidika kwa pesa hizi? Hili nalisisitiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye Benki ya *NMB*. Nashukuru sasa zile *shares* zinauzwa, wakati *NBC* inagawanywa wale wafanyakazi waliokuwa hawakupelekwa *NMB* walilipwa marupurupu yao. Sasa hivi benki hii imeanza kuza *shares* hata kama imebaki asilimia thelathini; kwa nini hawa wafanyakazi waliokuwepo *NMB* wasilipwe *share* zao waanze mikataba mipy? Hili ni lalamiko la wafanyakazi wengi, Serikali wamekataa lakini nawasihi sana walipeni fedha zao ili waanze mikataba mipy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu *Citi Bank*. Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikwenda *Citi Bank* nikiwa mshamba, naomba niseme hivi hivi na Ubunge wangu lakini nikiwa mshamba.

Nilikwenda kule *Citi Bank*, nikasema mwananguanasoma nje, nataka nichukue fedha na *documents* zangu zote ili apelekewe, akaunti yake ni ya *Citi Bank*. Unajua waliniambiaje? Walisema *Citi Bank* haichukui *individuals* inachukua wafanyakabiashara. Sasa jamani mbona mabenki yanabagua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipoambiwa vile nikasema sasa nataka kufungua akaunti, nikaambiwa hapana wewe siyo mfanyakabiashara. Kwa hiyo, kuna mabenki yamekuja kwa ajili ya wafanyakabiashara na kuna mabenki yamekuja kwa ajili ya wananchi. Naomba kama *Citi Bank* kwengine wananchi wa nchi hizo wanaweza kuweka akaunti; kwa nini na kwetu isiwe hivyo?

Naona Waziri anacheaka lakini hii ni *serious*; kwa nini benki nydingine zinaombwa ziwape wananchi lakini benki nydingine wanasema za wafanyakabiashara? Nasema benki zimekuja katika nchi hii ili kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi, lakini bado nasisitiza tena kuhusu huyu ndugu yangu Afisa Mkadiriaji, nina ushahidi kwanza ilinihusu mimi, siisemi ya kwangu kwa sababu nilisha-*deal* nayo vizuri, lakini juzi juzi nimethibitisha kumbe amezoea, anawakadiria watu vibaya sijui ili wamhonge, lakini ameingia kwenye suala la Serikali *officially* akasema vibaya. Sasa nimesema nitampa Ndugu Kitilya na nitampa Mheshimiwa Waziri, lakini kama kuna watu wengi wa aina hii wanawanyanya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia tena kusema kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda haututoshi kuendelea na zoezi hili, wachangiaji kwa kweli ni wengi; wakati ule naanza nilikuwa na wachangiaji kumi na nne na mpaka sasa hivi bado kumi na nne, maana yake wameongezeka wengine; kwa hiyo, bado mchango wetu utakuwa ni mkubwa tu kwa Wizara hii Siku ya Jumatatu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru kwa ushirikiano ambao tumekuwa nao kwa wiki nzima hadi leo Ijumaa. Naomba nitaarifu tu kwamba, shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa siku ya leo zimekamilika kufuatana na *Order Paper* yetu.

Kwa hiyo, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kikao cha hamsini na mbili cha tarehe 25 Agosti, 2008, yaani Jumatatu, saa tatu asubuhi na ili nisisahau kama jana, naomba kuahirisha kikao hiki. (*Kicheko*)

(*Saa 01.34 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,
Tarehe 25 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)